# KUCHUNGUZA ATHARI ZA KIFONOLOJIA ZA LUGHA YA KIHAYA KATIKA KUJIFUNZA LUGHA YA KISWAHILI

**ASIMWE ABEL**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

# UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma Tasnifu hii inayoitwa: "***Kuchunguza Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kihaya Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili" "*** na anapendekeza ikubaliwe kwa ajili ya Kukamilisha sehemu ya masharti ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili (MA. Kiswahili – Isimu) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Dkt. Hanna J. Simpassa

**(Msimamizi)**

Tarehe

# HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kukaririwa au kuhawilishwa kwa mbinu ya kielektroniki kama kunakili, kutoa kopi au kurudufu Sehemu yoyote ya tasnifui hii bila ya idhini kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

## TAMKO

Mimi **Asimwe Abel,** ninatamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii ya utafiti iitwayo **"*Kuchunguza Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kihaya Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili*"** ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa popote pale kwa lengo la kutunukiwa shahada yoyote katika Chuo Kikuu chochote.

Sahihi

Tarehe

## TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa mume wangu mpendwa Grayson M. Mutazamba. Kwa kunipa nafasi ya kusoma na kunitegemeza kiuchumi hadi kufikia mafanikio haya ya kitaaluma.

## SHUKURANI

Matokeo na mafanikio ya kazi hii yametokana na michango na mawazo ya watu na taasisi mbalimbali. Kwa hakika si rahisi vikundi vyote kuvitaja au kutaja majina yao kwa kila aliyehusika. Hata hivyo nalazimika kuwataja wachache walioshiriki kwa namna moja ama nyingine kufanikisha utafiti huu.

Awali ya yote sina budi kumshukru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, afya na akili njema iliyonisaidia kuifanya kazi hii kwa wepesi.

Pili, namshukuru msimamizi wangu Dkt. Hanna J. Simpassa kwa juhudi zake kubwa za kuniongoza katika mchakato huu na kunifanya niione kazi hii ni nyepesi japo ilikuwa ngumu. Alinivumilia katika madhaifu mbalimbali yaliyokuwa yakijitokeza kwangu kama mwanadamu na mwanafunzi wake alisimama upande wangu ili niweze kuifanya kazi hii vizuri. Kila wakati hakuchoka kunishauri na kuniongoza katika kuhakikisha namaliza kazi hii kwa muda uliopangwa, Mungu ambariki sana.

Tatu, Naushukuru uongozi na wafanyakazi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, tawi la Dar es Salaam kwa kunipa fursa ya kufanya utafiti kwa muda muafaka na katika eneo ambalo nililipendekeza kufanyia utafiti. Pia nawashukru kwa kunipangia msimamizi mzuri Dkt. Hanna J. Simpassa, bila kuwasahau wahudumu wa maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania - Dar es Salaam kwa jinsi walivyoweza kunisaidia kwa kunipatia kila maandiko na vitabu ambavyo vilikuwa vinaendana na kazi yangu ya utafiti. Ushirikiano huo ulinifanya kukamilisha kazi hii kwa wakati hasa kipindi cha kuandika pendekezo la mswada na wakati wa kuchambua data

Nne, napenda kuishukru ofisi ya afisa elimu wa wilaya ya Missenyi idara ya shule ya msingi kwa kunipatia kibali cha kufanya utafiti katika baadhi ya shule zake za msingi. Barua yake ya utambulisho kwa walimu wakuu ilinipatia upenyo mkubwa sana katika shule husika, pia niwashukru walimu na wanafunzi wa shule za msingi Kigazi, Nyakahanga, Kalagala, Minziro, Kiwelu, na Kyanumbu kwa ushirikiano wao walionipa katika ukusanyaji wa data za utafiti. Mawazo yao ndiyo yaliyowezesha kazi hii kukamilika kwa wakati.

Tano, nawashukuru wanafunzi wenzangu wote wa (M.A Kiswahili – Isimu, 2017/2018) kwa ushirikiano wao walionipa wakati wote wa masomo yetu hususan katika mijadala mbalimbali ya kitaaluma iliyokuwa inaibuka darasani. Mijadala hiyo ilinipa mwanga wa kuanza kuyaona mambo kwa mtazamo tofauti na ni katika mijadala hiyo imenipatia chachu katika uandishi wa tasnifu hii.

Sita, Naishukuru familia yangu kwa ujumla kwa kuniunga mkono na kunionesha uvumilivu mkubwa wakati wote wa masomo. Michango ya mawazo na ushauri wao mzuri uliniwezesha kuwa na moyo wa kuendelea na utafiti huu pasipo kukata tamaa licha ya kukabiliwa na majukumu mengi ya kitaifa na kifamilia.

## IKISIRI

Tasnifu hii ilichunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwa jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kihaya katika wilaya ya Misenyi. Wataalamu wengi wanakubaliana kuwa lugha zinapokutana huwa zinaathiriana kwa namna moja au nyingine. Kwa hivyo utafiti huu ulichunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kiswahili katika jamii ya Kihaya. Eneo lililohusika katika utafiti huu ni wilaya ya Missenyi, mkoani Kagera. Njia zilizotumika kuwapata watafitiwa ni usampulishaji makusudi na nasibu. Usampulishaji makusudi ulitumika kwa walimu wanaofundisha darasa la awali hadi darasa la tatu na walimu wakuu wa kila shule. Usampulishaji nasibu ulitumika kwa wanafunzi wote, walimu wanaofundisha darasa la nne hadi darasa sita, na wazazi wa vijiji husika. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia iliyoasisiwa na mwanaisimu Vennemann (1971) ingawa baadaye iliendelezwa na (Hooper, 1971). Nadharia hii imetumiwa ili kubaini namna lugha ya Kihaya ilivyoathiri lugha ya Kiswahili katika jamii ya Kihaya. Katika ukusanyaji wa data kutoka katika eneo la utafiti, mtafiti alitumia njia ya mahojiano na dodoso. Jumla ya watafitiwa 297 walihusika katika utafiti huu, kati yao wanafunzi walikuwa 239 sawa na asilimia 80.5% ya watafitiwa wote waliohusika, idadi nyingine ya 58 walikuwa walimu, na wazazi. Utafiti umeonesha kwamba, lugha ya awali ina nguvu ya kuathiri kifonolojia ya mtoto hata anapojifunza lugha ya pili. Ili kumsaidia mwanafunzi kujifunza lugha ya pili walimu na jamii nzima inabidi kushirikiana kwa karibu katika kumsaidia mwanafunzi kutamka maneno kwa lafudhi sahihi ya Kiswahili.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ..... ii

**HAKIMILIKI** ..... iii

**TAMKO** ..... iv

**TABARUKU** ..... v

**SHUKURANI** ..... vi

**IKISIRI** ..... viii

**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... xv

**ORODHA YA VIELELEZO** ..... xvii

**ISHARA ZILIZOTUMIKA** ..... xviii

**SURA YA KWANZA** ..... 1

**UTANGULIZI** ..... 1

1.1 Usuli wa Mada ..... 1

1.2 Tatizo la utafiti ..... 3

1.3 Malengo ya Utafiti ..... 3

1.3.1 Lengo Kuu ..... 3

1.3.2 Malengo Mahsusi ..... 3

1.4 Maswali ya utafiti ..... 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti ..... 4

1.6 Vikwazo vya Utafiti ..... 5

1.7 Mipaka ya Utafiti ..... 6

1.8 Mpangilio wa Tasninfu ya Utafiti ..... 6

1.9 Hitimisho ..... 7

**SURA YA PILI ........................................................................................................ 8**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA NADHARIA ............................................ 8**

2.1 Utangulizi ........................................................................................................ 8

2.2 Historia ya Jamii ya Wahaya ........................................................................... 8

2.3 Kazi Tangulizi ................................................................................................ 10

2.3.1 Athari ya Lugha ya Kwanza kwa ya Pili ...................................................... 10

2.3.2 Athari za Kifonolojia za Lugha za Kibatu katika Kiswahili............................ 13

2.3.3 Sababu Zinazofanya Lugha za Kibatu Ziweze Kuathiri Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili ........................................................................ 17

2.3.4 Makosa Wanayofanya Wanafunzi Wanapojifunza Lugha ya Kiswahili ...................................................................................... 18

2.4 Fonimu za Kiswahili...................................................................................... 20

2.4.1 Fonimu za Irabu/Vokali za Kiswahili Sanifu ................................................ 21

2.4.2 Irabu za Kiswahili Sanifu na Sifa zake Bainifu............................................. 23

2.4.3 Fonimu za Nusu Irabu za Kiswahili Sanifu /Viyeyusho ................................ 24

2.4.4 Sauti za Irabu za Kihaya ................................................................................ 24

2.4.5 Konsonanti za Kiswahili Sanifu .................................................................... 24

2.4.6 Konsonanti za Lugha ya Kihaya.................................................................... 26

2.5 Nadharia za Utafiti.......................................................................................... 28

2.5.1 Nadharia ya Konsonanti Vokali...................................................................... 28

2.5.2 Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia.............................................................. 29

2.6 Pengo la Utafiti ............................................................................................... 31

2.7 Hitimisho ........................................................................................................ 32

**SURA YA TATU .......... 33**

**MBINU ZA UTAFITI .......... 33**

3.1 Utangulizi .......... 33

3.2 Eneo la Utafiti .......... 33

3.3 Sampuli ya Watafitiwa .......... 34

3.4 Sampuli .......... 36

3.5 Usampulishaji .......... 37

3.5.1 Usampulishaji Lengwa .......... 37

3.5.2 Usampulishaji Nasibu .......... 38

3.6 Mkabala wa Utafiti .......... 39

3.7 Vyanzo vya Data .......... 40

3.7.1 Data za Msingi .......... 40

3.7.2 Data za Upili .......... 40

3.8 Mbinu za Ukusanyaji wa Data .......... 41

3.8.1 Hojaji .......... 41

3.8.2 Mahojiano .......... 43

3.8.3 Mbinu ya Maktabani .......... 45

3.9 Uchanganuzi wa Data .......... 45

3.10 Hitimisho .......... 46

**SURA YA NNE .......... 47**

**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA .......... 47**

4.1 Utangulizi .......... 47

4.2 Taarifa za Awali za Wahojiwa .......... 47

4.2.1 Jinsia ya Wahojiwa .......... 47

4.2.2 Umri wa Wahojiwa ........................................................................ 48

4.2.3 Elimu ya Wahojiwa ........................................................................ 50

4.2.4 Hadhi ya Ndoa ........................................................................ 51

4.2.5 Kabila ........................................................................ 52

4.3 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data ........................................................................ 53

4. 4 Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kihaya katika Kujifunza Kiswahili ........................................................................ 53

4.4.1 Kushindwa Kutamka Sauti ........................................................................ 53

4.4.1.1 Sauti / ð / Kutamkwa Kama Sauti /z/ ........................................................................ 54

4.4.1.2 Sauti /Ɵ/ Kutamkwa kama Sauti /S/ ........................................................................ 55

4.4.1.3 Sauti / γ / Kutamkwa kama Sauti /g/ ........................................................................ 57

4.4.1.4 Sauti /ng/ Kutamkwa kama Sauti / ŋ/ ........................................................................ 58

4.4.1.5 Sauti /tʃ/ Kutamkwa kama Sauti /ki/ ........................................................................ 60

4.4.1.6 Sauti /l/ Kutamkwa Kama Sauti /r/ ........................................................................ 61

4.4.1.7 Sauti / ʧ / Kutamkwa Kama Sauti /kya/ ........................................................................ 62

4.4.2 Uchopekaji wa Silabi Mwanzoni mwa Neno ........................................................................ 63

4.4.3 Kuongeza Viambishi Visivyohitajika katikati mwa Neno ........................................................................ 65

4.4.4 Kuongeza Viambishi Mwishoni mwa Neno ........................................................................ 66

4.4.5 Kupunguza Viambishi katika Maneno ........................................................................ 67

4. 5 Sababu Zinazofanya Lugha ya Kihaya iweze Kuathiri Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili ........................................................................ 69

4.5.1 Kukosekana kwa Baadhi ya Sauti Katika Lugha ya Kihaya ........................................................................ 69

4.5.2 Ndimi za Wanafunzi Kuathiriwa na Lugha ya Kihaya ........................................................................ 70

4.5.3 Uhusiano wa Karibu kati ya Lugha ya Kihaya na Kiswahili ........................................................................ 72

4.5.4 Wanafunzi Kukosa Muda wa Kufanya Mazoezi ya Kutosha Kuzungumza Sauti za Lugha ya Kiswahili ... 73
4.5.5 Upungufu wa Walimu wa Somo la Kiswahili ... 75
4.5.6 Mikakati Duni ya Ufundishaji ... 75
4.5.7 Mazingira Duni ya Kujifunza Lugha ya Kiswahili ... 77
4.5.8 Jamii ya Kihaya Kutoona Umuhimu wa Kutumia Lugha ya Kiswahili ... 77
4.5.9 Ukongwe wa Lugha ya Kihaya Ndani ya Jamii ... 80
4.5.10 Kihaya Kupewa Matumizi Makubwa ya Katika Shughuli za Kijamii ... 81
4.5.11 Lugha ya Kihaya Kutumika kama Utambulisho nje ya Jamii ... 84
4.5.12 Lugha ya Kihaya Kutumika kama Sehemu ya Kudumisha Utamaduni wa Jamii ... 86
4.6 Mbinu za Kuwasaidia Wanafunzi wa Kihaya Wanaojifunza Lugha ya ... 87
Kiswahili ... 87
4.6.1 Watoto Wafundishwe Lugha ya Kiswahili Tangia Utotoni ... 88
4.6.2 Kuwepo na Uwiano Mzuri kati ya Walimu na Wanafunzi Shuleni ... 89
4.6.3 Matumizi Sahihi ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia ... 89
4.6.4 Kuepuka Matumuzi ya Lugha Mbili za Kufundishia ... 91
4.6.5 Mwalimu Atumie Lugha ya Kiswahili Fasaha ... 95
4.6.6 Wazazi Waweke Kipaumbele cha Kuzungumza Lugha ya Kiswahili ... 96
4.7 Hitimisho ... 96
**SURA YA TANO ... 97**
**MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ... 97**
5.1 Utangulizi ... 97

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........................................................................ 97

5.3 Mapendekezo ya Utafiti ......................................................................................... 99

**MAREJELEO ............................................................................................................. 101**

**VIAMBATISHO ......................................................................................................... 107**

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 2.1: lrabu za Kiswahili Sanifu na Sifa zake Bainifu ..............................23

Jedwali Na. 2.2: Sauti za Irabu za Kihaya ................................................................24

Jedwali Na. 2.3: Konsonanti na Nusu Irabu za Kiswahili .........................................25

Jedwali Na. 2.4: Konsonanti za Lugha ya Kihaya .....................................................26

Jedwali Na. 2.5: Alfabeti za Kiswahili.......................................................................27

Jedwali Na. 3.1: Idadi Halisi ya Wanafunzi kwa kila Shule na Waslimu wa Kiswahili ..........................................................................................35

Jedwali Na. 3.2: Idadi Halisi ya Wahojiwa (297) ......................................................37

Jedwali Na. 3.3: Usampulishaji Lengwa....................................................................37

Jedwali Na. 3.4: Idadi ya Wahojiwa kwa Njia Nasibu ..............................................38

Jedwali Na. 3.5: Idadi ya Wanafunzi Walioteliwa katika Utafiti ..............................39

Jedwali Na. 4.1: Jinsia ya wahojiwa .........................................................................48

Jedwali Na. 4.2: Umri wa Wahojiwa .........................................................................49

Jedwali Na. 4.3: Elimu...............................................................................................50

Jedwali Na. 4.4: Hadhi ya Ndoa.................................................................................52

Jedwali Na. 4.5: Kabila ..............................................................................................52

Jedwali Na. 4.6: Sauti / *ð* / Kutamkwa kama Sauti /z/..............................................55

Jedwali Na. 4.7: Sauti /Ɵ/ Kutamkwa kama Sauti /S/................................................56

Jedwali Na. 4.8: Sauti / γ / Kutamkwa kama Sauti /g/...............................................58

Jedwali Na. 4.9: Sauti /ng/ Kutamkwa kama Sauti / ŋ/............................................60

Jedwali Na. 4.10: Sauti /tʃ/ Kutamkwa kama Sauti /ki/..............................................61

Jedwali Na. 4.11: Sauti /l/ Kutamkwa Kama Sauti /r/.................................................62

Jedwali Na. 4.12: Sauti / ʧ / Kutamkwa Kama Sauti /kya/ .........................................63

Jedwali Na. 4.13: Kuongeza Viambishi Visivyotakiwa Mwanzoni mwa Neno ..........65

Jedwali Na. 4.14: Kuongeza Viambishi Visivyotakiwa katikati mwa Neno ...............66

Jedwali Na. 4.15: Kuongeza Viambishi Tamati Visivyotakiwa..................................67

Jedwali Na. 4.16: Kupunguza Viambishi katika Maneno ............................................68

Jedwali Na. 4.17: Matumizi ya Sauti /l/ Badala ya /r/..................................................75

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 3.1: Ramani ya Wilaya ya Missenyi......................................................34

## ISHARA ZILIZOTUMIKA

/    / Mabano ya fonetiki.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Lugha ya Kiswahili chimbuko lake ni upwa wa Afrika Mashariki. Lugha hii awali ilianza kutumiwa na watu wachache walioishi mwambao wa Afrika Mashariki. Leo hii lugha ya Kiswahili imekua na kuenea kwa haraka katika bara la Afrika, Ulaya, Marekani, Asia na Australia. Ghanen (2005), anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa barani Afrika. Kwa ukubwa wake inafaa kabisa kuwa lugha ya kidiplomasia. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika maswala ya kidiplomasia yatakifanya Kiswahili kuenea kwa kasi kubwa zaidi na kupata wazungumzaji wengi kuliko ilivyo leo. Katika jamii zinazotumia lugha zaidi ya moja, mwingiliano kati ya lugha husika haukwepeki. Mtagusano wa lugha katika jamii yoyote ile huleta uwezekano mkubwa wa kuathiriana katika vipengele mbalimbali. Athari za aina hizi huweza kuwa za upande mmoja au pande mbili husika. Katika utafiti huu, mtafiti alichunguza athari za kifonolojia zinazojitokeza katika kazi za matamshi ya wanafunzi wazawa wa jamii ya Kihaya wanapowasilisha ujumbe kwa lugha ya Kiswahili.

Fonolojia ni tawi la isimu linalochunguza mifumo ya sauti za kutamkwa zinazotumika katika lugha asilia mahususi kwa binaadamu. Kama vile sauti za lugha ya Kiswahili, Kiingereza, Kigogo, Kihaya, Kisukuma, Kimakonde, na zinginezo. Kipashio cha msingi cha kifonolojia ni fonimu. Fonimu ni kipashio kidogo kabisa cha kifonolojia kinachoweza kubadili maana ya msingi wa neno. Hivyo basi, fonimu ina maana kwa kuwa inaweza kubadili maana ya neno inapobadilishana nafasi katika neno husika. Ni

fonimu chache zinateuliwa kutoka katika bohari la sauti ili zitumike katika mfumo wa sauti za lugha mahususi tu. Neno fonolojia, linatokana na maneno mawili ya Kigiriki ambayo ni "phone" ambayo ni sauti za kusemwa na "logos" ambayo ni taaluma. Kwa hiyo tunaweza kusema, fonolojia ni tawi la Isimu linalochunguza mifumo ya sauti kwa kuzingatia taaluma ya lugha husika. Masimulizi yanadai kuwa taaluma hii ilianza zamani sana kati ya mwaka 460 kabla ya Masihi huko India ya kale ambapo mtu aliyeitwa Panini, aliandika kuhusu fonolojia ya Kisankriti katika matini aliyoiita Shiva Sutras (Rubanza, 1979).

Watafiti wanadai kuwa fonolojia hupangwa katika mfumo maalumu kutegemeana na misingi ya lugha husika. Kimsingi, watafitiwa ambao wana umilisi katika lugha yao ya kwanza, huitegemea wakati wanapojifunza lugha ya pili. Kwa mujibu wa Richards (1974), tajriba ya mwanafunzi katika lugha ya kwanza huhamishiwa katika lugha ya pili kwa lengo la kurahisisha ujifunzaji wake. Uhamishaji wa aina hii husababisha kuwapo kwa makosa mbalimbali hususani iwapo mifumo ya lugha mbili husika ni tofauti.

Rubanza (Ameshatajwa) alichunguza uhusiano kati ya Kiswahili na Kihaya, aligundua kuwa kuna athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza katika matumizi ya Kihaya. Kati ya baadhi ya athari alizogundua ni baadhi ya watafitiwa wa jamii-lugha ya Kihaya kutumia matamshi ya Kihaya katika kuwasilisha ujumbe wao ilhali dhana husika zingeweza kutajwa kwa kutumia matamshi sahihi ya Kiswahili.Utafiti huu utaangalia athari za kifonolojia kutokana na lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili katika eneo la Missenyi, mkoani Kagera, ambako ni miongoni mwa jamii ya watu wanaozungumza lugha ya Kihaya.

## 1.2 Tatizo la utafiti

Lugha ndicho chombo kikubwa cha mawasiliano baina ya watu na watu au kundi na kundi au jamii na jamii. Maendeleo ya jamii yoyote yanatokana na matumizi madhubuti ya lugha ambao unakuwa na mfumo mmoja rasmi wa mawasiliano. Lugha yoyote lazima iwe na kanuni za watumiaji wa lugha husika zinazoonesha matamshi, lafudhi, na maana ili iwe rahisi wao kuwasiliana na wengine na kujifunza lugha hiyo. Kwenda kinyume na kanuni hizo kunaweza kuleta mkanganyiko kwa wazungumzaji wa lugha hizo.

Kwa kuzingatia uhusiano huo wa mwingiliano wa lugha ya awali katika kujifunza lugha ya pili, mtafiti ataangalia athari za kifonolojia kutokana na lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili katika eneo la Missenyi, mkoani Kagera.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

### 1.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

### 1.3.2 Malengo Mahsusi

(i) Kubainisha athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza Kiswahili.

(ii) Kuelezea sababu zinazoifanya lugha ya Kihaya iweze kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

(iii) Kubainisha mbinu za kutumia ili kuwasaidia wanafunzi wa Kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili.

## 1.4 Maswali ya utafiti

(i) Ni athari zipi za kifonolojia zinazojitokeza kwa wanafunzi wa Kihaya wakati wa kujifunza Kiswahili?

(ii) Ni sababu zipi zinazofanya athari za kifonolojia kutokea wakati wanafunzi wa Kihaya wanajifunza Lugha ya Kiswahili?

(iii) Ni mbinu zipi zinazoweza kutumika ili kuwasaidia wanafunzi wa Kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili kuepuka athari hizo za kifonolojia?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kwa kufanyika kwa utafiti huu, mtafiti analenga kutoa mchango ufuatao kwa jamii,

Moja, utafiti huu utatoa mwanga kwa jamii ya Kihaya katika kujua athari za kifonolojia ya lugha ya Kihaya kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi kirahisi athari hizo ili kupunguza ama kumaliza makosa ya kifonolojia katika kujifunza Kiswahili.

Mbili, Kwa upande wa taaluma, utafiti huu utapunguza pengo la kiutafiti juu ya athari za lugha ya Kihaya katika lugha ya Kiswahili ambalo kwa ufahamu wa mtafiti, hakuna utafiti uliofanyika kwa kina juu ya mada hii hususani katika wilaya ya Missenyi.

Tatu, matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kutoa msaada wa kitaaluma hasa kwa walimu wanaofundisha wanafunzi katika jamii ya Kihaya ili kutatua makosa endapo yatatokea wakati wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wanaozungumza Kihaya.

Nne, utafiti huu unatarajiwa kuwa kichocheo cha tafiti nyingine kuhusu kuathiriana kwa lugha mbalimbali za Kibatu na Kiswahili katika jamii za kitanzania.

## 1.6 Vikwazo vya Utafiti

Katika kukamilisha utafiti huu, mtafiti alikutana na vikwazo kadhaa ingawa alijitahidi katika kuhakikisha kuwa anavitatua ili kutoathiri mchakato wa ukusanyaji data. Baadhi ya vikwazo hivyo ni;

Kikwazo cha muda ambao ulikuwa tishio kwa mtafiti kwani wanafunzi wa darasa la saba walikuwa wameshamaliza shule, hata hivyo aliendelea na utafiti kwa wanafunzi wa darasa la awali hadi darasa la sita.

Ushirikiano kwa watafitiwa wanafunzi hasa wa darasa la awali ilikuwa shida sana kuwapata, hadi mwalimu wao wa darasa alipokuja kutoa msaada ndipo mtafiti aliweza kuendelea na kazi yake ya utafiti vizuri.

Wengi wa wanafunzi wanaosoma katika shule za msingi huwa ni waoga kuelezea mambo yao kwa wageni. Katika kukabiliana na changamoto hii, mtafiti alikuwa anatembea na mwalimu mwenyeji kwa ajili ya kumtambulisha kwa wanafunzi. Tatizo la kutoa taarifa pia liliweza kujitokeza kwa baadhi ya walimu wakihisi kuwa taarifa zao wanazotoa zinaweza kuwaathiri katika ajira zao hasa ikibainika kuwa wao ndio waliotoa taarifa hizo. Katika kukabiliana na hili tatizo, kabla ya kuanza kukusanya taarifa, mtafiti aliwapa maelezo mafupi kuhusu lengo la utafiti huu na kuwa utatumika kwa ajili ya kitaaluma tu na si vinginevyo, na mtafitiwa haruhusiwi kuandika jina lake mahali popote pale kwenye hojaji. Mtafiti aliweza kufanikiwa zaidi baada ya

kuonyesha barua kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambayo ilikuwa na jina la mtafiti na kichwa cha utafiti, na eneo la kufanyia utafiti, pia mtafiti alikuwa na barua kutoka ofisi ya afisa elimu wilaya idara ya shule za msingi ikiwataka walimu wa shule husika kumpa mtafiti ushirikiano katika kufanya utafiti.

Pia kuna wanafunzi ambao hawajui au hawakuweza kujieleza vizuri kwa kuandika, ambapo mtafiti ilibidi kutumia mbinu ya hojaji. Katika kukabiliana na hili, ilimlazimu mtafiti kuwa karibu sana na wanafunzi ili kuweza kubaini wanafunzi wenye matatizo ya kusoma na kuandika kwa kuwabadilishia mbinu za ukusanyaji wa data ambapo walilazimika kutoa taarifa zao kwa kuhojiwa.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika jamii ya Wahaya waishio wilayani Missenyi kata ya Minziro. Ndani ya utafiti huu, mtafiti amejikita katika kuchunguza athari, sababu na nini kifanyike kwa wanafunzi ambao wameathirika na fonolojia ya Kihaya wanapokuwa wanajifunza lugha ya Kiswahili.

## 1.8 Mpangilio wa Tasninfu ya Utafiti

Tasnifu hii ina sura tano ambazo ni; sura ya kwanza inayohusu utangulizi ambayo ndani yake ina vipengele hivi: utangulizi wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahususi ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti, mipaka ya utafiti. Sura ya pili ni mapitio ya kazi tangulizi ambayo ndani yake ina vipengele vifuatavyo: utangulizi wa sura ya pili, kazi tangulizi, nadharia za utafiti, njia za utafiti na hitimisho. Na sura ya tatu ni njia za utafiti,

ambayo ndani yake ina vipengele hivi: mbinu za kukusanya data, mbinu za uchanganuzi wa data, udhibiti wa data, na hitimisho.

Sura ya nne ambayo inahusu uchanganuzi wa data, data za utafiti zimechambuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti ambayo ni, kubaini athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza Kiswahili, kuelezea sababu zinazoifanya lugha ya Kihaya iweze kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, na Kutathimini mbinu za kutumia ili kuwasaidia wanafunzi wa Kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili.

Sura ya tano inahusika na muhtasari, matokeo, mapendekezo na changamoto za utafiti huu. Sura hii itagawanyika katika sehemu nne ambazo ni, utangulizi, muhtasari wa utafiti, kisha mtafiti atatoa mapendekezo ya maeneo ambayo watafiti wengine wanaweza kujikita katika kufanya utafiti.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura hii mambo yaliyozungumziwa na mtafiti ni usuli wa tatizo, lengo la utafiti, umuhimu wa utafiti huu, na mpangilio wa tasnifu hii.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ameelezea historia ya jamii ya Kihaya, kazi tangulizi za kitafiti ambazo zinazoendana na mada ya utafiti husika, fonimu za Kiswahili, nadharia iliyoongoza utafiti huu, pengo la utafiti, na hitimisho la sura.

## 2.2 Historia ya Jamii ya Wahaya

Lugha ya Kihaya huzungumzwa na jamii kubwa ya watu waishio katika mkoa wa Kagera.

Kwa mujibu wa Katoke (1970), Wahaya wa mwanzo waliishi *Bunyoro-Kitara* (Uganda ya sasa) kabla ya kuhamia Buhaya. Hivyo basi, Bunyoro-Kitara ifahamike kama chanzo cha historia ya Buhaya (Wahaya) na ndio maana tamaduni nyingi za ufalme wa zamani wa Bunyoro-Kitara ni sawa na tamaduni za Buhaya/Wahaya. Kabla ya kuja kwa watawala kutoka Bunyoro-Kitara sio kwamba Buhaya ilikuwa tupu; yaani haina watu na watawala, la hasha! Buhaya ilikuwa na koo ambazo mpaka sasa bado zipo. Kila koo (*Oruganda*) ilikuwa na mkuu wa ukoo (*O'mkulu wo'Oruganda*) ambaye alikuwa kama mfalme/mzee wa ukoo. Huyu alikuwa kama Jaji Mkuu (*Omulamuzi Mukuru*), yaani alikuwa msuluhishi wa mwisho wa matatizo.

Kuna baadhi za koo zilikuwa na nguvu au ushawishi mkubwa kuliko koo nyingine, lakini jambo la msingi hapa ni kwamba hizi koo ziliongea lugha zinazoelekeana, yaani lugha zinazofanana na Kihaya cha sasa. Hizi koo zilikuwa hazijaungana,

zilikuwa zimetapakaa ingawa zilishirikiana kwa mambo mengi mojawapo ikiwa ndoa. Kwa kuwa Wahaya hawakuweza kuoa katika koo zao wenyewe, yaani kwa mfano kama mtu anatoka ukoo wa *Abarwani* asingeweza kumuoa *Mrwani* mwenzake, inabidi atafute msichana anayetoka kwenye koo nyingine mfano *Omuziba.* Mwenendo huu wa ndoa ulisaidia kuongeza na kuunganisha jamii ya Wahaya na ndio maana mpaka leo unakuta koo zilizoko Buhaya unazikuta ziko mpaka Rwanda na hata Kongo.

Kuna mambo mengi yanaweza kusemwa kuhusu Buhaya kabla ya karne ya 14 (wakati wa koo hizo). Ikumbukwe kwamba enzi hizo hapakuwa na mipaka ya nchi kama iliyopo hivi sasa. Kwa hiyo inawezekana kabisa kuwa watu wengi kutoka nchi za Rwanda, Burundi, Uganda na hata Mashariki ya Kongo walikuwa wanaelewana kabisa kilugha na kimila na ndio maana mpaka hivi sasa Mhaya na Mnyankole/Mnyoro na mpaka Munyamurenge wanaelewana ingawa wakati mwingine kwa maneno machache wanatofautiana.

Lugha ya Kihaya imeendelea kutumika hadi sasa katika shughuli zote za kijamii mkoani Kagera. Kijamii, lugha hii inatumika katika shughuli za harusi, matambiko ya asili yanayofanywa na watu maalumu wanaopendekezwa na mamlaka maalumu za koo ambazo huitwa *Abazana bo O'mukama* (wasaidizi wa mfalme) ambao huishi katika *Ikulu ya Mfalme* (Ekikale kyo O'mukama). Hali hii iliendelea kubadilika hasa Bukoba. Matumizi ya lugha ya Kihaya yalikuwa tofauti na maeneo mengine kwani mashirika ya dini ya Kikatoliki na Kilutheri yaliendelea kutumia Kihaya katika huduma zao zote, mathalani katika madarasa ya dini, katika ibada na hata vitabu vya

ibada vilichapishwa kwa lugha ya Kihaya. Rubanza (ameshatajwa) akimnukuu Raum (1925:25) anaeleza kuwa:

> …..Walutheri walisisitiza ujifunzaji wa stadi za maarifa za mwanzo zitolewe kwa kutumia lugha ya awali na baada ya kumudu stadi hizo kwa kutumia lugha ya awali au mama ndipo mtoto afundishwe lugha ya pili.

## 2.3 Kazi Tangulizi

### 2.3.1 Athari ya Lugha ya Kwanza kwa ya Pili

Katika kuchunguza uhusiano uliopo kati ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kihaya, Rubanza (ameshatajwa) aligundua kuwa kuna athari mbalimbali zilijitokeza katika matumizi ya Kihaya. Baadhi ya watafitiwa wa jamii-lugha ya awali walitumia maneno ya Kiswahili katika kuwasilisha ujumbe wao ilhali dhana husika zingeweza kutajwa kwa kutumia maneno ya Kihaya. Hata hivyo, Rubanza hakujikita kuchunguza athari za kifonolojia zinazotokana na umilisi wa lugha ya awali katika kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Ila kubaini kwake juu ya matumizi ya maneno ya lugha ya awali mahali ambapo maneno ya Kiswahili yangeweza kutumika kulimfaa mtafiti kupata mwanga juu ya kutafiti athari za kimatamshi zinazotokana na lugha ya awali wakati wa kujifunza Kswahili kama lugha ya pili.

Katika kuchunguza athari za lugha za awali katika Kiswahili mkoani Mara nchini Tanzania, Massamba (1986) aligundua kuwa lugha za asili na lugha ya Kiswahili ziliathiriana kifonolojia, kimsamiati na kisarufi. Katika tawi la fonolojia, Massamba (ameshatajwa) anaonesha jinsi ambavyo sauti zilivyoongezwa au kudondoshwa katika

matumizi ya maneno ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha za kwanza, hali iliyosababisha makosa ya utamkaji. Kuhusu msamiati, Massamba anaeleza kuwa maneno fulani kutoka lugha za kwanza za eneo la utafiti, yalipenyezwa na kutumiwa katika Kiswahili Sanifu.

Katika ukopaji wa maneno kutoka katika lugha moja kwenda katika nyingine, Bosha (1993) alichunguza athari za Kiarabu katika Kiswahili. Aligundua kwamba asilimia 44.3 ya maneno yote yanayotumika katika Kiswahili chanzo chake ni Kiarabu. Pia anaendelea kueleza kwamba hali hiyo haiifanyi lugha ya Kiswahili kuchukuliwa kuwa ni Kiarabu, lahaja ya Kiarabu au pijini ya Kiarabu. Mtaalamu huyu anasisitiza kwamba hakuna lugha ambayo inaweza kukua kipweke kama kisiwa bila kuathiriwa wala kuathiri lugha nyingine.

Hoja hii inaungwa mkono na Hagège (1999) ambaye anaeleza kuwa athari za aina hiyo hujitokeza miongoni mwa watoto na hata watu wazima. Anasisitiza kuwa athari huwa kubwa iwapo wahusika ni watu wazima kwa kuwa miundo ya lugha ya kwanza huzidi kuimarika umri unapoongezeka. Mtaalamu huyu anaendelea kuelezea kwamba, athari miongoni mwa watoto hupungua kadiri wanavyoendelea kujifunza lugha ya pili na kuna uwezekano wa athari hizo kuisha kabisa. Hagège anaongezea kuwa, mwalimu husika anapaswa kuelewa kwamba katika harakati za ujifunzaji lugha ya pili, mtoto huathiriwa na miundo ambayo anaifahamu tayari kutokana na lugha ya kwanza au awali.

Katika kuchunguza namna lugha ya Kikikuyu ilivyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, Ngugi (2007) aligundua kuwa lugha ya kwanza huathiri ujifunzaji wa lugha

ya pili katika kiwango cha fonolojia. Mtafiti huyu aliweza kugundua kuwa athari husika zilijitokeza katika matamshi na pia katika tahajia. Ngugi anasema kwamba makosa mengi yaliyojitokeza katika matumizi ya lugha ya wanafunzi wa shule za upili waliotumiwa kama watafitiwa, yalitokana na uchopekaji, udondoshaji na unazalishaji. Ameeleza kwamba, mifanyiko hiyo ya kifonolojia ilidhihirika sana katika matumizi ya lugha ya wanafunzi husika huku makosa yakijitokeza kutokana na tofauti katika mifumo ya lugha hizi mbili. Hatimaye, mtafiti huyu alipendekeza kuwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu makosa ya kisarufi, kimsamiati na kitahajia.

Utafiti mwingine wa athari za kifonolojia kwa wasemaji wa lugha ya Kiluo wanaojifunza lugha ya Kiswahili ulifanywa na Mudhune (2008). Huyu aligundua kwamba kuna kutofautiana kwa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiluo kifonolojia. Alieleza kuwa wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili, wanafunzi wazawa wa Kiluo waliingiza kanuni za lugha yao ya kwanza katika Kiswahili. Athari kubwa ya kifonolojia aliyogundua mtafiti huyu, ilihusisha sauti ambazo zinapatikana katika lugha ya pili lakini zisizopatikana katika lugha ya kwanza. Mawazo ya wataalamu hawa wote yanaonesha kuwa panapotokea mtagusano kati ya lugha moja na nyingine, lugha hizo huathiriana kisarufi. Imejitokeza wazi kuwa lugha za kwanza za Kiafrika huathiri lugha za pili hususani zile za kigeni na hivyo kusababisha makosa ya aina mbalimbali. Aidha, kuna lugha za kigeni ambazo zimeathiriwa kwa mujibu wa wataalamu wengi kama vile Kiarabu kuathiri Kiingereza wakati wa ujifunzaji wa lugha ya pili. Ni kutokana na msingi wa mawazo ya wataalamu hawa ambapo utafiti huu unachunguza namna lugha ya Kihaya inavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili.

### 2.3.2 Athari za Kifonolojia za Lugha za Kibatu katika Kiswahili

Athari za kifonolojia zinaweza kujitokeza katika mazingira ambayo lugha moja huiathiri lugha nyingine hasa ikiwa mifumo ya uundaji silabi ni tofauti. Athari hii hutokea kupitia kwa uhamishaji wa mifumo ya kifonolojia kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Matokeo yake huwa matumizi ya lugha kuwa na kasoro katika kiwango cha fonolojia. Ngungi (Ameshatajwa) alibaini kuwa makosa ya kifonolojia yanayoweza kutokea yanasababishwa na udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa fonimu.

#### (a) Udondoshaji

Udondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio katika neno kwa njia ambayo inakiuka taratibu za lugha husika. Tofauti katika utaratibu wa mfuatano wa sauti katika uundaji wa maneno kati ya lugha ya kwanza na ile ya pili zilisababisha kudondoshwa kwa sauti au hata silabi nzima kwa njia iliyoleta kasoro katika maneno mbalimbali.

Makosa yaliyogunduliwa yalielekea kuchukua ruwaza fulani. Sauti ambayo ilidondoshwa sana ni nazali hasa ilipotokea katika sauti mwambatano. Kwa mujibu wa Mukuthuria (2004) na Ngugi (Ameshatajwa), sauti mwambatano huwa tatizi, na hivyo husababisha makosa katika maendelezo ya maneno yanayosheheni sauti za aina hiyo. Kutokana na insha zilizochanganuliwa na (Ontieri, 2010), baadhi ya maneno yaliyodhihirisha kasoro hiyo ni pamoja na:

| **Udondoshaji** | **Sahihi** |
|---|---|
| majo^zi | majonzi |
| u^gedhani | ungedhani |

| | |
|---|---|
| yakanido^doka | yakanidondoka |
| ukwe^si | ukwensi |
| g^amu | ghamu |

**Chanzo: Ngugi (2007:46)**

**(b) Uchopekaji**

Uchopekaji ni mchakato wa kifonolojia ambao unarejelea hali ambapo kipashio huongezwa katika neno. Matokeo ya hali hii ni kujazwa kwa neno ambalo limebeba sauti ya ziada ambayo haikuwapo katika neno la awali. Utafiti uliofanywa na Ngungi (Ameshatajwa) ulionesha kuwa wanafunzi wazawa wa Kikikuyu wakifanya uchopekaji mwingi katika sauti nazali /n/ na /m/. Hata hivyo, kulikuwa na baadhi ya maneno yaliyodhihirisha kuchopekwa kwa irabu hususani /u/. Maneno yaliyoathiriwa na mchakato huu wa kifonolojia ni pamoja na:

| **Uchopekaji** | **Sahihi** |
|---|---|
| Inje | Nje |
| Kumuwacha | Kumwacha |
| Amuka | Amka |
| Umewandia | Umewadia |
| Njanga La Njaa | Janga La Njaa |
| Mbumbuazi | Bumbuazi |

**Chanzo: Ngugi (2007:44)**

Katika mfano wa kwanza, mtafitiwa alichopeka /i/ mwanzoni mwa neno kwa njia yenye kasoro. Kwa mujibu wa Ngugi (Ameshatajwa), baadhi ya wanafunzi wazawa wa Kikikuyu wana mazoea ya kuchopeka irabu mwanzoni au katikati mwa baadhi ya

maneno. Irabu inayochopekwa husimama kama silabi huku sehemu hiyo nyingine ya neno ikitamkwa kama silabi moja. Kosa hili linatokana na mtafitiwa kutotambua usilabi katika lugha ya Kiswahili ambapo sauti ng'ong'o wakati mwingine huwa ni silabi kamili zisizohitaji kuongezewa irabu. Maneno "kumuwacha" na "amuka", yanaonesha jinsi irabu /u/ ilivyochopekwa katikati ya konsonanti mbili. Hivyo basi, uchopekaji wa /u/ katika mifano husika ulinuiwa kuyafanya maneno hayo yakubaliane na misingi ya Kikikuyu.

Hali hii ilisababisha kosa kwa kuwa kinyume na Kikikuyu, lugha ya Kiswahili ina silabi za konsonanti pekee kama vile /m/ katika neno "amka". Uchopekaji huo unatokea katika mazingira ambayo yanaweza kuelezwa kwa kuzingatia sheria maalumu. Sheria hii ni kuwa /u/ huchopekwa kati ya king'ong'o na nusu irabu au konsonanti kamili.

**(c) Ubadilishaji Fonimu**

Makosa mengine yanayoweza kujitokeza ni baadhi ya fonimu kutumika mahali ambapo fonimu nyingine iliyo sahihi ilistahili kutumiwa. Utafiti wa Ngungi (Ameshatajwa) unaonyesha kuwa, Katika insha zilizoandikwa na wanafunzi wa jamii lugha ya Kikikuyu fonimu zilizobadilishana nafasi ni /r/ na /l/, kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| **Ubadilishaji** | **Sahihi** |
|---|---|
| Ilibadirisha | ilibadilisha |
| Serikari | serikali |
| Tulilipoti | tuliripoti |

| | |
|---|---|
| Kuzilai | kuzirai |
| Tulijalibu | tulijaribu |

**Chanzo: Ngugi (2007:46)**

Matumizi ya /r/ badala ya /l/ katika mifano mitatu ya kwanza, yalitokana na ukweli kwamba katika lugha ya Kikikuyu hakuna sauti /l/. Wanafunzi husika walitumia sauti wanayoifahamu /r/; na hivyo kuleta kasoro katika maneno husika. Hali iliyo kinyume na hiyo ilijitokeza katika mifano mitatu ya mwisho ambapo watafitiwa walitumia /l/ mahali ambapo walistahili kutumia /r/. Kasoro hii ilisababishwa na ukuruba wa sifa za kifonetiki wa sauti husika. Insha zilizoandikwa na watafitiwa wa jamii-lugha ya Kikisii zilidhihirisha uwepo wa athari ya lugha hiyo ya kwanza kupitia ubadilishaji wa fonimu katika maneno anuwai. Baadhi ya maneno yanayodhihirisha kasoro hiyo ni pamoja na:

| **Ubadilishaji** | **Sahihi** |
|---|---|
| Msindo | mshindo |
| Kushugulika | kushughulika |
| Anayechinchwa | anayechinjwa |
| Kilichohusunisha | kilichohuzunisha |
| Siwani | ziwani |

**Chanzo: Ngugi (2007:40)**

Katika mfano wa kwanza, mwanafunzi ametumia /s/ badala ya /ʃ/. Kasoro hii imetokana na ukweli kwamba katika Kikisii hakuna fonimu /ʃ/. Hali hii ilimfanya mtafitiwa husika kutumia /s/ ambayo inapatikana katika lugha yake ya kwanza; na hivyo kusababisha kuwapo kwa upungufu wa kimaendelezo katika neno husika.

### 2.3.3 Sababu Zinazofanya Lugha za Kibatu Ziweze Kuathiri Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili

Kwa kawaida lugha mbili zikitumika kwa pamoja katika eneo au jamii moja huwa na kawaida ya kuathiriana kutokana na kwamba kila lugha huchukua baadhi ya msamiati toka lugha nyingine na kuuingiza katika lugha yake. Lugha zinaweza kuathiriana endapo kutakuwa na mwingiliano baina ya wanajamii wa lugha hizo. Wazungumzaji wa lugha hizo wazungumzapo huwa kuna baadhi ya tofauti zinazojitokeza katika maeneo ya kiisimu kama fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki.

Masebo na Nyangwine (Ameshatajwa), wanaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imeingiliana sana na lugha nyingine za Kibatu. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni ya pili katika jamii nyingi za Kibatu, athari ya lugha ya kwanza inaonekana sana katika matamshi. Vilevile lugha za Kibatu zimeathiri lugha ya Kiswahili katika maana, msamiati na sarufi.

Lugha inaweza kuathiriwa kutokana na matumizi ya watu ndani ya jamii kwa jinsi ambavyo wanaitumia lugha yao ya kila siku. Wazungumzaji wa lugha nyingi za kikabila hapa nchini wameathiriwa na lugha zao za kwanza wakiwemo Wahaya, ambapo wakati wa kuzungumza lugha ya Kiswahili hujikuta wameingiza kanuni na misingi ya lugha yao. Kitendo hiki huweza kuathiri lugha ya Kiswahili wakati wanapozungumza na pengine hata kupotosha ujumbe uliokusudiwa kwa msikilizaji.

Massamba na wenzake (ameshatajwa), wanaeleza kuwa wasemaji wa lugha mbili tofauti wanapokuwa na mawasiliano ya muda mrefu hawaachi kuathiriana kilugha. Lugha za Kibatu pia zimekiathiri Kiswahili (Masebo na Nyangwine, ameshatajwa)

wanaeleza kuwa, lugha za Kibatu zimechangia asilimia 64 ya maneno ya Kiswahili. Masebo na Nyangwine (Ameshatajwa), wanaeleza kuwa, Lugha ya Kiswahili imeingiliana sana na lugha nyingine za Kibatu. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni ya pili katika jamii nyingi za Kibatu, athari mojawapo inayoweza kuonekana kwa haraka ni katika matamshi.

### 2.3.4 Makosa Wanayofanya Wanafunzi Wanapojifunza Lugha ya Kiswahili

Corder (1967) anaeleza kuwa matatizo yajitokezayo mtu ajifunzapo lugha ya kwanza na lugha ya pili ni jambo la kawaida kutokea kabla ya mtumia lugha kuzoea matumizi kamili ya kanuni za lugha ya pili. Kazi ya Selinker (1969) inaonyesha kuwa kuna mifanyiko kadhaa ambayo ni muhimu katika kuchanganua matatizo katika matumizi ya lugha. Miongoni mwa mifanyiko hiyo kuna Ujumlishaji Kiholela, Uhamishaji Lugha ambapo kanuni za lugha ya kwanza hutumiwa na hivyo kukiuka kanuni za lugha ya pili.

Kila aina ya tatizo hudhihirika katika njia hizo zilizotajwa na Selinker (Ameshatajwa). Kwa mujibu wake, makosa hayo huibua kiwango kingine katika matumizi ya lugha kinachoitwa lugha kati yaani lugha inayojitokeza wakati mzungumzaji yuko katika harakati za kujifunza lugha ya pili kwani mzungumzaji wa lugha kati huhamisha kanuni za lugha ya kwanza na kuzitumia katika lugha lengwa. Richard (1974) na Selinker (1972) wameorodhesha aina nne za makosa katika kujifunza tungo za Kiswahili, Mathalani:

#### (a) Uhamishaji Lugha

Huu ni utaratibu wa kuhamisha kiambajengo cha lugha moja uliyoizoea na kukitumia katika lugha nyingine unayojifunza. Watu wengi huchukulia kuwa lugha ya kwanza

na za lugha ya pili zinafanana. Vilevile, wanafunzi husadiki kuwa kanuni zinazotawala lugha mbili ni moja kwa hiyo zinaweza kutumiwa katika lugha zote mbili kwa njia ya kubadilishana.

Masebo na Nyangwine (2008) wanaeleza kuwa lugha ya kwanza ni lugha ambayo mtu hujifunza utotoni mwake wakati anakua kabla hajaanza kujifunza lugha ya pili. Ni lugha ambayo mtoto hujifunza kwa kusikiliza kutoka kwa wazazi wake na majirani wanaomzunguka, kama wanazungumza lugha hiyo hiyo. Masebo na Nyangwine (2008) wanasema kuwa lugha ya pili ni lugha ambayo binadamu hujifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza.

**(b) Ufundishaji Mbaya wa Lugha ya Pili**

Ukosefu wa umilisi wa lugha ya pili, husababisha ufundishaji mbaya wa lugha ya pili. Baadhi ya walimu, aghalabu hukosa elimu mwafaka wajifunzapo lugha ya pili. Licha ya hayo baadhi ya walimu hukosa ujuzi wa kutosha unaohitajika katika kufundisha lugha ya pili. Baadhi yao hutumia mbinu zisizofaa za ufundishaji zikiwemo ujumlishaji wa kiholela na pia matumizi mabaya ya sheria za lugha husika.

Selinker (1972) anawalaumu baadhi ya walimu wafundishao somo la lugha ya pili kama Kiswahili, ambao hutumia mbinu zisizofaa wanapofundisha. Krashen (1987) anaeleza kuwa kielelezo mwafaka cha ujifunzaji wa lugha kinahitajika. Aidha ameongeza kuwa mwalimu anafaa kuwa kielelezo bora katika matumizi ya lugha ya pili kama kilivyo Kiswahili Kwa wanafunzi wa Kihaya. Walimu wanahimizwa kupiga msasa lugha yao maana makosa wanayoyafanya huigwa na wanafunzi wao.

### (c) Mikakati ya Kuwasiliana Katika Lugha ya Pili

Mawasiliano katika lugha ya pili hutokana na lugha mahsusi ambazo watu hujifunza ili kuweza kuwasiliana na wazungumzaji asilia na lugha lengwa. Mara nyingi mwanafunzi hujaribu kadri awezavyo ili akabiliane na upungufu alionao katika lugha lengwa. Hivyo ili afikie mawasiliano bora iwezekanavyo, mwanafunzi huyo hujikakamua katika kuhakikisha kwamba anaweza kufanya mawasiliano kwa njia sahihi. Mwanaisimu Curtain (1990) anasisitiza kuwa mwalimu hafai kuathiriwa na lugha ya kwanza atamkapo maneno katika lugha ya pili. Wataalamu hawa wamependekeza kuwa matatizo ya walimu yasipuuzwe. Aidha, kwa mujibu wa wataalamu, walimu wanatakiwa kuwa kielelezo bora kwa wanafunzi wao.

### (d) Ujumlishaji Mno Kiholela

Ujumlishaji huu ni utoaji wa mahitimisho maelezo ya kijumla sana hadi kuvuka mpaka. Mara nyingi wanafunzi hutumia sheria kiholela yaani hata pasipofaa. Hivyo kutokana na kufanya hivyo wanafunzi hubaini chukulizi katika lugha lengwa na pia kuzitumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili na vilevile kusababisha makosa mengi katika lugha ya pili. Katika utafiti wake Brown (1993) anaeleza kuwa, matatizo ya wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili ni kuwa huwa hawatambui mfumo na kanuni za lugha husika. Watu wengi hukosa ujuzi wa kutosha pale wanapojifunza lugha ya pili hasa kama lugha ya awali imepata mizizi ya kutosha ndani ya mhusika.

## 2.4 Fonimu za Kiswahili

Mwanaisimu Mgullu (2012) anaeleza kuwa fonimu ni kipashio kidogo kabisa katika lugha kilicho na uamilifu wa kutofautisha maana katika maneno. Massamba na

wenzake (2004) na Iribemwangi (2010) ni miongoni mwa wanaisimu walioushughulikia mfumo wa fonimu za Kiswahili. Hawa wameziainisha fonimu kama fonimu za irabu, fonimu za nusu irabu na fonimu za konsonanti. Katika kuchunguza mifumo-sauti ya lugha mbalimbali, mfanano wa kifonetiki kati ya sauti ni muhimu sana, kama vile mahusiano yote ya kifonolojia, kanuni pamoja na minyumbuo yote. Katika kuainisha sauti za lugha, ili kugundua zipi ni fonimu za lugha hiyo pamoja na alofoni zake, umuhimu huwekwa katika kuangalia uhusiano uliopo kati ya makundi ya sauti kufuatana na mahali pa kutamkia na namna ya utamkaji.

Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa, sauti za lugha zimeainishwa katika makundi mbalimbali kulingana na sifa zake bainifu. Kwa kutumia kigezo cha jinsi zinavyotamkwa, sauti za lugha zinagawanywa katika makundi mawili makuu ya Konsonanti na vokali.

### 2.4.1 Fonimu za Irabu/Vokali za Kiswahili Sanifu

Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa vokali hutamkwa ala zikiwa zimeachana hivi kwamba hakuna mkwaruzo wazi kama wakati wa kutoa konsonanti. Mgullu (2012) anaeleza kuwa, wakati wa kutamka irabu hewa huwa haizuiwi wala kubanwa mahali popote. Kuna aina nyingi za irabu. Idadi ya irabu hutegemea lugha inayohusika kwani kila lugha huchagua idadi ya irabu kadhaa tu kutoka katika bohari la sauti. Jumla ya irabu za Kiswahili ni tano nazo ni / a /, /ɛ /, / i /, / ɔ / , / u /. Hizi ndizo huungana na konsonanti ili kuunda silabi. Kwa mujibu wa Mgullu (ameshatajwa) Irabu huainishwa kwa kutumia vigezo vitatu, navyo ni:

**(i) Sehemu ya Ulimi**

Sehemu ya ulimi inayohusika wakati wa kutamka irabu inaweza kuwa ya mbele, kati au nyuma. Katika Kiswahili irabu za mbele ni na / i / na /ɛ / na ilhali zile za nyuma ni /ɔ / na / u / . Irabu ya kati ni / a /.


**(ii) Mwinuko wa Ulimi**

Ulimi unaweza kuinuliwa juu ukawa sambamba na sehemu ya juu ya kinywa. Irabu zitamkwazo ulimi ukiwa umeinuliwa juu na sambamba na paa la kinywa ni za [+ juu], nazo ni / i / na / u /. Lakini pia ulimi unaweza kulazwa chini kinywani wakati wa kutamka sauti. Irabu ambayo hutamkwa katika sehemu ya chini mwa kinywa ni /a /.

Pia irabu /ɛ / na / ɔ / zenyewe zina sifa ya [-kaze] yaani zinapotamkwa ulimi huwa umelegezwa ukilinganishwa na wakati wa kuzitamka sauti / a /, / i / na / u / ambazo hizi hutolewa wakati ambapo ulimi unakuwa umekazwa. Sauti hizi ambazo hutolewa wakati ulimi ukiwa umekazwa huwa na sifa ya [+ kaze]. Pia kuna Irabu zitamkwazo ulimi ukiwa katikati ambazo ni /ɛ / na / ɔ /.

**(iii) Mkao wa Midomo**

Wakati wa kutamka irabu, mkao wa mdomo unaweza kuwa na umbo la mviringo au umbo mtandazo. Irabu zinazotamkwa wakati mdomo ukiwa na umbo la mviringo ni /u/ na /ɔ/. Irabu zinazotamkwa wakati mdomo ukiwa na mkao wa mtandazo ni /a /, /ɛ / na /i/. Ikumbukwe kuwa kiwango cha mviringo au kutanda huwa tofauti kulingana na irabu inayohusika. Mathalani mdomo hutanda wakati wa kutamka /a / zaidi ya /ɛ / na / i /. Kielelezo namba 2.1 kinaonesha irabu za Kiswahili zitamkwavyo:




**Kielelezo Na. 2. 1: Irabu za Kiswahili**

Chanzo: Iribemwangi (2010)

### 2.4.2 Irabu za Kiswahili Sanifu na Sifa zake Bainifu

Jedwali 2.2 linaonesha kuwa irabu ambazo ni [+juu] na [+nyuma] zina sifa za [+mviringo]. Hivyo / u / ambayo ni sauti ya [+juu] na pia [+nyuma] ina sifa ya [+mviringo]. Vilevile, sauti za [-nyuma] na [-juu] ni [-mviringo]. Sauti hizo ni /a / na / ɛ /. Vivyo hivyo, sauti za [- chini] na [-nyuma] ni [+mbele] nazo ni /ɛ / na /i/. Sauti za [-chini] na [-juu] ni [-kaze]. Sauti /a / pekee ndiyo [+kati].

**Jedwali Na. 2.1: lrabu za Kiswahili Sanifu na Sifa zake Bainifu**

| **Eneo** | **Irabu za Kiswahili** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **/a /** | **/ ɛ /** | **/ i /** | **/ɔ /** | **/ u /** |
| Juu | - | - | + | - | + |
| Chini | + | - | - | - | - |
| Nyuma | - | - | - | + | + |
| Mbele | - | + | + | - | - |
| Mviringo | - | - | - | + | + |
| Kaze | + | - | + | - | + |
| Kati | + | - | - | - | - |

Chanzo: Iribemwangi (2010)

### 2.4.3 Fonimu za Nusu Irabu za Kiswahili Sanifu /Viyeyusho

Fonimu za nusu irabu ni /w/ na /j /. Sauti hizi hutamkwa kwa kuachilia hewa kutoka katika mapafu kupitia kinywani au kwenye mkondo hewa wa pua kwa mkwaruzo mdogo. Sauti /w/ hutamkwa mdomo ukiwa na mkao wa mviringo na shina la ulimi limevutwa nyuma kuelekea kwenye kaakaa laini. Lakini irabu /j/ hutamkwa midomo ikiwa imetanda huku bapa la ulimi likiwa limeinuliwa kuelekea kaakaa gumu. Kwa mujibu wa Iribemwangi (2010) sauti hizi hudhihirika wazi katika mifanyiko ya kifonolojia, hasa uyeyushaji.

### 2.4.4 Sauti za Irabu za Kihaya

Hizi ni sauti ambazo hutamkwa bila ya vikwazo katika sauti. Lugha ya Kihaya kama ilivyo lugha ya Kiswahili kina irabu tano za sauti kama inavyoonekana kwenye Jedwali namba 2.3.

**Jedwali Na. 2.2: Sauti za Irabu za Kihaya**

| Na. | Irabu | Kihaya | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | /i/ | Imuka | Amka |
| 2 | /ɛ/ | Ente | Ng’ombe |
| 3 | /a/ | Abana | Watoto |
| 4 | /ɔ/ | Oburola | Maisha |
| 5 | /Ʊ/ | Hulila | Sikia |

Chanzo: Mhilu (2008)

### 2.4.5 Konsonanti za Kiswahili Sanifu

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa, konsonanti ni sauti ya lugha inayotamkwa wakati ambapo hewa kutoka mapafuni huzuiliwa kabisa au kidogo hivi kwamba nafasi ya hewa ni ndogo sana kiasi cha hewa kupita kwa mkwaruzo. Mradi konsonanti hupita kwa mkwaruzo wa namna fulani.

Idadi ya Konsonanti za Kiswahili sanifu hutajwa tofautitofauti na wataalamu mbalimbali. Kwa mfano Mgullu (2001) na Polome (1967) wameorodhesha konsonanti 24, Massamba na wenzake (2004), wameainisha Konsonanti 23 na Iribemwangi (2010) ameorodhesha konsonanti 25. Katika utaiti huu, mtafiti alitumia idadi ya konsonanti 25 ambazo zimegawanywa katika makundi makuu sita. Makundi hayo ni Vizuiwa ( /p/, /b/, /t/, /d/, /k/, /g/), Vikwamizwa ( /s/, /z/, /f/, /v/, /ɵ/, /ð/,/ ʃ /, /x/, / γ /, /h/), Vizuiwa Kwamizwa (/ ʧ/, / ɟ / ) Nazali (/m/, /ɱ/ /n/, /ŋ /, / ɲ /), Kitambaza (/l/) na Kimadende (/ r/ ), kama inayoonekana kwenye Jedwali 2.4.

**Jedwali Na. 2.3: Konsonanti na Nusu Irabu za Kiswahili**

| **Namna ya Kutamka** | **Mahali Pa Kutamkwa** | | | | | | | | **Hali ya Glota** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vizuiwa/Vipasuo | Midomo | Midomo Na Meno | Meno | Ufizi | Kaka Gumu na Ufizi | Kaakaa Gumu | Kaakaa Laini | Koromeo | |
| | b | | | d | | | g | | Ghuna |
| | p | | | t | | | k | | Hafifu |
| Vizuiwa Kwamizwa | | | | | | /ɟ/ | | | Ghuna |
| | | | | | | / ʧ/ | | | Hafifu |
| Vikwamizwa | | v | ð | z | | | γ | h | Ghuna |
| | | f | ɵ | s | ʃ | | x | | Hafifu |
| Nazali | m | ɱ | | n | | ɲ | ŋ | | Ghuna |
| Kitambaza | | | | l | | | | | Ghuna |
| Kimadende | | | | r | | | | | Ghuna |
| Nusu Irabu | w | | | | | y | | | Ghuna |

Chanzo: Iribemwangi (2010)

### 2.4.6 Konsonanti za Lugha ya Kihaya

Jedwali namba 2.5 linaonesha konsonanti za lugha ya Kihaya, Lugha ya Kihaya ina jumla ya konsonanti 20 kama zifuatazo;

**Jedwali Na. 2.4: Konsonanti za Lugha ya Kihaya**

| No. | Konsonanti | Maneno ya Kihaya | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | /p/ | Pokya | Nyusi |
| 2 | /b/ | Binga, Bona | Kimbiza, kuona |
| 3 | /t/ | Tuma, Toma | Tuma, hisia |
| 4 | /d/ | Mwenda, ,Luganda | Tisa, ukoo |
| 5 | /k/ | Kami, Kingula | Panya, fungua |
| 6 | /g/ | Genda, Guruka | Nenda, Ruka |
| 7 | /f/ | Furura, Fumora | Hamisha, ongea |
| 8 | /s/ | Singa, Sindika | Pikicha, Sukuma |
| 9 | /z/ | Zinduka, Zoka | Safiri, tokeza |
| 10 | /S/ | Shweka, Shura | Funika, salimia |
| 11 | /tS/ | Chumba, Cholera | Pika, |
| 12 | /I/ | Leba, Lekera | Angalia, simama |
| 13 | /r/ | Rola | Ona |
| 14 | /ŋ/ | Nyegera, Nyenkya | Karibu, kesho |
| 15 | /n/ | Nagira, Naga | kulala, kutupa |
| 16 | /m/ | Mubwi, Mata | Mbu, Maziwa |
| 17 | /h/ | Huririza, Hanu | sikiliza, hapa |
| 18 | /dʒ/ | Juna, Juba | Saidia, samaki |
| 19 | /j/ | Yombeka, Yega | Jenga, jifunza |
| 20 | /w/ | Waitu, Wanyu | Yetu, wao |

Chanzo: Mhilu (2008)

### 2.4.7 Alfabeti za Kiswahili

Alfabeti ni kiasi cha alama zinazotumiwa kwa kuandika sauti mbalimbali za lugha husika. Alama hizi hupangwa katika orodha maalumu na kwa ufuatano uliokubaliwa katika lugha hiyo. Kwa mfano lugha ya Kiswahili ina alfabeti kama vile; a, b, ch, d, dh, e, f, g, gh, h, I, j, k, kh, I, m, n, ny, ng', o, p, r, s, sh, u, t, th, v, w, y, z. Jedwali namba 2.6 linaonesha alfabeti za lugha ya Kiswahili na jinsi ya kuzitamka zikiambatana na mifano ya maneno na jinsi maneno hayo yanavyotamkwa kwa lugha ya Kiswahili fasaha.

**Jedwali Na. 2.5: Alfabeti za Kiswahili**

| Namba | Herufi | Mnukuu | Neno | Mnukuu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | a A | [a] | ana | [ana] |
| 2. | b B | [b] | babu | [babu] |
| 3. | ch CH | [ʧ] | chana | [ʧana] |
| 4. | d D | [d] | dua | [dua] |
| 5. | dh DH | [ð] | dhana | [ðana] |
| 6. | e E | [e] | embe | [embe] |
| 7. | f F | [f] | fupi | [fupi] |
| 8. | g G | [g] | gogo | [gɔgɔ] |
| 9. | gh GH | [ɣ] | ghali | [ɣali] |
| 10. | h H | [h] | hai | [hai] |
| 11. | i I | [i] | ingia | [iŋgia] |
| 1.2 | j J | [ɟ] | jua | [ɟua] |
| 13. | k K | [k] | kuku | [kuku] |
| 14. | kh KH | [x] | kheri | [xeri] |
| 15. | l L | [l] | leo | [leo] |
| 16. | m M | [m] | mia | [mia] |
| 17. | n N | [n] | nuru | [nuru] |
| 18. | ng' NG' | [ŋ] | Ng'oa | [ŋɔa] |
| 1.9 | ny NY | [ɲ] | nyoka | [ɲɔka] |
| 20. | o O | [ɔ] | ogopa | [ɔgopa] |
| 21. | p P | [p] | pia | [pia] |
| 22. | r R | [r] | rudi | [rudi] |
| 23. | s S | [s] | saa | [saa] |
| 24. | sh SH | [ʃ] | shati | [ʃati] |
| 25. | t T | [t] | taa | [taa] |
| 26. | th TH | [ɵ] | thamani | [ɵamani] |
| 27. | u U | [u] | ubao | [ubao] |
| 28. | v V | [v] | vua | [vua] |
| 29. | w W | [w] | watu | [watu] |
| 30. | y Y | [j] | yai | [jai] |
| 31. | z Z | [z] | zizi | [zizi] |

Chanzo: Massamba (2004)

## 2.5 Nadharia za Utafiti

Wataalam mbalimbali wamejaribu kutoa maana ya neno nadharia, katika kutoa mchango wao Mdee na wenzake (2011) wanaeleza kuwa nadharia ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani. Massamba (2004:63) kama ambavyo alinukuliwa na Msanjila (2006:42) anasema kuwa, nadharia ni utaratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumika kama kielelezo cha kuelezea jambo.

Kuna nadharia mbalimbali zinazoweza kutumika katika tasnifu hii ili kufanya utafiti uwe na mwelekeo sahihi wa kimawazo na dhana. Mtafiti amejadili nadharia mbili na kisha akachagua moja ya kuitumia kama dira ya utafiti. Kati ya zilizojadiliwa ni nadharia ya Konsonanti vokali na nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia.

### 2.5.1 Nadharia ya Konsonanti Vokali

Nadharia ya Konsonanti Vokali iliasisiwa na Kahn (1976) ili kuweza kudhibiti uchanganuzi wa silabi za maneno kwa kupambanua mifanyiko mbalimbali ya kifonolojia na kimofolojia inayofanyika katika ngazi ya silabi. Hatimaye nadharia hii ilijizolea umaarufu na kuonekana kuwa na umuhimu mkubwa kwenye uchanganuzi wa masuala ya kifonolojia na yale ya kimofolojia na hivyo ikapata kuendelezwa na wataalamu kama (Katamba, 1989; Goldsmith, 1990). Haule (2014) anamnukuu Kahn (1976: 37) anafafanua muundo wa silabi na kusema kuwa;

(i) Kila kipande cha silabi kinahusishwa na silabi moja

(ii) Kila kipande ambacho hakina hadhi ya silabi kinahusishwa na silabi.

(iii) Mistari inayohusisha silabi na vipande haipaswi kukatizwa.

Kahn (keshatajwa) aliongeza kuwa muundo wa silabi unategemea lugha husika na kwamba kama hakuna utambuzi wa silabi ni vigumu kutambua mpangilio wa mofimu katika neno husika. Nyagah (2016) anaiunga mkono hoja kwa kusema kuwa, nadharia hii ilishaleta matokeo mazuri katika kubaini athari na michakato inayosawiri athari hizo katika baadhi ya lugha za Kibatu kutokana na lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia uchanganuzi wa silabi.

### 2.5.2 Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia

Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia iliasisiwa na mwanaisimu Vennemann (1971) ingawa baadaye iliendelezwa na (Hooper, 1971) katika tasnifu yake iliyoitwa "Aspects of Generative Phonology". Wanaisimu kadhaa walivutiwa na ujio wa nadharia hii kwani waliiona kama mkombozi wa matatizo ya kifonolojia. Baadhi ya waliovutiwa na ujio wa nadharia hii kuiko ya Fonolojia Asili ni Massamba (1996:160), anaeleza kuwa Fonolojia Asilia Zalishi ni mkabala. Hivyo ni wazi kabisa kuwa matatizo yaliyojitokeza ya Fonolojia Zalishi ndiyo yaliyoifanya Fonolojia Zalishi Asilia izuke ili kujaribu kuyatatua. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia huchunguza maumbo ya ndani ya maneno ili kupunguza udhahania. Hivyo humwezesha mchunguzi wa lugha kufikia utabiri sahihi kuhusu Lugha Asilia.

Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ina lengo la kutoa udhahania kwa kupendekeza namna ambayo miundo ya ndani na nje inapaswa kuwa na uhusiano wa moja kwa moja. Hii inaitwa kanuni ya uasilia kamili katika sheria hii, vipashio vya kifonolojia vinavyojitokeza katika uwasilishaji wa kileksia wa mofimu ni zile zinazojitokeza katika muundo nje wa mofimu hiyo. Sheria hii inasisitiza kuwa, kila kanuni ya sarufi

ya fonolojia yaani sheria zinazopata motisha kifonolojia katika lugha lazima zionyeshe ujumlishaji kuhusu muundo wa nje wa maneno.

Nadharia ya fonolojia Zalishi Asilia ina makundi makuu manne ya sheria nayo ni: (i) sheria za kifonetiki (ii) sheria za kifonolojia (iii) sheria za via (iv) sheria za sandhi. Aidha, nadharia hii hudhihirisha upekee wa kila lugha kwa hivyo ni muhimu katika kuyaweka wazi matatizo yanayoibuka katika kila kutokea kwa lugha ambayo Selinker (ameshatajwa) anaitaja kama lugha kati ambayo ni lugha inayojitokeza kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili. Dhana hii ilitokea kwa maana ya kwamba, lugha hiyo hupata sifa zake kutoka kwa lugha zote mbili. Hivyo basi, lugha huwa ni mali ya jamii kama anavyosema Cook (1969:12). Wanazuoni Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa, kila lugha inakuwa na sifa zake na kanuni ziliizoweza kubadilishwa ili kutosheleza lugha nyingine.

Ni matarajio ya mtafiti kuwa nadharia hii inaweza kuongeza katika kuchambua athari za kionolojia katika lugha ya Kiswahili yaliyosababishwa na lugha ya Kihaya kama ilivyotatua madhaifu yaliyotokana na udhaifu wa Fonolojia Zalishi katika kazi za Chomsky (1950). Zaidi ya hayo Chomsky (Ameshatajwa) alitoa andiko lilioitwa "Sound patterns of English", ambayo ilichunguzwa na wanaisimu kama Vennemann (1971) na kugundua kuwa kuna udhahania mwingi katika uwasilishaji wa elementi zake.

Kwa kuzingatia kuwa nadharia ni dira na mwongozo, utafiti huu utaongozwa na nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia imepenekezwa na mtafiti kwani nadharia hii ina uwezo wa huchunguza

maumbo/miundo ya ndani ya maneno na kuihusianisha na muundo/maumbo ya nje ili kupunguza udhahania. Nadharia hii pia, ina uwezo wa kutambua chanzo cha athari na vilevile kutabiri ama kuangalia kama kutatokea kwa athari yoyote katika lugha ya pili. Dhana hii inaendana na lengo kuu la utafiti huu ambao mtafiti anachunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza Kiswahili.

Kwa hivyo, katika kuchunguza athari ya lugha ya Kihaya na Kiswahili hasa katika tawi la fonolojia, nadharia ya Fonolojia zalishi Asilia itakuwa msaada kwa mtafiti katika kupanua miundo sahihi ya lugha hizi mbili na itamsaidia mtafiti kuelezea visababishi vya kila aina ya athari inayodhihirika, kubaini athari ya lugha ya Kihaya kwenye Kiswahili sanifu, pia, nadharia hii imetuwezesha mtafiti kulinganisha mfumo wa lugha mbili mathaalani Kihaya na Kiswahili na hivyo kubaini tofauti zinazojitokeza baina ya lugha hizo mbili. Mtafiti anaamini kuwa nadharia hii itamsaidia kubainisha atahari za kofonolojia, sababu zinazofanya lugha ya Kihaya iweze kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, na kutathimini mbinu za kuwasaidia wanafunzi walioathirika na lugha ya Kihaya.

## 2.6 Pengo la Utafiti

Tafiti nyingi zimekuwa zikifanyika juu ya athari za lugha za Kibatu katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Wanazuoni mbalimbali wamekuwa wakifanya juhudi za kuimarisha na kuboresha lugha ya Kiswahili kwa njia ya tafiti ili kumsaidia mwanafunzi ambaye anajifunza lugha ya Kiswahili bila kufanya makosa. Lakini ni ukweli kuwa bado wazungumzaji wengi wa lugha ya Kiswahili wanafanya makosa ama ya Mofolojia, Fonolojia, Sintaksia au Semantiki. Wanaisimu wamekuwa mstari wa mbele kubaini chanzo cha makosa na vilevile kubuni mbinu kadhaa zinazochangia

katika kutatua matatizo hayo. Utafiti huu ni mwendelezo wa mchango huo ambapo mtafiti atachunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti amezungumzia mapitio mbalimbali yanayohusu athari, sababu, na mbinu za kuwasaidia wanafunzi walioathirika na lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili kwenye fonolojia.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi


Sura hii inahusu mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu, sura hii ina vipengele kadhaa kama ifuatavyo; eneo la utafiti, sampuli ya watafitiwa, usampulishaji, aina za sampuli zilizotumika katika utafiti huu, mkabala wa utafiti, vyanzo vya data, mbinu za ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, na hitimisho.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika mkoa wa Kagera, wilayani Missenye. Wilaya hii imepakana na nchi ya Uganda kwa upande wa kaskazini, Upande wa mashariki inapakana na Ziwa Viktoria, na upande wa kusini inapakana na wilaya ya Karagwe. Katika sensa ya mwaka 2012, idadi ya wakazi wa wilaya ya Missenyi ilikuwa 202,632, ikiwa na eneo la ukubwa wa $km^2$ 2,709 (NBS, 2012).

Wilaya ya Missenyi ina kabila moja kubwa ambalo ni Wahaya. Lugha ya Kihaya huzungumzwa katika makabila mengine madogo madogo yanayopatikana katika wilaya hii ingawa hutofautiana katika lafudhi kutokana na maeneo ambayo watu huishi. Mfano eneo la Kiziba wanaoongea Kihaya kwa lafudhi ya Kiziba, na Waganda wa Kyaka huongea Kihaya ambacho lafudhi yake imeathiriwa na lugha ya Kiganda. Kuathirika huku kunatokana na kuishi jirani na nchi ya Uganda. Watu walioathirika na lugha ya Kiganda ni wale wanaokaa maeneo ya Kyaka, Bunazi, Mtukula, na Minziro.

Utafiti huu ulilenga kubainisha athari ya kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Utafiti ulifanyika katika eneo la Missenyi kata ya Minziro katika shule za msingi za Kigazi, Nyakahanga, Kalagala, Minziro, Kiwelu, na Kyanumbu. Eneo la Missenyi liliteuliwa na mtafiti kwa sababu, ni miongoni mwa jamii kubwa zinazozungumza lugha ya Kiswahili kilichoathiriwa na lugha ya Kihaya. Uwepo wa wazungumzaji wengi wa lugha ya Kihaya katika eneo la Missenyi ni kiwakilishi kizuri kinachoweza kutupatia data za kutosha katika utafiti huu.




**Kielelezo Na. 3.1: Ramani ya Wilaya ya Missenyi**
Chanzo: Ramani ya Wilaya ya Missenyi, (NBS, 2012)

### 3.3 Sampuli ya Watafitiwa

Babbie (1992) anasema kwamba sampuli ni sehemu ya idadi ya watu ambayo mtafiti huwatumia kukusanyia data ili kurahisisha katika kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake. Sigh (2007) aliongeza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua

kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa.

Kothari (2004) anasema kuwa kiutafiti ukubwa wa sampuli lazima ijitosheleze, pia inapaswa iwe ni ile inayotokana na kile unachotaka kukitafiti, na iwe inayowakilisha eneo msingi la utafiti. Kama sampuli ni ndogo mno, uwezekano wa malengo ya utafiti kutofikiwa ni mkubwa, na kama sampuli ni kubwa mno pia upo uwezekano wa utafiti kutumia kiasi kikubwa cha fedha na muda mrefu hivyo kazi kutokukamilika kwa wakati. Mtafiti aliamua kutumia sampuli kutokana na muda mfupi uliopo wa kukamilisha utafiti huu kwa wakati na uhaba wa fedha kwani utafiti ulikuwa unatumia pesa binafsi za mtafiti. Jedwali namba 3.1 linaonesha idadi halisi ya wanafunzi kwa kila shule na walimu ambao wanafundisha somo la Kiswahili katika kila shule.

**Jedwali Na. 3.1: Idadi Halisi ya Wanafunzi kwa kila Shule na Waslimu wa Kiswahili**

| **Jina la Shule ya Msingi** | **Wanafunzi** | | | **Walimu wa Kiswahili** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jinsia** | | **Jumla** | **Jinsia** | | **Jml** |
| | **Wavulana** | **Wanawake** | | **Me** | **Ke** | |
| Karagala | 383 | 339 | 722 | 1 | 1 | 2 |
| Kiwelu | 153 | 158 | 311 | 1 | 1 | 2 |
| Kigazi | 133 | 126 | 259 | 1 | 1 | 2 |
| Kyanumbu | 164 | 161 | 325 | 2 | 1 | 3 |
| Minziro | 202 | 184 | 386 | 1 | 1 | 2 |
| **Jumla kuu** | **1,035** | **968** | **2003** | **6** | **5** | **11** |

Chanzo: Data kutoka eneo la utafiti, (2019)

Data za utafiti zinaonesha kuwa, kwa shule zote 5 zina jumla ya wanafunzi 2,003, wavulana wakiwa 1,035 ambao ni sawa na asilimia 51.7% ya wanafunzi wote waliohusika katika utafiti huu, huku wasichana wakiwa 968 sawa na asilimia 48.3% ya watafitiwa wote waliohusika katika utafiti huu. Idadi ya walimu wanaofundisha kwa kila shule kuna wastani wa walimu wawili (2) ambao kwa ujumla wako walimu 11 katika shule zote tano (5).

## 3.4 Sampuli

Sampuli ni mchakato wa kuteua kundi dogo la watafitiwa waliolengwa kutumiwa katika utafiti. Sampuli ya watafitiwa ziliteuliwa kutoka katika kundi kubwa la watu ili watumiwe katika utafiti (Kothari, 1990).

Wakati wa kukusanya data, jumla ya watafitiwa wanafunzi 239 kutoka katika shule mbalimbali walihusishwa kutoka katika darasa la awali hadi la sita katika kuainisha jinsi lugha ya Kihaya inavyoiathiri lugha ya Kiswahili kifonolojia.

Mtafiti aliteua sampuli ya utafiti kulingana na sifa zao za kutoa data sahihi zinazotakiwa kulingana na lengo la utafiti huu yaani waliokuwa na uwezo wa kutoa habari zilizojibu kikamilifu maswali ya utafiti. Wanafunzi wa darasa la saba hawakuhusishwa katika utafiti huu kwani kipindi cha utafiti walikuwa tayari wameshamaliza mitihani yao ya kitaifa. Hivyo, darasa la saba hawakuhusika katika utafiti huu, badala yake nafasi zao zilijazwa na wanafunzi wa darasa la awali. Pamoja na kutokuwepo kwa wanafunzi wa darasa la saba hakukuathiri idadi ya walengwa waliokusudiwa kama inavyoonekana kwenye jedwali 3.2.

**Jedwali Na. 3.2: Idadi Halisi ya Wahojiwa (297)**

| Watafitiwa | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Wanafunzi | 239 | 80.5% |
| Walimu | 17 | 5.7% |
| Wallimu Wakuu | 05 | 1.7% |
| Wazazi | 36 | 12.1% |
| **Jumla** | **297** | **100** |

Chanzo: Data kutoka eneo la utafiti, (2019)

## 3.5 Usampulishaji

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia aina mbili za usampulishaji ambazo ni usampulishaji lengwa, na usampulishaji nasibu, kama ifuatavyo;

### 3.5.1 Usampulishaji Lengwa

Hii ni aina ya usampulishaji ambayo kundi la watafitiwa huchaguliwa mahususi kulingana na upekee wake katika utafiti. Watafitiwa waliohusika katika eneo hili ni walimu wanaofundisha darasa la awali hadi darasa la tatu, na walimu wakuu wa shule zote zilizohusika. Jumla watafitiwa waliohusika katika usampulishaji lengwa walikuwa ni 20 kama Jedwali namba 3.3 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 3.3: Usampulishaji Lengwa**

| Wahojiwa | Idadi |
|---|---|
| Walimu wanaofundisha darasa la awali hadi darasa la pili | 15 |
| Walimu Wakuu | 05 |
| **Jumla** | **20** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti, (2019)

### 3.5.2 Usampulishaji Nasibu

Mtafiti alitumia mbinu ya usampulishaji nasibu katika kupata idadi ya watafitiwa inayotakiwa kwa sababu watafitiwa wote walikuwa na sifa na uwezo unaolingana katika kutoa data za utafiti. Kombo na Tromp (2006) anasema usampulishaji nasibu ni mchakato wa kuteua sampuli ambapo kila sampuli katika idadi ya watafitiwa huwa na nafasi sawa ya kuchaguliwa.

Usampulishaji nasibu ulitumiwa na mtafiti kwani ni mbinu ambayo huondoa upendeleo katika kuteua sampuli ya watafitiwa. Mtafiti alitumia mbinu hii kuwapata wanafunzi katika shule zote tano ambazo zilihusika katika utafiti huu, pamoja na wazazi. Mtafiti alipofika eneo la utafiti hasa kwa wanafunzi aliwapatia kadi mbalimbali zilizokuwa zimeandikwa (ndiyo) na (hapana). Kadi za ndiyo zilikuwa na idadi sawa ambayo mtafiti aliihitaji katika kila shule na darasa husika. Lakini kadi za hapana zilikuwa nyingi kwani pia wengi haawakuhusika katika utafiti huu. Mtafiti aliamua kutumia mtindo wa kadi ili kumsaidia kuondoa dhana ya kuwa anapendelea. Ingawa wanafunzi walikuwa katika makundi makuu mawili ya kijinsia kwa maana ya kundi la wasichana na wavulana. Mtafiti aliamua kutenga makundi haya ili kuweka uwiano sawa wa kijinsia kwa kila darasa. Jedwali namba 3.4 linaonesha idadi ya wahojiwa waliopatikana kwa njia ya usampulishaji nasibu ambao walikuwa 275.

**Jedwali Na. 3.4: Idadi ya Wahojiwa kwa Njia Nasibu**

| Wahojiwa | Idadi |
|---|---|
| Wanafunzi | 239 |
| Wazazi | 36 |
| **Jumla** | **275** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti, (2019)

Jedwali namba 3.4 linaainisha idadi ya wanafunzi ambao waliteuliwa katika utafiti huu katika kila shule na idadi yake kwa kila darasa. Jedwali 3.5 linaonesha idadi ya wanafunzi waliohusika katika utafiti huu. Pia jedwali linaonesha mgawanyo wa kila darasa wa wanafunzi kwa kila shule. Jedwali pia linaonesha idadi ya kila darasa kwa shule zote walikuwa wangapi, na shule nzima kuanzia darasa la awali hadi darasa la sita walikuwa wangapi.

**Jedwali Na. 3.5: Idadi ya Wanafunzi Walioteliwa katika Utafiti**

| **Shule za Msingi** | **Madarasa** | | | | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Awali** | **I** | **II** | **III** | **IV** | **V** | **VI** | |
| Kigazi | 4 | 14 | 7 | 9 | 3 | 6 | 4 | **47** |
| Nyakahanga | 5 | 6 | 6 | 4 | 3 | 2 | 2 | **28** |
| Kalagala | 6 | 8 | 6 | 8 | 5 | 3 | 3 | **39** |
| Minziro | 6 | 9 | 9 | 7 | 2 | 4 | 3 | **40** |
| Kiwelu | 7 | 6 | 9 | 6 | 4 | 2 | 3 | **37** |
| Kyanumbu | 6 | 8 | 11 | 9 | 6 | 4 | 4 | **48** |
| **Jumla** | **34** | **51** | **48** | **43** | **23** | **21** | **19** | **239** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti, (2019)

### 3.6 Mkabala wa Utafiti

Mtafiti alitumia mkabala wa uwandani kama ulivyoelezwa na Neuman (1991). Mtafiti aliamua kutumia mkabala wa uwandani kwani mkabala huu unafaa sana kutumika kwa kutumia mbinu za hojaji na mahojiano. Mtafiti pia alitumia mbinu za hojaji na mahojiano katika ukusanyaji data za utafiti. Mkabala huu wa uwandani uliomuwezesha mtafiti kukusanya data nyingi na kufanya majumuisho ya matokeo

ya utafiti. Kwa kutumia mbinu za hojaji na mahojiano, data zilikusanywa na majumuisho yalifanywa kutokana na matokeo ya data hizo.

### 3.7 Vyanzo vya Data

Muligo (2012) anasema kwamba kuna aina kuu mbili za data, nazo ni data za msingi na data za upili.

#### 3.7.1 Data za Msingi

Data za msingi ni data ambazo zinakusanywa na mtafiti kutoka katika eneo la utafiti. Kwa mujibu wa Berg (2007) maskani ni mahali ambapo watu wanaishi na mtafiti anapokwenda kutafuta kupata data ambazo ni mpya halisi ghafi ambazo kwanza hazikuwahi kukusanywa na mtu mwingine yeyote kwa ajili ya utafiti kama wake. Data za msingi katika utafiti huu zilipatikana kutoka kwa wanafunzi, walimu na wazazi.

#### 3.7.2 Data za Upili

Data za upili katika utafiti ni zile data ambazo hupatikana kwa kusoma vitabu na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada husika ya utafiti. Mara nyingi, data hizi zinapatikana maktaba au kwenye mitandao ambayo imeunganishwa na maktaba.
Ewan na Calvert (2000) wanasema kwamba, maktaba ni mahali maalumu palipohifadhiwa nyaraka, vitabu, majarida, magazeti yenye taarifa mbalimbali kwa wasomaji na utafiti wa kada tofauti tofauti za taalam.

Data za upili zilizopatikana na kutumika katika utafiti huu zilipatikana katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tawi la Dar es Salaam, na machapisho mbalimbali ya kutoka katika mtandao. Vitabu na machapisho mbalimbali yaliyotumika ni yale tu

yaliyokuwa yanahusu jinsi lugha ya awali inavyoweza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Hivyo data hizi za upili zilimsaidia mtafiti katika kuongeza uelewa mpana wa mada ya utafiti, pia zilimsaidia mtafiti kuandika rejea za tafiti zingine, kupata nadharia, mbinu za ukusanyaji data na uchambuzi wake.

## 3.8 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Katika kuchunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili, mtafiti alitumia mbinu mbalimbali katika kukusanya data ambazo ni hojaji, na mahojiano. Mtafiti alitumia mbinu hizi mchanganyiko ili kukamilishana kwani kila moja ina madhaifu na uimara wake, hivyo mapungufu ya mbinu moja hukamilishwa na mbinu nyingine.

### 3.8.1 Hojaji

Hojaji ni mbinu ya kukusanyia data ambayo mtafiti huandika maswali na baadaye huwapa watoa taarifa ili wayajibu na kumrudishia (Kothari, 2004). Lakini Williman (2011) aliongeza kuwa, maswali ya hojaji yako ya aina mbili ambayo ni funge na yasiyofunge. Maswali funge ni maswali ambayo huhitaji majibu mafupi kama ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika majibu mengine. Aina ya pili ya maswali ya hojaji yasiyofunge, yenyewe hutoa fursa au uhuru kwa watafitiwa kujieleza kwa kina juu ya anachokijua.

Katika kutumia maswali funge, mtafiti aliandaa maswali ya dodoso ambayo yalikuwa na sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ilihusu utambulisho au utangulizi ambao unaelezea lengo la dodoso na maelezo ya jumla ya kujibu dodoso, na utambulisho wa mtafiti kwa mtafitiwa. Sehemu ya pili kilihusu taarifa binafsi za mhojiwa ambazo

zilihusisha umri, jinsia, hadhi ya ndoa, kiwango cha elimu na kabila. Jina na mawasiliano ya mhojiwa hayakuwekwa ili kumpa uhuru mtafitiwa kujihisi salama zaidi anapokuwa anajibu dodoso. Katika sehemu hii, mtafitiwa alitakiwa kuweka alama ya (√) mahali penye mabano kwa kile unachokifikiria kuwa ni sahihi kwake.

Maswali yasiyofunge yalitumika pia katika utafiti huu kwenye sehemu ya tatu ya dodoso iliyobeba maswali yaliyohitaji mhojiwa kujieleza kwa kina juu anachokifahamu kuhusiana na swali husika. Maswali yalihusu matumizi ya lugha kwa ujumla kulingana na lengo la utafiti. Lengo la maswali haya lilikuwa ni kupata maoni ya watafitiwa wenyewe kuhusu matumizi ya lugha ya Kihaya na athari yake katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

Baada ya kufika eneo la utafiti, mtafiti alijitambulisha kwa uongozi wa shule husika na kuwaomba wanafunzi pamoja na walimu ambao walihusika kwenye utafiti huu. Mtafiti alitoa maelezo ya kina kwa walimu na wanafunzi hasa wale wanaojua kusoma na kuandika kwa kuwaeleza namna ya kujibu dodoso hatua kwa hatua. Wanafunzi ambao walikuwa hawajui kusoma wala kuandika, mtafiti alitumia mbinu nyingine ili kukusanya data zao.

Lengo likiwa ni kupunguza makosa ya ujazaji wa madodoso hivyo kuathiri kazi nzima ya utafiti. Mtafiti aliwapa watafitiwa wanafunzi hojaji wajaze papo kwa papo katika chumba cha darasa ambacho kiliandaliwa na walimu. Katika chumba hicho wanafunzi walikuwa chini ya uangalizi wa mtafiti na walimu ili kila mwanafunzi aliyekuwa anahitaji msaada aupate papo kwa papo. Baada ya kujaza dodoso zote kwa ukamilifu waliyakusanya kwa mtafitiwa kwa ajili ya uchambuzi.

Walimu walitumia dodoso na walipewa uhuru wa muda mrefu zaidi kutokana na kuwa na majukumu mengi ya kikazi ambayo mtafiti alikuta wakiyatekeleza. Utafiti ulifanyika kipindi ambacho shule zilikuwa zinakaribia kufungwa, hivyo walimu walikuwa na majukumu mengi ya kusahihisha mitihani, kuandaa matokeo, na kazi zingine zinazohusiana na ufundishaji.

Mtafiti aliamua kutumia mbinu ya dodoso kwani inafaa sana kwa kukusanyia data katika kundi kubwa la watu na kwa muda mfupi sana hasa dodoso za papo kwa papo. Lakini pia inaharakisha katika kukusanya na kuchanganua data. Pia, ikisimamiwa vizuri data nyingi zinaweza kupatikana kwa usahihi zaidi kutokana na uhuru anaokuwa nao mtafitiwa wakati wa kutoa data.

### 3.8.2 Mahojiano

Kwa mujibu wa Enon (1998), mahojiano ni mbinu ya ukusanyaji wa taarifa inayohusisha uulizaji wa maswali kwa njia ya mdomo au majadiliano. Kwa maneno mengine, mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana au kwa njia ya simu, kati ya watu wawili au zaidi kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti. Mbinu hii ya mahojiano ilitumika katika utafiti huu kwa sababu ilisaidia kupata taarifa za ziada ambazo si rahisi kuzipata kwa kutumia mbinu ya dodoso.

Mbinu hii pia ilisaidia kupata maoni na mtazamo wa mtafitiwa kuhusu athari ya lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Sababu nyingine ya kutumia mbinu ya mahojiano ni kwamba ilimsaidia mtafiti kulinganisha na kuchunguza mlingano wa data zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya dodoso.

Mahojiano yalifanyika ofisini kwa mwalimu mkuu ambapo alijadiliana na mtafiti kuhusu athari ya lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Mwalimu mkuu pia alielezea jinsi athari ilivyo na mbinu ambazo zinatumika katika kukabiliana na tatizo hilo. Baada ya mahojiano na mwalimu mkuu, mtafiti pia alikaa na walimu katika chumba kimoja ambacho kilikuwa kimeandaliwa. Walimu walihojiana na mtafiti katika makundi mawili, kundi la kwanza walikuwa ni walimu wanaofundisha darasa la awali hadi la tatu, na kundi la pili ni walimu wanaofundisha darasa la nne hadi darasa la sita.

Mtafiti aliwagawa walimu katika makundi hayo kwani changamoto wanazokutana nazo walimu wa darasa la awali hadi la tatu ni tofauti na madarasa mengine. Walimu walijadili baadhi ya maneno ambayo wanafunzi wa kabila la Kihaya wanapata ugumu katika kuyatamka, lakini pia walipata muda wa kujadili na mtafiti mbinu ambazo wanazitumia katika kuwasaidia wanafunzi kujifunza lugha ya Kiswahili.

Mtafiti pia alitumia mbinu ya mahojiano kwa wanafunzi waliokuwa wanasoma darasa la awali hadi darasa la pili. Lengo la kutumia mbinu hii kwa wanafunzi wa madarasa haya ni kutokana kuwa wengi wao walikuwa hawawezi kujieleza kwa ufasaha kwa kuandika.

Lakini kwa njia ya mahojiano ilikuwa ni rahisi kupata data kutoka kwao. Wanafunzi waliwekwa kwenye chumba ambacho kiliandaliwa na walimu kwa kushirikiana na mtafiti. Wanafunzi walipewa picha na kuwataka kutamka majina yao, mfano walipewa picha za ng’ombe, mbuzi, kondoo, shule, na zingine. Lengo la kuwapa picha za wanyama ilikuwa ni kupata namna halisi ya jinsi wanavyotamka. Utaratibu

huu pia ulitumika kwa wazazi ili kujua namna wazazi pia wanavyotamka maneno haya. Wanafunzi waliohojiwa waliwekwa kwenye chumba maalumu ili kutengeneza mazingira rafiki ya kuhojiana bila kuathiriwa na mazingira ya nje.

### 3.8.3 Mbinu ya Maktabani

Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti katika kukusanya taarifa au data zilizopo katika vitabu, makala, majarida na makala ambazo zinaendana na athari za kifonolojia za lugha ya awali katika Kujifunza lugha ya pili. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata data za upili ambazo zilimsaidia mtafiti kuongeza uelewa katika kufanya utafiti. Data upili ni data ambazo tayari zinapatikana, yaani ambazo tayari zilikwisha kusanywa na kuchambuliwa na watu wengine (Kothari 2004:111). Kothari anaendelea kusema kuwa data upili zinaweza kuwa zimechapwa au kutochapwa. Mara nyingi data upili hupatikana katika machapisho, majarida, rekodi za umma na takwimu, ripoti zilizoandaliwa na tasnifu mbalimbali nakadhalika.

## 3.9 Uchanganuzi wa Data

Data za utafiti zilizokusanywa kwa njia ya mahojiano, na hojaji zilichanganuliwa kwa kutumia njia za kimaelezo na kiidadi. Njia ya kimaelezo ilitumika kuelezea ni namna gani jamii ya Wahaya waishio wilaya ya Missenyi walivyoathirika na fonolojia ya Kihaya katika kutamka maneno ya Kiswahili. Matokeo yaliyopatikana yamewasilishwa katika muundo wa majedwali kulingana na utokeaji wake na kuzingatia asilimia ya watafitiwa wa jamii ya Wahaya ili kufikia hitimisho.

Uwasilishaji na uchambuzi wa data ulifanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti wa mada hii na maswali yanayoambatana na malengo hayo. Aidha, baada ya

kuzikusanya na kuzipanga data zilizopatikana kutoka kwenye majedwali ziliingia katika hatua ya uchambuzi ili tuweze kuona ukweli unaotawala katika data hizo na hatimaye kupata msimamo sahihi kuhusu mada ya utafiti huu Kwa mantiki hiyo, mbinu zifuatazo tulizitumia. Kwanza, kuunda majedwali yaliyotuwezesha kuzipata takwimu zilizosaidia kufikia malengo mahususi ya utafiti huu. Pili, data iliwasilishwa kimaelezo na kitakwimu. Maelezo yalitolewa kwa kifupi huku yakiambatanishwa na majedwali yenye takwimu hasa asilimia ili kuwasilisha data ya kutegemewa. Majedwali yalikuwa muhimu katika kuwakilisha na kulinganisha matokeo ya data za makundi mbalimbali mfano wanafunzi, walimu na wazee.

### 3.10 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti alibainisha mbinu za utafiti kwa kuzingatia muundo wa utafiti, sampuli na usampulishaji, pamoja na namna ya ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Katika sehemu hii mtafiti amewasilisha taarifa za awali za wahojiwa ambazo zinahusisha vigezo mbalimbali vilivyotumika kuwapata wahojiwa hao kama vile, jinsia, umri, kiwango cha elimu, hadhi ya ndoa, na kabila la mhojiwa. Kipengele cha pili kimehusisha uwasilishaji na uchambuzi wa data kutoka eneo la utafiti ambalo ni wilaya ya Missenyi mkoani Kagera.

## 4.2 Taarifa za Awali za Wahojiwa

Taarifa za awali za wahojiwa zilizojadiliwa katika utafiti huu ni jinsia, umri, kiwango cha elimu, hadhi ya ndoa, na kabila la mhojiwa kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Jinsia ya Wahojiwa

Wakati wa ukusanyaji data kutoka kwa wahojiwa, mtafiti alikuwa anazingatia uwiano na usawa wa kijinsia. Hii imefanyika ili kubeba mawazo ya pande zote mbili kwa maana ya wanawake na wanaume ili kuondoa dhana ya mfumo dume wa kuhoji aina moja tu ya jinsia na kuisemea jinsia nyingine. Jedwali namba 4.1 linaonyesha kuwa, wanawake walikuwa 159 sawa na asilimia 53.5% ya watu wote waliohusika katika utafiti huu. Wanaume walikuwa 138 ikiwa ni sawa na asilimia 46.5% ya watu wote waliohojiwa katika utafiti huu. Kwa hiyo, wanawake walikuwa wengi zaidi katika utafiti huu kuliko wanaume. Taarifa inaendana na takwimu za sensa za watu na makazi ya mwaka 2012 ambayo inaonyesha kuwa wanaume ni wachache kuliko wanawake.

**Jedwali Na. 4.1: Jinsia ya wahojiwa**

| Jinsia | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Wanaume | 138 | 46.5 |
| Wanawake | 159 | 53.5 |
| **Jumla** | **297** | **100** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti, (2019)

### 4.2.2 Umri wa Wahojiwa

Jedwali namba 4.2 linaonesha umri wa wahojiwa waliohusika katika utafiti, data kutoka eneo la utafiti zinaonyesha kuwa watafitiwa waliohojiwa walikuwa wa kuanzia miaka 4 hadi 70. Kundi ambalo limechukua idadi kubwa katika utafiti huu ni umri kuanzia miaka 6 – 10 ambao walikuwa 189 sawa na salimia 63.6% ya watafitiwa wote waliohusika katika utafiti huu. Kundi hili limekuwa na wahojiwa wengi kwani utafiti ulilenga wanafunzi wa shule za msingi ambao wengi wao wako chini ya miaka 14. Katika umri wa miaka 4 – 10 huu ndio umri ambao wanafunzi wengi wanakuwa darasa la awali hadi darasa la nne. Hili kundi lilikuwa muhimu sana kwa mtafiti kwani ni rahisi sana kuona athari ya lugha ya Kihaya kwa mwanafunzi katika kutamka ama kujifunza maneno ya lugha ya Kiswahili.

Kundi la pili kwa idadi kubwa ya wahojiwa ni lile la kuanzia miaka 11 hadi 20 ambalo lina wahojiwa 67 sawa na 22.5% ya jumla ya wahojiwa wote waliohusika katika utafiti huu. Kwa mujibu wa data za kiuchambuzi, kundi hili limekuwa kubwa kwa kuchangiwa na uwepo wa wanafunzi wa darasa la tano na sita ambao umri wao wengi ulikuwa miaka 11 na 12, wale wa miaka 13 hadi 20 walikuwa wachache sana kwani kwa kiasi kikubwa utafiti ulifanyikia shuleni. Watafitiwa wengine wa umri wa kundi hili walipatikana kwenye jamii.

Kwa mujibu wa data kutoka eneo la utafiti zinaonyesha kuwa kundi lililokuwa na idadi ndogo zaidi ni mika 51 – 60, likifuatiwa na 61 – 70 ambayo yalikuwa na wahojiwa 1 na 2 sawa na asilimia 0.3% na 0.7% kwa mfuatano wa wahojiwa wote waliohusika katika utafiti huu. Makundi haya yote ukiacha makundi ya yaliyohusisha idadi kubwa ya wanafunzi yalikuwa na walimu hasa wale ambao wanafundisha madarasa ya chini kwa maana darasa la awali hadi darasa la pilli, na wazazi kutoka katika jamii ya vijiji vilivyokuwa na shule zilizohusika katika utafiti huu.

Wazazi na jamii nzima imehusishwa katika utafiti huu kwani mwanafunzi kabla hajafundishwa lugha ya Kiswahili shuleni na walimu huwa anafundishwa kwanza lugha ya awali ambayo ni Kihaya na wazazi na jamii kwa ujumla. Kwa vile utafiti huu unagusa lugha ya Kiswahili na Kihaya, ilikuwa ni busara jamii pia kuhusushwa ingawa ni kwa kiwango kidogo ili kuwapa nafasi ya kuelezea na kuchanganua baadhi ya maneno jinsi yanavyotamkwa kihalisia katika lugha ya Kihaya.

**Jedwali Na. 4.2: Umri wa Wahojiwa**

| **Kundi la Umri** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Miaka 4 - 10 | 189 | 63.6% |
| Miaka 11 - 20 | 67 | 22.5% |
| Miaka 21-30 | 13 | 4.4% |
| Miaka 31-40 | 10 | 3.4% |
| Miaka 41-50 | 15 | 5.1% |
| Miaka 51-60 | 01 | 0.3% |
| Miaka 61-70 | 02 | 0.7% |
| **Jumla** | **297** | **100** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

### 4.2.3 Elimu ya Wahojiwa

Elimu inamsaidia mtu kuwa na uwelewa wa kuelezea jambo au mambo kwa upana na usahihi zaidi. Katika kuzingatia hilo, mtafiti alitaka kupata watu wenye viwango tofauti tofauti vya kielimu kuanzia wale ambao hawakusoma kabisa hadi wale waliofika katika viwango vya vyuo vyenye ngazi mbalimbali vya kitaaluma. Wale ambao hawakusoma katika mfumo rasmi wa kielimu hawakuachwa kwani uzoefu wao wa miaka mingi unatija sana katika kutafiti lugha ya Kihaya. Mchanganyiko wa kielimu uliangaliwa ili kuleta uwiaano sawa wa kitaarifa na kimaarifa.

Jedwali namba 4.3, linaonesha kuwa kundi kubwa la watafitiwa liko kwenye elimu ya shule ya msingi. Kundi hili lina jumla ya wahojiwa 257 sawa na 86.5% ya wahojiwa wote. Kundi hili limekuwa kubwa kwani limechangiwa na wanafunzi ambao wote wako shule ya msingi. Kwa ujumla hili ndilo kundi lengwa la utafiti. Kundi linalofatia kwa ukubwa ni chuo, kundi hili lina wahojiwa 28 sawa na asilimia 9.5% ya wahojiwa wote wa utafiti huu. Kundi hili nalo limechangiwa kwa kiasi kikubwa na walimu ambao sifa yao kubwa ni lazima upitie chuo cha ualimu, na baadhi ya wana jamii ya Kihaya ambao wamefika chuo katika ngazi mbalimbali ya kitaaluma nao walipatikana kipindi cha ukusanywaji wa data.

**Jedwali Na. 4.3: Elimu**

| Kundi la elimu | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Wasiosoma | 9 | 3.0 |
| Elimu ya msingi | 257 | 86.5 |
| Sekondari | 3 | 1.0 |
| Chuo | 28 | 9.5 |
| **Jumla** | **297** | **100** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

Kundi dogo kabisa ni la elimu ya sekondari likifatiwa kwa udogo na ambao hawakusoma ambao wana wahojiwa 3(1.0%), na 9(3.0%) kwa mfuatano. makundi haya kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na jamii ya Kihaya ambayo ilihusika katika ukusanyaji wa data.

### 4.2.4 Hadhi ya Ndoa

Jedwali namba 4.4 linaonyesha hadhi ya ndoa kwa watafitiwa waliohusika katika utafiti huu. Lengo la mtafiti kuweka kipengele hiki ilikuwa ni kupata kundi la wazazi ambao pia ni wadau muhimu katika utafiti huu. Wazazi ni wadau wakuu katika kujua athari za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwani wao ndio watu wa kwanza kuanza kumfundisha mwanafunzi lugha ya awali, yaani Kihaya.

Idadi ya kijumla katika kundi hili imepungua sana kwani wanafunzi hawakuingia katika kipengele hiki. Kanuni na taratibu za shule za msingi haziruhusu wala kutambua ndoa kwa mwanafunzi. Kipengele hiki kilihusu tu watu walio na sifa za kisheria kuingia kwenye ndoa kwa maana kuwa na umri wa miaka 18 na kuendelea na hayuko katika mfumo rasmi wa kielimu hata kama hajaingia kwenye ndoa. Kwa hiyo idadi kamili ya kundi hili ni wahojiwa 28 tu.

Kwa mujibu wa jedwali namba 4.4 linaloonyesha kuwa, kundi la wahojiwa wenye idadi kubwa ni walioko kwenye ndoa ambalo lina watu 12 sawa na asilimia 42.9% ya wahojiwa wote katika kipengele cha hadhi ya ndoa. Lakini kundi dogo zaidi ni lile la waliofiwa na wenza wao wa ndoa ambao wako 2 sawa na asilimia 7.1% ya wahojiwa wote walioko kwenye kundi la hadhi ya ndoa.

**Jedwali Na. 4.4: Hadhi ya Ndoa**

| Hadhi ya ndoa | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Hawapo kwenye ndoa | 9 | 32.1% |
| Wako kwenye ndoa | 12 | 42.9% |
| Wameachana | 5 | 17.9% |
| Amefiwa | 2 | 7.1% |
| **Jumla** | **28** | **100** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

### 4.2.5 Kabila

Jedwali namba 4.5, linaonyesha kabila la watafitiwa waliohusika katika utafiti huu. Kama ambavyo lengo kuu la utafiti huu linavyosema kuwa ni kuchunguza athari za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Hivyo utafiti huu uliwalenga watu wa jamii ya Kihaya tu ambao wanapatikana katika mkoa wa Kagera wilaya ya Misenyi katika vijiji na shule tajwa tu. Lakini kutokana na umuhimu wa kuwapata wahojiwa ambao si wa jamii ya Kihaya, kama walimu, mtafiti alichanganya kidogo pale ilipobidi kufanya hivyo kama inavyoonyesha kwenye Jedwali namba 4.5. Hata hivyo, kabila ya Kihaya lilikuwa na watu 291 sawa na asilimia 98.0% ya wahojiwa wote waliohusika katika utafiti huu, na makabila mengine walikuwa 2.0% ya wahojiwa wote waliohusika katika utafiti huu.

**Jedwali Na. 4.5:** Kabila

| Kabila | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Wahaya | 291 | 98.0% |
| Makabila mengine | 6 | 2.0% |
| **Jumla** | **297** | **100** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

### 4.3 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Kipengele cha pili katika sura hii kimehusisha uwasilishaji na uchambuzi wa data kutoka eneo la utafiti. Sehemu hii mtafiti amewasilisha, na kuchambua data zilizokusanywa juu ya athari za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

Malengo makuu matatu ambayo yamejadiliwa katika sehemu hii ni, moja, kubaini athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza Kiswahili, pili, kutathmini sababu zinazoifanya lugha ya Kihaya iweze kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, na tatu ni kupendekeza mbinu za kutumia ili kuwasaidia wanafunzi wa Kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili.

### 4. 4 Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kihaya katika Kujifunza Kiswahili

Kwa mujibu wa Yule (2010) matamshi ni utamkaji wa sauti za binadamu kwa kuzingatia muktadha wa mazungumzo. Naye mwanaisimu Nkwera (1979) anaeleza kuwa muhimili wa mawasiliano mazuri ni utoaji wa matamshi yanayoeleweka kwa msikilizaji. Ni kweli kwamba mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili huweza kufanya makosa mengi ya kifonolojia kutokana na athari ya lugha mama. Makosa haya yakijitokeza hufanya neno linalotamkwa kutokuwa sahihi na huweza kupoteza maana ya neno kwa msikilizaji.

#### 4.4.1 Kushindwa Kutamka Sauti

Katika utafiti huu mtafiti alishuhudia uwepo wa athari kubwa ya kifonolojia inayoletwa na lugha ya Kihaya pale mwanafunzi anapojifunza lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, zifuatazo ni athari zilizojitokeza kwa wanafunzi wa jamii ya Kihaya wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

#### 4.4.1.1 Sauti / ð / Kutamkwa Kama Sauti /z/

Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba wanafunzi wa kabila la Kihaya walishindwa kutofautisha kati ya sauti /*ð*/ na /z/ katika baadhi ya maneno waliyopewa na mtafiti ili wayatamke. Kwa hiyo sauti /*ð*/ ilitamkwa kama sauti / z / yaani silabi za dha, dhe, dhi, dho, na dhu, ambazo hutamkwa kwa sauti za [/*ða*/, /*ðe*/, /*ði*/, /*ðɔ*/, /*ðu*/] zilitamkwa kimakosa kama *za*, *ze, zi, zo, zu*. Wanafunzi wa Kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili wanapata changamoto ya kutofautisha sauti /z/ na sauti */ ð /*.

Changamoto hii hutokea kwa wanafunzi kwani sauti /z/ na sauti */ ð,* / zote ni vikwamizi guna. Kwa hiyo wanafunzi walishindwa kutofautisha utamkwaji wa sauti hizi kwa ufasaha. kwa mujibu wa Iribemwangi, (2010), Sauti hizi hutamkwa wakati ala za sauti zinapokaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida na hivyo kusababisha mkwaruzo wa sauti.

Katika utafiti huu, wanafunzi walipewa fursa ya kusoma baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyokuwa na sauti /*ð*/ ili kupima utamkaji wao. Maneno waliyopewa na mtaiti ni kama vile; dharau, dhahabu, dhambi, dhoruba, dhaifu na dhahiri. Matokeo ya utafiti yaliyowasilishwa kwenye Jedwali namba 4.6 yalionesha kuwa kwa wastani wanafunzi 15 sawa na asilimia 6.3% ya wahojiwa wote waliohusika katika utafiti huu waliweza kutamka maneno hayo kwa usahihi na walifanikiwa kutofautisha sauti /*ð*/ na sauti /z/ katika matamshi yao. Wanafunzi 225 sawa na asilimia 94.1% ya wahojiwa wote waliohusika katika utafiti huu walishindwa kutamka maneno waliyopewa na mtafiti kwa usahihi. Wanafunzi hawa walishindwa kutofautisha kati ya sauti /*ð*/ na sauti /z/.

Mtafiti aligundua namna ambavyo wanafunzi walivyokuwa wanatamka maneno kwa kuchanganya sauti kimakosa. Makosa mengi yalikuwa ubadilishanaji wa sauti za maneno mfano, neno dhambi lilitamkwa kama zambi. Haya makosa huleta ukakasi kwa msikilizaji wa lugha ya Kiswahili hata kumpotosha msikilizaji. Makosa haya ya kimatamshi pia yalishuhudiwa ndani ya jamii ya watu wazima wa kabila ya Kihaya. Hii ni kutokana na athari ya muda mrefu ya kutumia lugha ya Kihaya kama lugha ya awali na ambayo ina nguvu kubwa katika kabila ya Wahaya. Jedwali namba 4.6 linaonesha athari ya kimatamshi katika sauti / *ð* / na sauti /z/.

**Jedwali Na. 4.6: Sauti / *ð* / Kutamkwa kama Sauti /z/**

| Neno sahihi | Neno lisilo sahihi | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Dharau | Zarau | 12 (5.0%) | 227 (95.0%) |
| Dhahabu | Zahabu | 09 (3.8%) | 280 (96.2%) |
| Dhambi | Zambi | 14 (5.9%) | 225 (94.1%) |
| Dhoruba | Zoruba | 18 (7.5%) | 221 (92.5%) |
| Dhaifu | Zaifu | 23 (9.6%) | 216 (90.4%) |
| Dhahiri | Zahiri | 11 (4.6%) | 228 (95.4%) |
| **Wastani** | | **15 (6.3%)** | **225 (94.1%)** |

Chanzo: Data kutoka eneo la Utafiti (2019)

#### 4.4.1.2 Sauti /Ɵ/ Kutamkwa kama Sauti /S/

Jedwali namba 4.7 linaonyesha kuwa wanafunzi 223 sawa na asilimia 93.3% ya watafitiwa wote waliohusika katika utafiti huu walishidwa kutamka sauti /ɵ/ kwa usahihi na badala yake walitamka kwa sauti /s/. Tatizo lilikuwa kubwa kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na pili kwani hata mtafiti alipotamka sauti /ɵ/ na kuwataka na wao watamke kama mtafiti alivyotamka walishindwa kabisa. Kwa madarasa ya juu kama darasa la tano wao walikuwa wanakosea kutamka lakini walipokuwa wanapata

msaada wa kimatamshi wengi wao waliweza kutamka vizuri. Katika mahojiano na walimu hasa wa jamii ya Kihaya, mtafiti alitaka kujua kama katika lugha ya Kihaya kuna neno ambalo lina sauti /ɵ/. Majibu waliyotoa walimu hao yalionesha kuwa katika lugha ya Kihaya hakuna sauti /ɵ/ na badala yake kuna sauti /s/. Tatizo hili la ukosekanaji wa sauti /ɵ/ lipo kwenye makabila ya mengi ya Kibatu ambayo yanapatikana katika ukanda wa ziwa viktoria, kwani hata utafiti uliofanywa na Wenceslaus (2015) katika kabila la Kijita ambalo nalo linapatikana katika ukanda wa ziwa viktoria alikutana na tatizo hili.

Mtafiti aligundua kuwa wanafunzi wa Kihaya hushindwa kutofautisha sauti /ɵ/ na sauti /s/ katika maneno yao. Sauti /ɵ/ yenyewe ni kikwamizi na ni sauti inayotamkika kwenye meno, sauti hii hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapowekwa katikati ya meno ya juu na ya chini. Ili kuitamka sauti hii kwa ufasaha, ni lazima kubana mkondohewa kabisa na kuiachia kupita ingawa kwa kugusanisha kidogo alasogezi na alatuli kiasi cha kuifanya sauti kutoka kwa kukwamakwama. Maneno yanayotokana na sauti hii ni kama thamani, thelathini, thawabu na zinginezo zenye sauti za [/ɵa/, /ɵe/, /ɵi/, /ɵɔ/, /ɵu/,].

**Jedwali Na. 4.7: Sauti /Ɵ/ Kutamkwa kama Sauti /S/**

| Neno | Makosa | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Thamani | Samani | 21 (8.8%) | 218 (91.2%) |
| Thelathini | Selasini | 19 (7.9%) | 220 (92.1%) |
| Thawabu | Sawabu | 14 (5.9%) | 225 (94.1%) |
| Themanini | Semanini | 11 (4.6%) | 228 (95.4%) |
| Thumuni | Sumuni | 26 (10.9%) | 213 (89.1%) |
| Theluthi | Selusi | 08 (3.3%) | 231 (96.6%) |
| **Wastani** | | **17 (7.1%)** | **223 (93.3%)** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

#### 4.4.1.3 Sauti / γ / Kutamkwa kama Sauti /g/

Jedwali namba 4.8 linaonyesha kuwa wastani wa wanafunzi 225 sawa na asilimia 94.1% ya watafitiwa wote waliohojiwa katika utafiti huu walishindwa kutamka maneno ya Kiswahili yenye sauti /γ/ kwa usahihi. Mtafiti aliwapatia watafitiwa maneno ya Kiswahili yenye sauti /γ/ kama vile; gharama, lugha, ghorofa, na aghalabu. Data zilionesha kuwa wanafunzi walishindwa kutofautisha kati ya sauti /γ/ na sauti /g/ katika matamshi yao. Badala ya kutamka /ghali/ wao walitamka /gali/. Utamkaji huu unaleta mkanganyiko kwani neno /ghali/ linaendana sana na neno /gari/ kiasi ambacho msikilizaji asipokuwa makini anaweza kupoteza maana iliyokusudiwa. Kwa mfano, neno ghali linahusiana na masuala ya bei kuwa juu, wakati neno gari linamaanisha chombo ha usafiri.

Ni idadi ndogo sana ambayo iliweza kutamka kwa ufasaha sauti /γ/. Idadi hiyo ni asilimia 6.3% ya wahojiwa wote waliohusika katika utafiti huu. Mtafiti aligundua kuwa kundi la waliotamka vizuri sauti /γ/ ni ile ambayo linajua Kihaya vizuri lakini pia, wengi wao walikuwa ni wale waliokaa maeneo mengine ya mjini. Kwa hiyo pamoja na kuzaliwa Misenyi, na kukulia Missenyi, lakini katika ukuaji wao waliwahi kukaa na jamii nyingine ambayo kwa namna moja ama nyingine ilinoa lafudhi yao ya Kiswahili. Lakini kwa wanafunzi ambao walionesha kwenye madodoso yao kuwa hawajawahi kukaa maeneo mengine, walishindwa kabisa. Kushindwa kwao kunatokana na upungufu wa baadhi ya fonimu katika lugha ya Kihaya. Kati ya sauti hizo ni /γ/ ambayo huwa na silabi “gha, ghe, ghi, gho, ghu”.

Sauti /γ/ ni ya kwamizo pia ni sauti ambayo hupatikana kwenye kaakaa laini (kaakaa la nyuma). Hujulikana kama sauti ya nyuma kwani utamkwaji wa sauti hii

huambatana na sehemu ya nyuma ya ulimi, ambao hujulikana kitaalamu kama alasogezi. Ili sauti hii itoke kwa ufasaha, inabidi alasauti zikaribiane na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida kiasi cha kusababisha mkwaruzo wa sauti.

Kwa kawaida, sauti /g/ na /γ/ zote ni zinapatikana kwenye kaakaa laini. Ukaribu na uhusiano huu wa karibu ndio humfanya mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yake ya pili kushindwa kuitofautisha kirahisi na kujikuta akiitumia kama sauti moja.

**Jedwali Na. 4.8: Sauti / γ / Kutamkwa kama Sauti /g/**

| Neno | Walivyotamka | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Ghala | Gala | 12 (5.0%) | 227 (95.0%) |
| Gharama | Galama | 23 (9.6%) | 216 (90.3%) |
| Lugha | Luga | 14 (5.9%) | 225 (94.1%) |
| Ghati | Gati | 19 (7.9%) | 220 (92.1%) |
| Ghorofa | Golofa | 16 (6.7%) | 223 (93.3%) |
| Aghalabu | Agalabu | 02 (0.8%) | 237 (99.2%) |
| **Wastani** | | **15 (6.3%)** | **225 (94.1%)** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

#### 4.4.1.4 Sauti /ng/ Kutamkwa kama Sauti /ŋ /

Data kutoka eneo la utafiti zilizoainishwa kwenye jedwali 4.9 zinaonesha kwamba kwa wastani wanafunzi 235 sawa na asilimia 98.3% ya wahojiwa wote waliohusika katika utafiti huu katika jamii ya kabila la Kihaya walishindwa kutamka sauti /ŋ / na badala yake waliitamka kwa sauti /g/. Mwanafunzi mmoja kutoka shule ya msingi Minziro alipoulizwa kwa nini anashindwa kutamka vizuri sauti /ŋ / alisema kuwa

katika uongeaji wake wa lugha ya Kihaya hajawahi kusikia watu wakitamka maneno yenye mfano huo. Kwetu sisi ni kawada kutamka neno /ngombe/ badala ya neno / ŋɔmbe/, /ngoa/ badala ya neno /ŋ ɔa/. Kauli hii iliungwa mkono na mwalimu mmoja wa kabila la Kihaya ambaye anatoka katika shule ya msingi Kyanumbu aliyesema kuwa katika lugha ya Kihaya hakuna neno ambalo lina sauti /ŋ / badala yake kuna maneno yenye sauti /g/. Hii inawafanya wanafunzi kupata ugumu wanapokutana na utamkwaji wa maneno kama /ŋ ɔmbe/. Changamoto ya kubadilika ni ngumu kwani jamii imeshakubaliana na upotoshwaji wa matamshi haya na hutumiwa kama sauti sahihi. Mtoto anapozaliwa hukuta jamii inayomzunguka ikitamka maneno hayo kwa sauti za kimakosa na kuyapokea kama sauti sahihi za maneno ya Kiswahili.

Mtafiti alijaribu kuwarekebisha wanafunzi wa shule moja ya Kigazi, wanafunzi walionekana kumshangaa na kumwona kama yeye ndiye anakosea kuyatamka maneno hayo kwa ufasaha. Mwalimu anayefundisha wanafunzi wa shule ya Msingi Kigazi darasa la pili alisema;

> Nimejitahidi sana kuwarekebisha wanafunzi wangu kutamka vizuri sauti /ŋ / hadi nimeshindwa sijui nifanyeje. Kila nikijitahidi kuwatamkia neno /ŋ ɔmbe/ wao hutamka /ngombe/ nikiwaambia sema /ŋ ɔa/ wao hutamka /ngoa/.

Maneno ya mwalimu huyu yanaungwa mkono na walimu wenzake wanaofundisha madarasa ya juu kama darasa la tano na sita kuwa hata wao hukutana na tatizo hilo. Mtafiti alipojaribu kuuliza mbinu wanayotumia kuwasaidia waanafunzi kutamka vizuri walisema wanatumia mbinu ya kutamka na wanafunzi kurudia alichotamka mwalimu.

Baada ya kuona tatizo ni kubwa, mtafiti alipokuwa shule ya Kigazi alitafuta picha ya ng'ombe na kuwaonyesha wanafunzi wa darasa la kwanza ili wamtajie jina la huyo mnyama. Kama ilivyotarajiwa na mtafiti, wanafunzi wote walimuita kwa sauti ya /ngombe/ badala ya sauti ya /ŋ ɔmbe/. Mtafiti alipokuwa katika shule ya msingi Kalagala aliwauliza wanafunzi kuwa wanatumia maziwa ya mnyama gani, wengi wao walisema kwa sauti ya /ngombe/ badala ya /ŋ ɔmbe/.

**Jedwali Na. 4.9: Sauti /ng/ Kutamkwa kama Sauti /ŋ /**

| Neno sahihi | Neno lisilo sahihi | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Ng'atuka | Ngatuka | 17 (7.1%) | 222 (92.9%) |
| Ng'ombe | Ngombe | 03 (1.3%) | 236 (98.7%) |
| Ng'arisha | Ngarisha | 01 (0.4%) | 238 (99.6%) |
| Ng'ang'ania | Ngangania | 0 (0%) | 239 (100%) |
| Ng'amua | Ngamua | 06 (2.5%) | 233 (97.5%) |
| Ng'oa | Ngoa | 02 (0.8%) | 237 (99.2%) |
| **Wastani** | | **5 (2.1%)** | **235 (98.3%)** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

#### 4.4.1.5 Sauti /tʃ/ Kutamkwa kama Sauti /ki/

Jedwali namba 4.10 linaonyesha athari za matumizi ya sauti /tʃ/ na sauti /ki/ katika utamkwaji wa maneno kwa lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili. Data zinaonesha kuwa wastani wa wanafunzi 228 sawa na asilimia 95.4% ya watafitiwa wote waliohojiwa katika utafiti huu walishindwa kutamka maneno yenye sauti /ki/ badala wakatamka kwa sauti /tʃ/. Kwa mfano, neno kikoi walitamka kwa sauti ya /tʃiɔi/. Athari hii pia inaonekana kwenye maneno yenye mfanano huo kama kijana, kisu, shati, kitambaa. Utafiti imeonesha kuwa katika mfumo wa sauti za Kihaya hauna sauti /ki/. Mzungumzaji wa Kihaya anapotumia Kiswahili hutumia sauti /tʃ/ akimaanisha

/ki/ kwa sababu ya kuathirika na lugha ya kwanza. Wao hutumia fonimu inayokaribina na fonimu / tʃ/. Utafiti umeonesha kuwa, kwa wastani wanafunzi 12 sawa na asilimia 5.0% ya watafitiwa wote, ndio waliweza kutamka maneno hayo kwa ufasaha.

**Jedwali Na. 4.10: Sauti /tʃ/ Kutamkwa kama Sauti /ki/**

| Neno sahihi | Neno lisilo sahihi | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Kijana | Chijana | 15 (6.3%) | 224 (93.7%) |
| Kikoi | Chikoi | 09 (3.8%) | 230 (96.2%) |
| Kisu | Chisu | 04 (1.6%) | 235 (98.4%) |
| Kitambaa | Chitambaa | 19 (7.9%) | 220 (92.1%) |
| **Wastani** | | **12 (5.0%)** | **228 (95.4%)** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

#### 4.4.1.6 Sauti /l/ Kutamkwa Kama Sauti /r/

Data za utafiti zilizokusanywa kwenye Jedwali namba 4.11 zinaonesha mwingiliano wa sauti /l/ na sauti /r/ katika maneno ya Kiswahili. Utafiti unaonesha kuwa kuna wakati wanafunzi walitumia sauti /r/ badala ya sauti /l/ katika matamshi na kuandika kwao. Utafiti huu uligundua kuwa, wanafunzi wengi wa Kihaya huchanganya herufi hizi kutokana na mazoea yao tu na ugeni wa kujifunza lugha ya Kiswahili. Katika kujifunza lugha ya pili makosa kama haya huweza kutokea na hupungua kwa kadri mwanafunzi anavyozidi kujifunza na kufanya mazoezi ya mara kwa mara ya kutamka. Hii inadhihirika kwa kuwa hata namna ya kuachana kati ya waliotamka vizuri na waliokosea kutamka maneno hayo si kubwa sana kama baadhi ya sauti zingine. Uwiano wa waliotamka vizuri na waliokosea kutamka vizuri ni 23% na 77% kwa mfaatano. Hii inaonesha kuwa tatizo la utamkaji wa sauti /l/ na sauti /r/ si kubwa sana kwenye jamii ya Kihaya.

**Jedwali Na. 4.11: Sauti /l/ Kutamkwa Kama Sauti /r/**

| Neno sahihi | Neno lisilo sahihi | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Nzuri | Nzuli | 32 (13.4%) | 207 (86.6%) |
| Ripoti | Lipoti | 23 (9.6%) | 216 (90.4%) |
| Zirai | Zilai | 45 (18.8%) | 194 (81.2%) |
| Porini | Polini | 50 (20.9%) | 189 (79.1%) |
| Jaribu | Jalibu | 82 (34.3%) | 157 (65.7%) |
| Bara | Bala | 98 (41.0%) | 141 (59%) |
| **Wastani** | | **55 (23.0%)** | **185 (77%)** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

#### 4.4.1.7 Sauti / ʧ / Kutamkwa Kama Sauti /kya/

Jedwali namba 4.12 linaonesha athari ya kimatumizi kati ya sauti / ʧ / na sauti /kya/. Utafiti umegundua kwamba, jamii ya Wahaya wanatumia sana sauti /kya/ katika lugha yao badala ya sauti /ʧ/. Wanafunzi ambao ni wazumgumzaji wa Kihaya hupachika sauti /kya/ katika maneno ya lugha ya Kiswahili yenye sauti /ʧ/.

Utafiti huu umebaini kuwa miongoni mwa maneno ambayo yanakosewa ni yale ambayo yana ukaribu sana wa kimatamshi kati ya lugha ya Kiswahili na Kihaya lakini pia yakiwa na maana sawa. Hii humfanya mwanafunzi kutumia lafudhi ya lugha ya Kihaya ambayo ameizoea sana. Mfano, “chai” katika lugha ya Kihaya huitwa “kyai” kwa hiyo ni rahisi mwanafunzi kutamka neno “kyai” badala ya “chai”.

Utafiti ulionesha kuwa pamoja na kwamba maneno yake ni machache lakini kiwango cha kukosea pale inapotokea kilikuwa kikubwa zaidi. Utafiti unaonesha kuwa, wanafunzi 235 sawa na asilimia 98.3% ya watafitiwa wote waliohojiwa walishindwa kutamka maneno hayo vizuri. Ni asilimia 2.1% ya watafitiwa wote ambao waliweza kutamka vizuri bila kuchanganya na lafudhi ya Kihaya.

**Jedwali Na. 4.12: Sauti / ʧ / Kutamkwa Kama Sauti /kya/**

| Neno sahihi | Neno lisilo sahihi | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Chai | Kyai | 19 (7.9%) | 220 (92.1%) |
| Chakula | Kyakulya | 03 (1.3%) | 236 (98.7%) |
| Chombo | Kyombo | 01 (0.4%) | 238 (99.6%) |
| Chama | Kyama | 0 (0%) | 239 (100%) |
| Chako | Kyawe | 05 (2.1%) | 234 (97.9%) |
| Changu | Kyange | 02 (0.8%) | 237 (99.2%) |
| **Wastani** | | **5 (2.1%)** | **235 (98.3%)** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

### 4.4.2 Uchopekaji wa Silabi Mwanzoni mwa Neno

Kwa mujibu wa Jedwali namba 4.13, mtafiti alipowataka wanafunzi kutamka kwa sauti picha mbalimbali ambazo alikuwa nazo kama baiskeli, biskuti, kitabu, mchele, na meza. Matokeo yanaonesha kuwa, kati ya wanafunzi 239, ni wanafunzi 51 tu ambao ni asilimia 21.3% ya watafitiwa wote waliohusika katika utafiti huu ndio waliweza kutamka kwa usahihi. Lakini wanafunzi 189 sawa na asilimia 79.1% ya watafitiwa wote waliohusika katika utafiti huu walishindwa kutamka kwa usahihi.

Wengi waliongeza sauti kimakosa mwanzoni mwa neno la awali hasa sauti /e/ na /o/. Mtafiti aligundua kuwa, wale wanafunzi wachache (21.3%) walioweza kutamka maneno kwa ufasaha walikuwa wa madarasa kuanzia darasa la tano na darasa la sita, kwa uchache sana walitoka dasara la kwanza. Hii inatokana na ukweli kuwa wanafunzi wa darasa la tano na sita wameshapitia kwenye mazoezi ya mara kwa mara ya kurekebishwa na walimu wao namna sahihi ya utamkaji wa maneno.

Utafiti huu umeonyesha kuwa, wanafunzi wengi wa Kihaya hufanya uchopekaji wa baadhi ya maneno hasa kwa sauti za mwanzo wa neno. Uchopekaji hufanya neno kuwa na sauti ya ziada ambayo haikuwapo katika neno la awali. Mfano neno "baiskeli" linakuwa "**e**baiskeli", neno "kitabu" linakuwa "**e**kitabu".

Matokeo haya yanaendana sambamba na matokeo ya utafiti aliyofanya Ngugi (2007:44), aliyekuwa anafanya utafiti wa kujua athari ya lugha ya Kikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Utafiti wake ulibaini kuwa, baadhi ya wanafunzi wazawa wa Kikikuyu wana mazoea ya kuchopeka irabu mwanzoni mwa baadhi ya maneno. Irabu inayochopekwa husimama kama silabi huku sehemu hiyo nyingine ya neno ikitamkwa kama silabi moja.

Kwa mujibu wa Ngungi (Ameshatajwa) tatizo la wanafunzi kuongeza viambishi awali mwanzoni linatokana na mtafitiwa kutotambua usilabi katika lugha ya Kiswahili ambapo sauti ng'ong'o wakati mwingine huwa ni silabi kamili zisizohitaji kuongezewa irabu. Maneno "eshule" badala ya "shule" na "omuchele" badala ya "mchele", yanaonesha jinsi sauti /e/ na sauti /o/ zilivyochopekwa mwanzoni mwa konsonanti.

Katika utafiti huu, mtafiti aliweza kukutana na tatizo hili hata pale alipokutana na watu wazima hata waliobahatika kupata elimu ya kuanzia sekondari hadi vyuo mbalimbali. Mtafiti alibaini kuwa, kwa mwanafunzi mzawa ni vigumu kuacha tabia hii ya uchopekaji kwani imezoeleka sana katika jamii ya Kihaya hata wanaozungumza Kiswahili. Hii huwafanya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili, kutamka maneno ya Kiswahili kwa lafudhi ya Kihaya.

**Jedwali Na. 4.13: Kuongeza Viambishi Visivyotakiwa Mwanzoni mwa Neno**

| Neno sahihi | Neno lisilo sahihi | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Baiskeli | Ebaiskeli | 56 (23.4%) | 183 (76.6%) |
| Biskuti | Ebishguti | 49 (20.5%) | 190 (79.5%) |
| Shule | Eshule | 37 (15.5%) | 202 (84.5%) |
| Kitabu | Ekitabo | 49 (20.5%) | 190 (79.5%) |
| Meza | Emeza | 12 (5.0%) | 227 (95%) |
| Mchele | Omuchele | 99 (41.4%) | 140 (58.6%) |
| **Wastani** | | **51 (21.3%)** | **189 (79.1%)** |

**Chanzo:** Data kutoka eneo la utafiti (2019)

### 4.4.3 Kuongeza Viambishi Visivyohitajika katikati mwa Neno

Jedwali namba 4.14 linaonesha data kutoka eneo la utafiti ambapo 183 sawa na asilimia 76.6% ya wahojiwa wote waliohusika katika utafiti huu walionesha kuongeza viambishi visivyohitajika katikati mwa neno. Watafitiwa 57 sawa na asilimia 23.8% ya watafitiwa wote waliohusika katika utafiti ndio waliweza kutamka maneno bila kuongeza viambishi katikakti mwa neno.

Athari hii hujitokeza hasa pale mzungumzaji wa lugha ya awali anapotumia nguvu ya ziada katika kutamka baadhi ya maneno ya Kiswahili. Baadhi ya maneno ambayo wazungumzaji huyatamka kwa kuongeza viambishi katikati mwa neno ni Muzee, nawo, muji, waitu, mupya na mengine kama Jedwali namba 4.17 linavyoonesha.

Katika mazungumzo ya kawaida, msikilizaji anaweza kuelewa maana ya mzungumzaji ingawa si katika usanifu wa Kiswahili. Kwa mfano, neno mzee kutamkwa muzee, ni dhahiri kuwa wataelewana ingawa si katika umahili wa lugha. Ni rahisi sana kwa anayejua kutambua na kubashili kuwa mzungumzaji huyu ni mtu aliye

athiriwa na lugha ya kwanza hasa Kihaya. Mzungumzaji mahili wa lugha ya Kiswahili huweza kugundua kwa sababu, huwa tayari anajua sauti za lugha ya Kiswahili zinatamkwaje na mahali pakutamkia. Utofauti hujitokeza pale mzungumzaji anapotamka kwa sauti ya Kiswahili maana hutumia matamishi na lafudhi ya lugha ya Kihaya.

**Jedwali Na. 4.14: Kuongeza Viambishi Visivyotakiwa katikati mwa Neno**

| Neno sahihi sahihi | Neno lisilo | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Mzee | Muzee | 27 (11.3%) | 212 (88.7%) |
| Nao | Nawo | 43 (18.0%) | 196 (82%) |
| Mji | Muji | 71 (29.7%) | 168 (70.3%) |
| Mtoto | Mutoto | 40 (17.7%) | 199 (82.3%) |
| Mpya | Mupya | 96 (40.2%) | 143 (59.8%) |
| Mke | Muke | 62 (25.9%) | 177 (74.1%) |
| **Wastani** | | **57 (23.8%)** | **183 (76.6%)** |

Chanzo: Data kutoka eneo la utafiti (2019)

### 4.4.4 Kuongeza Viambishi Mwishoni mwa Neno

Jedwali namba 4.15 linaonesha Katika uzungumzaji wa kimatamshi, kuna wakati jamii ya Kihaya huongea viambishi mwishoni mwa neno kwa kuweka sauti "po" kila anapomaliza kutamka neno la Kiswahili. Hii hutokea kutokana na kwamba kuna baadhi ya maneno ya Kihaya humalizia pia na silabi fulani hasa "lao". Mwanafunzi anapojifunza lugha ya Kiswahili hujikuta pia ameathirika na mfumo huo wa "lao". Maneno yaliyopimwa katika utafiti huu ni "Nipe, Niambie, Nisamehe, na Ng'ata".

Mathalani, wanafunzi waliotamka vizuri neno "Nipe" walikuwa 58 ambao ni sawa na asilimia 24.3% ya wanafunzi wote waliotamka neno hili. Wanaunzi 181 sawa na

asilimia 75.7% walishindwa kutamka neno hili kwa usahihi kwani walitamka "Nipepo". Katika utafiti, mtafiti aligundua kuwa wanafunzi walishindwa kutamka vizuri neno hili kwani walichanganya na kanuni ya lugha ya Kihaya ambayo hutamkwa kwa kumaliziwa na kiambishi "ho". Neno "Nipe" kwa Kihaya linatamkwa "Nishabaho". Makosa haya pia yalifanyika kwa maneno mengine kama niambie ambapo walitamka niambiepo, kwa lugha ya Kihaya likitamkwa "Ngambilao". Vile vile neno "Nisamehe kwa Kihaya linaitwa "Ngambililao". Na vile vile neno "Ng'ata kwa Kihaya linaitwa "Ndumilao". kwa ujumla wanafunzi wengi walishindwa kuyatamka maneno haya vizuri kwani ni asilimia 30.9% tu ndiyo iliweza kuyatamka kama yalivyo, lakini asilimia 69.5% walishindwa kuyatamka maneno haya kutokana na kuathirika na kanuni ya lugha ya awali ambayo ni Kihaya.

**Jedwali Na. 4.15: Kuongeza Viambishi Tamati Visivyotakiwa**

| Neno sahihi | Neno lisilo sahihi | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Nipe | Nipepo | 58 (24.3%) | 181 (75.7%) |
| Niambie | Niambiepo | 99 (41.4%) | 140 (58.6%) |
| Nisamehe | Nisamehepo | 37 (15.5%) | 202 (84.5%) |
| Ng'ata | Niumiepo | 100 (41.8%) | 139 (58.2%) |
| **Wastani** | | **74 (30.9%)** | **166 (69.5%)** |

Chanzo: Data kutoka eneo la utafiti (2019)

### 4.4.5 Kupunguza Viambishi katika Maneno

Jedwali 4.16 linaonesha athari nyingine inayowaathiri wanafunzi wa Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Athari hii hutokea pale wazungumzaji wa lugha ya kwanza wanapopunguza viambishi vya awali vya mzizi wa neno husika. Aidha,

wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili walioathiriwa na lugha Kihaya hupunguza viambishi wakati wa kuzungumza lugha ya Kiswahili, lengo lao ni kukidhi mazungumzo ya wakati huo bila kujali kanuni za lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla utafiti huu ulibaini kuwa Wahaya wengi hupunguza vitamkwa katika maneno ya lugha ya Kiswahili.

Katika utafiti huu maneno yaliyofanyiwa utafiti na kuonekana kuwa yana athari ya moja kwa moja kwa lugha ya Kiswahili ni maneno ambayo yanaanza na sauti /h/ ambapo wanafunzi wengi wakati wa kutamka, sauti /h/ huwa haitajwi katika matamshi yao. Mfano neno “Hayupo” linatamkwa “Ayupo”, neno “Hatari” hutamkwa “Atari” na mengine kama yalivyoandikwa kwenye Jedwali namba 4.20. Utafiti ulibaini kuwa kwa wastani, jumla ya wanafunzi 161 ambao ni sawa na asilimia 67.4% ya watafitiwa wote waliohusika katika utafiti huu walionyesha athari hiyo kwani sauti /h/ haikusikika katika matamshi yao.

**Jedwali Na. 4.16: Kupunguza Viambishi katika Maneno**

| Neno sahihi | Neno lisilo sahihi | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Hayupo | Ayupo | 17 (7.1%) | 222 (92.9%) |
| Hamsini | Amsini | 89 (37.2%) | 150 (62.8%) |
| Hatari | Atari | 79 (33.1%) | 160 (66.9%) |
| Hereni | Ereni | 40 (17.7%) | 199 (82.3%) |
| Hamisi | Amisi | 88 (36.8%) | 151 (63.2%) |
| Hawa | Awa | 69 (28.9%) | 170 (71.1%) |
| Hajaenda | Ajaenda | 121 (50.6%) | 118 (49.4%) |
| Hapana | Apana | 95 (39.7%) | 144 (60.3%) |
| Haya | Aya | 71 (29.7%) | 168 (70.3%) |
| Hana | Ana | 92 (38.5%) | 147 (61.5%) |
| Hataki | Ataki | 101 (42.3%) | 138 (57.7%) |
| Harusi | Arusi | 75 (31.4%) | 164 (68.6%) |
| Habari | Abari | 88 (36.8%) | 151 (63.2%) |
| Harufu | Arufu | 92 (38.5%) | 147 (61.5%) |
| Hakika | Akika | 62 (25.9%) | 177 (74.1%) |
| **Wastani** | | **79 (33.1%)** | **161 (67.4%)** |

Chanzo: Data kutoka eneo la utafiti (2019)

Hiki kiwango kinaashiria jinsi athari ilivyo kubwa kwa wanafunzi wa jamii ya Kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili. Athari hii inatokana na ukweli kwamba kwenye lugha ya Kihaya sauti /h/ haipo na badala yake humezwa na sauti /a/. sauti zote hizi wakati wa kutamkwa hewa hutoka katika kinywa cha mtamkaji /h/, na /a/. Ni asilimia 33.1% ya watafitiwa wote waliohusika katika utafiti huu ndio waliweza kutamka kwa usahihi.

## 4. 5 Sababu Zinazofanya Lugha ya Kihaya iweze Kuathiri Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili

Zifuatazo ni sababu zinazofanya lugha ya Kihaya iweze kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama ambavyo imebainishwa na mtafiti wakati wa ukusanyaji data katika eneo la utafiti.

### 4.5.1 Kukosekana kwa Baadhi ya Sauti Katika Lugha ya Kihaya

Data kutoka eneo la utafiti zinaonesha kuwa lugha ya Kihaya ina upungufu wa baadhi ya sauti ambazo zinapatikana katika lugha ya Kiswahili. Upungufu huu huwafanya wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kihaya kutumia sauti mbadala katika kufanya mawasiliano yao. Ukiangalia jedwali namba 2.5 sauti ambazo hazipo katika jedwali hilo, ndizo sauti ambazo zilionesha kuwasumbua sana wanafunzi kuzitamka. Jedwali namba 4.6 linaonesha mfano wa mapungufu haya ambapo, sauti / *ð* / wanatumia mbadala wa sauti /z/, kwa hiyo maneno yenye sauti /*ð*/ utayasikia kwa sauti /z/. kwa hiyo si ajabu kukuta mwanafunzi wa Kihaya akizungumza sauti /zahabu/ akimaanisha /*ðahabu*/. Jedwali namba 4.7 linaonyesha matamshi ya sauti /ɵ/ yakitamkwa kwa sauti /s/ na kuathiri maneno yenye sauti thamani, thelasini, na zinginezo zenye sauti za [/ɵa/, /ɵe/, /ɵi/, /ɵɔ/, /ɵu/,] na kuwa semanini, selasini kwa mfuatano. Pia sauti / γ /

haipo kwenye lugha ya Kihaya hivyo hutamkwa kwa sauti mbadala wa /g/. Jedwali namba 4.8 linaonyesha athari ya kimatamshi iliyotokea kutokana na ukosefu wa sauti /γ/. Wanafunzi badala ya kutamka /γali/ wao walitamka /gali/. Jedwali 4.9 pia linaonesha athari ya upungufu wa sauti /ŋ / unavyoathiri utamakaji fasaha wa maneno ya lugha ya Kiswahili ambapo wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili hujikuta wakitumia mbadala wa sauti /g/. Makosa haya yakifanyika maneno ya Kiswahili yenye sauti /ŋ ɔmbe/, utasikia wakiyatamka kwa sauti /ngombe/, neno lenye sauti / ŋɔa/ utalisikia wanafunzi wakitamka /ngoa/. Athari ya upungufu wa sauti ni kubwa kwani hata sauti /ki/ iliyoandikwa kwenye jedwali 4.10 linaonesha kuwa wanafunzi hulitamka kwa sauti /tʃ/. Makosa haya yakitokea maneno ya lugha ya Kiswahili kama kikoi utaliskia likitamkwa kwa sauti ya /tʃiɔi/.

### 4.5.2 Ndimi za Wanafunzi Kuathiriwa na Lugha ya Kihaya

Data za utafiti zinaonesha kuwa miongoni mwa sababu ambazo zilichangia sana lugha ya Kihaya iweze kuiathiri lugha ya kiswahili ni ndimi za wanafunzi kuathiriwa na lugha ya kwanza ambayo ni Kihaya.

Kwa mfano kuna baadhi ya sauti ambazo hazipo kwenye lugha ya Kihaya lakini zinapatikana kwenye lugha ya Kiswahili. Utamshi fasaha wa sauti za Kiswahili unaendana na eneo ambalo sauti hizo zinatamkika, mkao wa ulimi na meno, na aina ya uachiaji wa sauti. Ukikosea huu utaratibu, ni dhahiri kuwa utakosea kutamka sauti husika kwa ufasaha pia. Utamkaji wa sauti husika mara kwa mara hufanya ulimi uzoee kutamka sauti hiyo, na kama ulimi umeathirikia na aina fulani ya sauti, hutengeneza mazoea ya kudumu na kuwa kama kilema cha mhusika katika matamshi. Utafiti unaonesha kuwa wanafunzi wengi walishindwa kutamka maneno ya lugha ya

Kiswahili yenye sauti / ð / na kujikuta wakitamka maneno hayo kwa sauti /z/. Kwa mujibu wa Iribemwangi, (Ameshatajwa), anasema kuwa sauti/ ð / hutamkwa wakati ala za sauti zinapokaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida na hivyo kusababisha mkwaruzo wa sauti.

Lakini pia sauti /ɣ/ ilionesha kuwasumbua wanafunzi wanojifunza lugha ya Kiswahili kutokana na athari ya ndimi zao kuzoelea maeno ya Kihaya. Ili mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili aweze kutamka vizuri sauti /ɣ/ ambayo ni ya kwamizo pia ni sauti ambayo hupatikana kwenye kaakaa laini (kaakaa la nyuma). Sauti hii inajulikana pia kama sauti ya nyuma kwani utamkwaji wa sauti hii huambatana na sehemu ya nyuma ya ulimi, ambao hujulikana kitaalamu kama alasogezi. Ili mwanafunzi atamke sauti kwa ufasaha, inabidi alasauti zake zikaribiane na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida kiasi cha kusababisha mkwaruzo wa sauti. Changamoto inakuja pale ambapo mwanafunzi anaweza kuzichanganya sauti kwani sauti /g/ na /ɣ/ zote ni zinapatikana kwenye kaakaa laini (Jedwali 2.2). Uhusiano huu wa karibu ndio humfanya mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yake ya pili kushindwa kuitofautisha kirahisi kutokana na kulemaa kwa ulimi wake katika matamshi ya sauti mbalimbali za Kihaya na kujikuta akiitumia kama sauti moja.

Lakini pia, kulemaa kwa ndimi za wanafunzi kunakotokana matumizi ya lugha ya Kihaya kwa muda mrefu huweza kumfanya achopeke kimakosa sauti /e/ na /o/ kwa baadhi ya sauti kwenye maneno ya Kiswahili. Maneno ya Kiswahili kama baiskeli, biskuti, kitabu, mchele, na meza. Huweza kuhopekwa sauti na kuwa "**e**baiskeli", neno "kitabu" linakuwa "**e**kitabu" (Jedwali namba 4.13). Kwa mujibu wa Ngungi

(Ameshatajwa) tatizo la wanafunzi kuongeza viambishi awali mwanzoni linatokana na mwanafunzi kutotambua usilabi katika lugha ya Kiswahili ambapo sauti ng’ong’o wakati mwingine huwa ni silabi kamili zisizohitaji kuongezewa irabu. Uchopekwaji huu unaweza kufanyika katikati mwa neno kama inavyoonesha kwenye jedwali 4.14, au mwishoni mwa neno kama inavyoonesha jedwali 4.15, lakini pia mazoea ya ulimi ulioathirika na lugha ya Kihaya yanaweza kumfanya mwanafunzi kushindwa kutamka baadhi ya sauti zilizo mwanzoni mwa neno kama Jedwali 4.16.

### 4.5.3 Uhusiano wa Karibu kati ya Lugha ya Kihaya na Kiswahili

Data za utaiti zinaonesha kuwa wazungumzaji wa lugha ya Kihaya huweza kuiathiri lugha ya Kiswahili kutokana na uwepo wa mwingiliano mkubwa wa kimatamshi na kimaana kati ya lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili. Ukaribu na mwingiliano huu wa sauti huweza kumfanya mwanafunzi wa Kihaya anayejifunza lugha ya Kiswahili kujiona kuwa yuko sahihi kwani anahamisha sauti ya lugha mama na kuitumia kwenye lugha ya Kiswahili. Hali hii hutokea kwani lugha ya Kihaya ni miongoni mwa lugha ya Kibatu ambayo imechangia pia upatikanaji wa lugha ya Kiswahili.

Jedwali namba 4.12 linaonesha athari ya kimatumizi kati ya sauti / ʧ / na sauti /kya/. Utafiti umegundua kwamba, jamii ya wahaya wanatumia sana sauti /kya/ katika lugha yao badala ya sauti /ʧ/. Wanafunzi ambao ni wazumgumzaji wa Kihaya hupachika sauti /kya/ katika maneno ya lugha ya Kiswahili yenye sauti /ʧ/. Mfano, “chai” katika lugha ya Kihaya huitwa “kyai” kwa hiyo ni rahisi mwanafunzi kutamka neno “kyai” badala ya “chai”. Kwa mujibu wa data za utafiti wa jedwali 4.12, idadi ya wanafunzi waliotamka sauti sahihi ya lugha ya Kiswahili walikuwa 2.1% ya wahusika wote waliohusika katika utafiti huu. Lakini zaidi ya 98% walishindwa kuonesha utofauti

huu na sababu kubwa ni ukaribu wa kifonolojia kati ya lugha ya Kihaya na lugha ya Kiswahili.

#### 4.5.4 Wanafunzi Kukosa Muda wa Kufanya Mazoezi ya Kutosha Kuzungumza Sauti za Lugha ya Kiswahili

Katika utafiti huu, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kama kutakuwa na juhudi za makusudi za kuwasaidia wanafunzi kufanya mazoezi ya kutosha katika kutamka baadhi ya sauti ambazo haipo kwenye lugha ya Kihaya lakini zinapatikana kwenye lugha ya Kiswahili, basi athari hii itaisha.

Data zinaonesha kuwa wanafunzi kati ya wanafunzi 114 waliopewa mazoezi ya kutamka sauti za lugha ya Kiswahili ambazo hazipo kwenye lugha ya Kihaya, matokeo yalionesha kuwa wanafunzi 92 ambao ni sawa na 80.7% ambao walikuwa na tatizo la kimatamshi wa sauti hizo waliweza kutamka vizuri. Ni asilimia 19.3% ya wanafunzi wote waliofanyiwa usaili huu ndio walishindwa kabisa kutamka sauti za lugha ya Kiswahili ambazo hakizo kwenye lugha ya Kihaya. Matokeo haya yanaonesha kuwa, kumbe wanafunzi wakipata mazoezi mengi ya kutamka maneno ya Kiswahili kwa ufasaha, wanaweza kuondoa tatizo hili.

Matokeo ya utafiti yanaonesha wazi kuwa sauti /l/ inatamkwa kwa sauti /r/ kwa sababu ya mazoezi duni tu ya wanafunzi ya utamkaji wa sauti hizi. Jedwali namba 4.11 linaonesha kuwa tatizo la kuchanganya sauti /l/ na sauti /r/ katika maneno ya Kiswahili lilionekana kupungua kwa kadri darasa alimokuwemo wanafunzi. Kwa maana kwamba, tatizo hili lilikuwa kubwa kwa wanafunzi wa madarasa ya chini lakini kwa wanafunzi wa madarasa ya juu kwa maana ya darasa la tano na sita, hili

tatizo lilionekana kupungua sana. Data za awali katika jedwali 4.11 zinaonesha kuwa wanafunzi waliotamka vizuri sauti /l/ na sauti /r/ ni 23% na asimia 77% walikosea katika matamshi yao. Jedwali namba 4.14 linaonesha baada ya wanafunzi wale wale waliokosea ambao walikuwa 23, matokeo ya utafiti yanonesha kuwa wastani wa wanafunzi 16 sawa na asilimia 70.0% ya wanafunzi wote waliorudia kusoma sauti walizoshindwa, waliweza kutamka maneno ya Kiswahili vizuri kwa kutofautisha kati ya sauti /l/ na sauti /r/. Lakini wastani wa wanafunzi 8 sawa na wastani wa asilimia 35% ya wanafunzi wote waliohusika ndio walishindwa kutamka maneno haya kwa usahihi.

Data zinaonesha kuwa, maneno yenye sauti /zirai/ na /porini/ yameendelea kuwa na makosa mengi kimatamshi kwani wanafunzi waliotamka vizuri neno zirai walikuwa 12 sawa na asilimia 52.2% na waliokosea kutamka neno hili wakiwa 11 sawa na asilimia 47.8% ya wahojiwa wote waliohusika. Pia, neno /porini/ wanafunzi waliotamka vizuri walikuwa 10 sawa na 43.5% ya wahojiwa wote waliohusika na wanafunzi 13 sawa na asilimia 56.5% ya wanafunzi wote waliohusika walishindwa kwa mara nyingine tena kutamka neno hili kwa ufasaha.

Lakini wanafunzi walionesha mabadiliko makubwa kwenye maneno /nzuri/ ambapo ni wanafunzi 3 tu ndo walishindwa ikiwa sawa na asilimia 13.1% ikifuatiwa na neno /ripoti/ ambapo wanafunzi 19 sawa na asilimia 82.6% ya waliohojiwa waliweza kutamka vizuri neno hilo huku wanafunzi 4 sawa na asilimia 17.4% ya waliohojiwa walishindwa kutamka vizuri. Matokeo haya yanaonesha kuwa, maneno ambayo wanafunzi walipata mabadiliko ya haraka katika kuyatamka ni maneno ambayo yanatamkwa mara kwa mara kwenye jamii tofauti na maneno mengine. Hii

inamaanisha, mwanafunzi anajifunza kwa haraka sauti ambazo anazisikia mara kwa mara kuliko sauti ambazo hazisikii mara kwa mara.

**Jedwali Na. 4.17: Matumizi ya Sauti /l/ Badala ya /r/**

| Neno sahihi | Neno lisilo sahihi | Waliotamka vizuri | Waliokosea kutamka |
|---|---|---|---|
| Bara | bala | 16 (69.6%) | 7 (30.1%) |
| Jaribu | jalibu | 18 (78.3%) | 5 (21.7%) |
| Zirai | Zilai | 12 (52.2%) | 11 (47.8%) |
| Porini | Polini | 10 (43.5%) | 13 (56.5%) |
| Ripoti | lipoti | 19 (82.6%) | 4 (17.4%) |
| Nzuri | nzuri | 20 (86.9%) | 3 (13.1%) |
| **Wastani** | | **16 (70.0%)** | **8 (35%)** |

Chanzo: Data kutoka eneo la utafiti (2019)

### 4.5.5 Upungufu wa Walimu wa Somo la Kiswahili

Walimu ni watu wa muhimu sana wanaoweza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa mwanafunzi wa anayetokea katika kabila ya Kihaya. Mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili anamtegemea sana mwalimu katika kumsaidia na kumwongoza katika utamkaji sahihi wa sauti za Kiswahili. Data za utafiti huu zinaonesha kuwa kuna uhaba mkubwa sana wa walimu katika shule ambazo utafiti ulifanyika. Jedwali namba 3.1 linonesha kuwa kwa wastani, kila shule kunawalimu wawili ambao wanafundisha somo la Kiswahili kuanzia darasa la kwanza hadi la saba. Upungufu huu huwafanya walimu kuzidiwa mzigo wa kuwafatuilia nkwa kina wanafunzi kutamka maneno ya Kiswahili kwa ufasaha.

### 4.5.6 Mikakati Duni ya Ufundishaji

Uwepo wa walimu wa kutosha au kutokuwepo kwa walimu ni tofauti na aina ya ufundishaji. Hapa mtafiti alikuwa anaangalia mikakati waliyokuwa wanaitumia

walimu katika kufundisha kwa masomo mbalimbali kwa kutumia lugha la Kiswahili. Data za utafiti zinaonesha kwamba, katika shule alizotembelea mtafiti, lugha kuu rasmi inayotumika kwa masomo mengi ni lugha ya Kiswahili. Katika masomo anayosoma mwanafunzi kuanzia darasa la awali hadi darasa la tatu ni Kiswahili, na kuanzia darasa la nne hadi darasa la saba masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya Kiswahili isipokuwa somo moja tu la Kiingereza ambalo hufundishwa kwa lugha Kiingereza.

Mtafiti aligundua kuwa walimu wengi wanaofundisha wanafunzi hawana mkakati wa pamoja wa kuwasaidia wanafunzi katika kujifunza matamshi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Walimu wengi huwasiliana na wanafunzi wao kwa kujali uelewa wa maana lengwa tu na kupuuza utamkaji sahihi wa maneno kwa sauti ya Kiswahili. Kwa mfano, mwalimu wa somo la Hisabati anapofundisha somo lake, mwanafunzi akitamka jibu kuwa ni “selusi” mwalimu huendelea bila kujali kuwa mwanafunzi amekosea utamkaji wa sauti sahihi ya Kiswahili kwani alitakiwa atamke “theluthi”. Urekebishaji wa sauti kwa maneno ya Kiswahili umeachwa kwa walimu wanaofundisha somo la Kiswahili pekee ambao hawezi kupambana na ukubwa wa tatizo jinsi ulivyo. Mbaya zaidi, hata walimu wenyewe wa somo la Kiswahili hasa wanaofundisha madarasa kuanzia darasa la nne hadi darasa la saba huwa hawaangalii makosa ya kifonolojia wanapowasiliana na wanafunzi wao. Kazi hiyo imeachwa kwa walimu wa darasa la kwanza na pili.

Katika mahojiano na walimu wa shule zilizofanyiwa utafiti, data zinaonesha kuwa hapakuwa na mkakati wowote wa walimu wa kuwasidia wanafunzi kuongea Kiswahili fasaha. Kila mwalimu alionekana kuwa katika harakati za kumaliza silabasi yake na

malengo mengine ya kitaaluma. Kwani hata shuleni wanafunzi walionekana huru kuongea Kihaya na wenzao bila kikwazo chochote.

### 4.5.7 Mazingira Duni ya Kujifunza Lugha ya Kiswahili

Mazingira ni jumla ya mambo yote yanayoizunguka jamii husika. Ili mwanafunzi aweze kujiunza lugha ya pili kunatakiwa kuwepo na mkakati makini sana unaootengenezwa na mazingira kwa mwanafunzi huyo. Lugha ni mali ya jamii na inatakiwa kutumika kwa ajili ya kuifanya jamii hiyo iweze kuwasiliana na kupeana taarifa. Katika utafiti huu, matafiti amebaini kuwa, mwanafunzi anapata nafasi ya kuzungumza lugha ya Kiswahili akiwa shuleni tu, na akifika nyumbani hulazimika kuzungumza lugha ya Kihaya. Haya si mazingira mazuri kwa mwanafunzi kujifunza lugha ya Kiswahili na kuwa mahiri katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti anaamini kuwa lugha isiyoongelewa mara kwa mara hufa. Kwa kuwa mahusiano ya mwanafunzi na jamii ni makubwa kuliko na taasisi ya shule, basi mwanafunzi hulazimika kujifunza tu lugha ya Kiswahili ili akubalike katika jamii ndogo ya shuleni lakini hujikuta akibobea sana katika lugha ya Kihaya ambayo ndiyo ina wazungumzaji wengi zaidi waliomzunguka.

### 4.5.8 Jamii ya Kihaya Kutoona Umuhimu wa Kutumia Lugha ya Kiswahili

Katika utafiti huu, watafitiwa zaidi ya 79% walisema wanapenda kuongea lugha ya Kihaya hata kama anajua lugha ya Kiswahi na lugha zingine. Kwa hivyo, wengi wa watafitiwa hawatumii sana kiswahili katika mawasiliano yao bali hutumia lugha Kihaya katika mawasiliano wanapokuwa nyumbani, kwenye shughuli za kijamii kama misiba, harusi, na mikutano ya kijamii. Pia utafiti umegundua kuwa, wazazi waliohojiwa 90% walisema hupenda kutumia lugha ya Kihaya wakiwa nyumbani na

watoto wao. Walipoulizwa kwa nini hupendelea kutumia lugha ya Kihaya, walisema, lugha yetu ndiyo lugha nzuri kimawasiliano kuliko lugha yoyote ile. Mzee mmoja aliyejitambulisha kwa mtafiti kuwa ana umri wa miaka 80 alisema kwa lugha ya Kihaya kuwa, hakuna lugha hapa duniani ambayo anajivunia kuitumia zaidi ya Kihaya. Hoja hii inapata nguvu zaidi hasa pale mtafiti alipomuuliza mama mmoja kutoka katika kijiji cha Kalagala ambaye alisema ana miaka 62-mama huyu alisema;

> Natamani kama kila mtu angekuwa anazungumza lugha ya Kihaya tu, hizi lugha zingine ni za kikoloni na zimejaa utapeli.

Katika utafiti huu, mtafiti amegundua kuwa hata wanafunzi hupenda kuongea zaidi Kihaya kwani ndiyo lugha ambayo hujisikia huru zaidi kuongea. Baadhi ya wanafunzi walionekana kuchukia kuongea lugha ya Kiswahili kwani wamejenga dhana mbaya kuwa lugha ya Kiswahili huambatana na fimbo. Dhana hii inapata nguvu zaidi miongoni mwa wanafunzi kwani walimu wengi hupenda kutumia fimbo wawapo darasani. Hali hii huwafanya wanafunzi wao kutoona umuhimu wa kuenzi lugha ya Kiswahili ingawa bado kuna wanafunzi wengine na wanajamii pia ambao wanatamani lugha ya Kiswahili kipate heshima ndani ya jamii.

Utafiti unaonesha kuwa pamoja na uwepo wa mkakati mzuri wa kuitunza na kuienzi lugha ya Kihaya, lakini bado changamoto ni kubwa kukubalika katika rika la kati na vijana. Vijana wengi ambao wako chini ya miaka 13 hupenda sana kuongea na kutumia lugha ya kiswahili kuliko Kihaya. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa 88% ya wahojiwa wanaozungumza lugha ya Kihaya, wamekiri kuwa lugha ya Kiswahili imepokea mabadiliko makubwa sana ya kifonolojia kutoka lugha ya Kihaya.

Takwimu za kiutafiti zinaonesha kwamba zaidi ya 79% ya watafitiwa waliohojiwa, walionesha kupenda kutumia lugha ya Kihaya katika mawasiliano yao ya kila siku, ni asilimia 21% ya watafitiwa ambao walisema kuwa wanataka kuwepo na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao.

Kundi lililotaka lugha ya Kiswahili kupewa kipaumbele ndani ya jamii ni lile ambalo huona kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha ya wasomi na wanaoishi maeneo ya mjini. Hili kundi linabebwa na idadi kubwa ya vijana ambao wako shuleni. Changamoto inayolikumba kundi hili ni kwamba halina maamuzi ya kujitegemea ndani ya jamii ya Kihaya, hivyo hujikuta likifanya maamuzi ambayo siyo ya kwao. Japo kundi hili linapata nguvu kidogo ya kuungwa mkono ndani ya jamii, bado si kundi la kubezwa kwani jamii ya Kihaya inaendelea kupokea mabadiliko ya kijamii na kitamaduni ambayo nguzo yake ni lugha.

Kwa mwamko uliopo kwenye jamii ya Kihaya ya kusomesha watoto wao, ni dhahiri kuwa kila mtoto angependa kuonekana wa kisasa na msomi ndani ya jamii ya Kihaya. Vijana wengi huongea lugha ya Kihaya pale tu wanapokuwa na wazazi wao, lakini makundi ya vijana hupendelea kuongea lugha ya Kiswahili labda kutokana na msukumo wa walimu wa kuwahimiza kuongea lugha ya Kiswahili wakiwa shuleni.

Pamoja na jitihada hizi zote, bado mtafiti aliona kuwa ushawishi na guvu ya kundi la watu wazima una nguvu kubwa zaidi kuliko kundi la vijana. Wazazi bado wameendelea kuwahamasiha vijana wao kupenda kujifunza kwa lazima lugha ya Kihaya na kuizungumza kila wapatapo nafasi. Akifafanua zaidi hii hoja, mzee mmoja alisema kuwa huwa hapendi kuongea na watoto wake kwa lugha ya Kiswahili hata

wakiwa wakubwa. Hii hoja ya kutopenda kuongea lugha nyingine badala ya Kihaya iliungwa mkono wa wazazi wengi waliohojiwa. Kundi hili hujisikia fahari sana pale linapoongea lugha ya Kihaya hata katika jamii isiyo ya Kihaya.

### 4.5.9 Ukongwe wa Lugha ya Kihaya Ndani ya Jamii

Unapokuwa eneo la Misenyi, lugha pekee kongwe inayotumika katika shughuli za kijamii ni lugha ya Kihaya. Lugha ya Kihaya ina historia ndefu sana ndani ya jamii ya Kihaya kuliko hata lugha ya Kiswahili.

Ukongwe wa matumizi ya lugha ya Kihaya unadhihirishwa na mtafiti Rubanza (1979:26) alipokuwa akimnukuu Raum (1925:25) anaeleza kuwa, Matumizi ya lugha ya Kihaya yalikuwa tofauti na maeneo mengine kwani mashirika ya dini ya Kikatoliki na Kilutheri yaliendelea kutumia Kihaya katika huduma zao zote za kidini, katika ibada na hata vitabu vya ibada vilichapishwa kwa lugha ya Kihaya.

Uwepo wa ukongwe huu unaifanya lugha ya Kihaya kuendelea kuwa maarufu minongoni mwa jamii ya Kihaya na jamii zingine ambazo ziko ndani ya wilaya ya Misenyi. Mtafiti aligundua kuwa wapo watu ndani ya wilaya ya Misenyi ambao hulazimika kujifunza lugha ya Kihaya ili kuonekana kama wanajamii halisi katika jamii ya Kihaya.

Hii huwafanya watoto wote kujifunza, ama kufundishwa lugha ya Kihaya kwa lazima. Hata wanapofikia utu uzima wao, huwa hawaoni haya kuizungumza lugha yao, na matokeo yake huwa kunatokea athari za kifonolojia katika ujifunzaji wa lugha ya kiswahili.

Mzee mmoja katika mahojiano na mtafiti alisema kuwa;

> Lugha hii ndiyo inayotumika hadi leo katika shughuli zote za kijamii katika jamii ya Wahaya. Katika shughuli zote za harusi, matambiko ya asili yanayofanywa na watu maalumu wanaopendekezwa na mamlaka maalumu za koo ambazo huitwa Abazana hutumia lugha ya kihaya.

Ukongwe wa lugha ya Kihaya katika jamii ya Missenyi kunaifanya kuwa na hadhi ya kuitwa lugha mama na lugha ya Kiswahili kujikuta ikipewa hadhi ya lugha ya pili. Sifa hizi huipa hadhi lugha ya kihaya na watu wa jamii ya wahaya kuhisi kuwa lugha yao ni ya maana Zaidi kuliko lugha zingine duniani.

Kiswahili kwa jamii ya Kihaya ni lugha ya pili ambayo mwanafunzi hujifunza akiwa katika mazingira ya shuleni. Hii hufanya kuwepo kwa athari mbalimbali kwa mwanfunzi anapojifunza lugha hii hasa kwa vipindi vya mwanzo. Kauli hii inaungwa mkono na mtafiti Lucius (1978) ambaye alisema kuwa, athari mbalimbali zinazojitokeza kwa mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili ni kwa sababu wengi wao Kiswahili ndiyo lugha ya pili kujifunza. Kwa hiyo ni dhahiri kuwa lugha ya Kihaya inaathari kubwa kifonolojia kwa mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili.

#### 4.5.10 Kihaya Kupewa Matumizi Makubwa ya Katika Shughuli za Kijamii

Utafiti huu umeonesha kuwa, lugha yeyote ambayo hupewa matumizi makubwa katika jamii ili iweze kutumika katika shughuli zao za kila siku, lugha hiyo huwa na hadhi kubwa sana kwenye jamii pia. Katika jamii inayotumia lugha mbili kwa pamoja katika shughuli za mawasiliano, basi, lugha moja huwa na kawaida ya kumeza lugha nyingine. Lugha inayomeza nyingine ndiyo huonekana kubwa kuliko iliyomezwa

katika jamii hiyo, hii hutokea kwa lugha hiyo kuzungumzwa mara kwa mara na wanajamii. Kwa mujibu wa utafiti huu, hata makosa ya kifonolojia ambayo wanafunzi walikuwa wakiyafanya ni matokeo ya matumizi makubwa ya lugha ya awali yaani Kihaya kutumika katika maeneo mengi ya mawasiliano.

Katika utafiti huu, mtafiti alikutana na wazee wengi wenye umri wa miaka 50 na kuendelea ambao hawajui kabisa lugha ya Kiswahili badala yake wanaongea lugha ya Kihaya tu. Wengi walipoulizwa kwa nini hawajui lugha ya Kiswahili, walisema kuwa ni kwa sababu hawakuenda shule au hawakuishi mjini. Dhana ya kuunganisha kujua lugha ya Kiswahili na kwenda shule inatokana na ukweli kuwa wengi wao hujifunza lugha ya Kiswahili wakiwa shule, pia huongea Kiswahili wakiwa mjini. Hali hii humfanya mtoto kupata misamiati mingi ya lugha ya Kihaya na lafudhi ya Kihaya. Hii huwa changamoto pale ambapo wanaanza kujifunza lugha ya Kiswahili akiwa shule.

Wakati lugha ya Kihaya ikipewa hadhi kubwa katika shughuli za kijamii, lugha ya Kiswahili yenyewe hutumika zaidi katika shughuli zote rasmi za kiserikali kama hospitali, mahakama, shuleni, ofisi zote za umma. Hii huwafanya watu kuanza kujifunza lugha ya Kiswahili ili kuweza kupata huduma kwa urahisi katika maeneo au ofisi za serikali. Matumizi ya Kiswahili katika sekta za umma yanapata mashiko kutumika kwani wataalamu wengi wa serikali huwa hawaajiriwi kutokana na maeneo wanayopenda.

Hivyo hujikuta wamepata watu ambao hawajui kuzungumza Kihaya. Katika utafiti uliofanywa na Barton (1980), yeye alieleza kuwa kuna kuongezeka kwa wigo mkubwa wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kuliko lugha za asili. Alibaini pia kuwa

Kiswahili kinatumika katika shughuli rasmi kama vile katika vyombo vya habari, kampeni za uelimishaji na shughuli za kisiasa.

Kwa upande wake, Polome (1980) alieleza kuwa Kiswahili na lugha za jamii zinatumika katika maeneo tofauti. Kiswahili kilionekana kutumika zaidi katika shughuli rasmi za kiserikali na lugha za asili zilionekana kuendelea kutumika katika shughuli zisizo rasmi, kwa mfano katika maeneo ya nyumbani. Lakini jambo la msingi kwa Polome (keshatajwa) ni kuwa uchaguzi wa lugha gani itumike unatokana na sababu za kiutamaduni na kijamii.

Katika utafiti huu, mtafiti amebaini kuwa, pamoja na uwepo wa matumizi ya lugha ya kiswahili katika maeneo rasmi, bado lugha ya Kihaya ina nafasi kubwa sana katika jamii ya Kihaya. Wanafunzi wa Kihaya wanapojifunza lugha ya Kiswahili, wanatumia kanuni za lugha ya Kihaya katika uundaji wa misamiati na fonolojia. Hii hufanya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili kuzungumza Kiswahili kwa fonolojia ya Kihaya.

Maelezo haya, hayana tofauti sana na mtafiti Mhilu (2005) ambaye anasema kwamba, lugha mama au ya awali hutumika katika shughuli za mawasiliano ya kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo, kama lugha ya Kihaya inatumika kama lugha ya awali au lugha mama katika maeneo hayo, inaipa nguvu sana lugha ya Kihaya katika jamii kuliko lugha ya Kiswahili. Kiswahili kwa jamii ya Kihaya ni lugha ya pili ambayo mwanafunzi hujifunza akiwa katika mazingira ya shuleni. Hii hufanya kuwepo kwa athari mbalimbali kwa mwanafunzi anapojifunza lugha hii hasa kwa vipindi vya mwanzo.

### 4.5.11 Lugha ya Kihaya Kutumika kama Utambulisho nje ya Jamii

Lugha kama chombo cha jamii kina wajibu wa kuitambulisha jamii husika katika jamii zingine. Lugha ya Kihaya inatumika kama utambulisho katika jamii ya Wahaya. Hii inamaana kuwa popote utakapomsikia mtu anaongea lugha ya Kihaya, moja kwa moja inamtambulisha au kumhusisha na jamii ya Kihaya, ingawa kwa kiasi kidogo sana inawezekana isiwe kweli kwani mtu anaweza kufahamu lugha nyingine kwa kujifunza tu.

Mwanaisimu Giles (1979 na 1982) anatuonesha kuwa upo uhusiano wa karibu kati ya lugha na utambulisho. Anaeleza kuwa utambulisho wa jamii ni mchakato unaoendelea ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamiilugha ambayo huunda kiini cha utambulisho wa jamii. Kwa mujibu wa Giles (keshatajwa), jamiilugha inaundwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wao wanatokana na jamiilugha moja ambayo iko tofauti na jamiilugha nyingine.

Hoja hii inaungwa mkono na mtafiti ambaye alipowahoji wanajamii wengi kuhusu kwa nini wanapenda sana kuongea lugha ya Kihaya hata wakiwa maeneo ya nje ya jamii yao, watafitiwa wengi walisema, huwa tunalenga kujitambulisha kuwa sisi ni wahaya. Mzee mmoja yeye alisema, ukiongea Kihaya kwenye mkusanyiko wa watu wengi, kama kuna Mhaya mwenzako ambaye mlikuwa hamfahamiani kabla, mnaweza kufahamiana kirahisi kwa njia hiyo. Matokeao yake unapata msaada au kutoa msaada kwa ndugu yako.

Akitoa ushuhuda halisi uliomtokea, mtafitiwa mmoja alieleza jinsi ambavyo aliweza kupata msaada ndani ya treni akitokea Mwanza kwenda Dar es Salaam. Kwa mujibu

wa maelezo ya mama huyo, alimsemesha mtoto wake lugha ya Kihaya kumbe aliyekuwa amekaa naye jirani alikuwa Mhaya, na walikuwa wamefika eneo la Tabora. Mama huyo aliendelea kusema kuwa hela aliyokuwa ameitenga ya kula njiani ilikuwa imeisha kutokana na maandalizi duni ya safari yake hivyo alikuwa katika uhitaji mkubwa sana wa hela ya kula. Lakini baada ya jirani yake kugundua kuwa ni Mhaya mwenzake mara moja walianza kuzungumza Kihaya huku wakitambulishana maeneo ambayo wanatokea. Baadaya kufahamiana vizuri, mtafitiwa alieleza kuwa aliweza kujieleza juu ya shida aliyokuwa nayo, na haikuchukua muda aliweza kumpa msaada. Kwa mujibu wa mtafitiwa huyo, msaada alioupata ulikuwa ni matokeo ya kutambuana kwa njia ya lugha ya Kihaya.

Mtafiti alibaini kuwa hofu ya kupata msaada unapokuwa nje ya jamii yako iko kwa watu wengi hasa wanapokuwa katika jamii zingine katika maeneo ya mjini. Njia nyepesi ambayo jamii hii huitumia ni kuzungumza lugha ya Kihaya popote pale apatapo nafasi. Mwanaisimu Coulmas (2005) anaunga mkono hoja hii kwa kusema kuwa lugha ni utambulisho wa jamii, hutumiwa kama ishara ya mshikamano na hubainisha aina ya watu wanaotumia lugha hiyo kama lugha yao.

Mtafiti aligundua kuwa, Wahaya wengi huongea Kihaya hadharani kama njia ya kujitambulisha na hivyo kuongeza wigo wa ndugu. Wahaya wengi wakiwa nje ya wilaya zao, hujiona ndugu wa karibu sana wakifahamiana. Na njia nyepesi ya kufahamiana ni kuongea kihaya. Hii ndiyo sababu wazazi wengi huwahimiza watoto wao kujifunza na kupenda kuongea Kihaya popote pale walipo. Hii ina maana kuwa, lugha ya Kihaya itakuwa matumizi mengi zaidi katika jamii hivyo kuifanya kuwa lugha maarufu miongoni mwa jamii ya Kihaya. Kwa mantiki hii, lugha ya Kihaya

itakuwa na nguvu ya kuiathiri lugha ya Kiswahili hasa kifonolojia. Hii ni dhahiri kwani, mtu akibobea katika kuzungumza lugha moja, hulazimika kujifunza na miundo mingine ya lugha husika ikiwemo fonolojia. Hivyo, ni rahisi Mhaya kuongea lugha ya Kiswahili kwa fonolojia ya Kihaya kwani atashindwa kutamka baadhi ya maneno mengine ya Kiswahili kwa fonolojia husika.

### 4.5.12 Lugha ya Kihaya Kutumika kama Sehemu ya Kudumisha Utamaduni wa Jamii

Jamii ya Kihaya ni kati ya jamii ambayo hupenda kudumisha tamaduni zake katika jamii. Kwa kuwa lugha ni sehemu ya utamaduni wa jamii, jamii hii hupenda sana kutumia lugha ya Kihaya kama sehemu ya kudumisha mila zao. Mtafiti alibaini kuwa mambo mengi ya kitamaduni katika jamii ya Wahaya hufanywa kwa lugha ya Kihaya. Nyimbo nyingi zinazopendwa kwenye matukio ya kijamii kama harusi, misiba, sherehe za kijadi, huimbwa kwa lugha ya Kihaya. Hoja hii inapata nguvu kwani hata katika hafla za kiserikali, nyimbo zinazochaguliwa kuimbwa ni zile zinazoimbwa kwa lugha ya Kihaya.

Utafiti huu umebaini kuwa 95% ya watafitiwa wote waliohusika katika utafiti huu hasa wazazi hawako tayari kuona lugha ya Kihaya ikipotea miongoni mwa jamii ya Wahaya. Matokeo haya ya watafitiwa wazee yanaweza kutafsiriwa kuwa watafitiwa wazee wanadumisha utamaduni wa jamii ya Wahaya kwa kuendelea kutumia lugha ya Kihaya katika eneo la nyumbani.

Lakini pia lugha huakisi utamaduni wa wazungumzaji wake. Lugha ya Kihaya imebeba utamaduni pia wa Kihaya katika maana ya majina ya vyakula vyao, mavazi

yao, na salamu zao pia. Namna wahaya wanavyosalimiana ni tofauti na makabila mengine hata majina ya vyakula vyao ni tofauti na jamii zingine.

Kwa mfano, jamii ya Kihaya chakula chao kikuu ni ndizi, hivyo hujikuta lina majina mengi sana ya ndizi yanayotamkika kwa Kihaya kama vile; Embile, Ekonjwa, Akanana, Enshakala, Enyoya, Nyakasheshe, Enjugu, Enchocho, Enjoge, Entobe, Kainja, Akashubi, Entundu, na Mbile. Hata salamu zao utazisikia katika lugha ya Kihaya kama vile; maesipota salaamu kwa mama, tatasipota ambayo ni salaamu kwa baba wakati wa mchana.

Kigezo cha kudumisha utamaduni ndani ya kabila la Kihaya kunaipa nguvu lugha ya Kihaya kuwa na uhitaji mkubwa ndani ya jamii. Data za utafiti zinaonesha kuwa asilimia 78% ya wahojiwa wote walioulizwa kama wako tayari kujitenga na tamaduni za Kihaya walionesha kukataa. Ni asilimia 22% ya wahojiwa wote ndio waliokubali kuwa wanaweza kujitenga nautamaduni wa Kihaya. Hii ina maana kwamba, mtoto alazimishwa tu kuzungumza lugha ya Kihaya ili akubalike ndani ya jamii. Kwani inatafsrika kuwa kama mtoto hajui kuongea lugha ya Kihaya basi, huyo mtoto amepotea katika jamii.

## 4.6 Mbinu za Kuwasaidia Wanafunzi wa Kihaya Wanaojifunza Lugha ya Kiswahili

Katika utafiti huu inaonesha kuwa wanafunzi wa jamii ya Kihaya wameathirika kwa namna moja ama nyingine kifonolojia wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa utafiti huu, mwanafunzi aliyeathirika na lugha ya awali anaweza kusaidika pale ajifunzapo lugha ya pili kwa kufuata mbinu zifuatazo.

### 4.6.1 Watoto Wafundishwe Lugha ya Kiswahili Tangia Utotoni

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa, wanafunzi zaidi ya 90% ambao hushindwa kujifunza Kiswahili kwa ufasaha ni wale ambao lugha ya Kiswahili ni ya pili katika kujifunza. Utafiti umebainisha kuwa lugha ambayo mtoto hujifunza utotoni mwake huwa na nguvu sana katika maeneo yote ya lugha kwa maana kifonolojia, kimofolojia, semantiki, na sintakisia.

Katika utafiti huu tumesisitiza kuwa lugha Kiswahili inapaswa kufundishwa tangu utotoni kumjengea mawasiliano kama nadharia ya fonolojia zalishi asilia ambayo inasisitiza uhusiano kati ya watu. Pia wazazi au walezi wa watoto hao wahamasishwe ili waweze kutumia lugha ya Kiswahili katika kuwasiliana na waondoe fikra potofu kuwa mtoto kujua Kiswahili ndicho chanzo cha kupoteza utamaduni wa kabila lao au jamii yao. Kwahiyo, iwapo wazazi au walezi, watahamasika kwa pamoja, watoto wao watakuwa wazungumzaji wazuri wa lugha ya Kiswahili. Jitihada ziongezwe zaidi katika kufanikisha suala hilo. Asilimia 87 ya watafitiwa waliohojiwa walisema kuwa, walitaja njia hiyo kuwa, itapunguza athari hizo katika lugha Kihaya wakati wa kujifunza Kiswahili.

Kwa ujumla, katika utafiti huu mtafiti anasema kuwa msingi bora wa kuwa mahiri (mjuzi) katika lugha huanzia utotoni lugha inapaswa kufundishwa tangu utotoni, hali ambayo itamsaidia katika mawasiliano kwa baadaye. Vilevile wazazi au walezi wahamasishwe ili waweze kutumia lugha ya Kiswahili katika kuwasiliana na watoto wao na kuondoa imani potofu kuwa mtoto anapojifunza lugha ya Kiswahili ndiyo chanzo cha kupoteza utamaduni wao. Watakuwa wazazi wazuri wa lugha ya Kiswahili. Jitihada ziongezwe zaidi katika kufanikisha suala hili. Walimu kumi na tatu

tuliwatafiti. Pia kwa kufanya hivi itawafanya watoto wao kuwa wazungumzaji wazuri wa lugha ya Kiswahili.

Lugha ya asili ni lugha inayotokana na wanajamii wa eneo fulani ambao wana mila, desturi na utamaduni wa aina moja (Msanjila na wenzake 2009). Hivyo basi, lugha ya Kihaya ni lugha inayotokana na watu wa jamii ya Kagera. Jamii hii hutumia sana lugha ya Kihaya katika kuwasiliana kwao. Kihaya ni lugha ya awali kwa jamii ya watu wa Kagera na Kiswahili ni lugha ya pili ya kujifunza. Kiswahili ni lugha ya pili kwa watu wengi wa Tanzania.

### 4.6.2 Kuwepo na Uwiano Mzuri kati ya Walimu na Wanafunzi Shuleni

Ili mwanafunzi ajifunze lugha vizuri ni lazima kuwepo na mambo mbalimbali yatakayomsaidia mwanafunzi kujifunza kwa ufasaha. Mazingira hayo yanaambatana na uwepo wa walimu ambao huendana na idadi ya wanafunzi. Wadau wa elimu ni lazima kuzingatia uwiano mzuri wa wanafunzi na walimu kwa kila darasa. Hii itasaidia mwanafunzi kupata msaada wa haraka na sahihi pale anapouhitaji. Mtafiti aligundua kuwa kwa wastani shule zote alizotembelea kuna upungufu mkubwa wa walimu. Mtafiti alikuta kwa wastani kuna walimu 5 kwenye kila shule yenye wanafunzi kuanzia darasa la kwanza hadi la saba. Hii huwafanya walimu kushindwa kutoa msaada unaohitajika kwa mwanafunzi punde anapouhitaji msaada huo. Kwa mfano, mwalimu anayepaswa kufundisha vipindi 10 kwa wiki, hujikuta wakifundisha vipindi vingi kuliko uhalisia wa kazi.

### 4.6.3 Matumizi Sahihi ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Katika harakati za kuwasaidia wanafunzi wa jamii ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili, walimu hawana budi kutumia zana za kujifunzia na kufundishia ambazo

zitamsaidia mwanafunzi kujifunza kutamka maneno au misamiati ya lugha ya Kiswahili kwa ufasaha. Akifanfanua zaidi kuhusu zana mwalimu mmoja wa shule ya Minziro alisema kuwa, zana za kujifunzia ni vifaa au kifaa ambacho anatumia mwanafunzi katika kupata maarifa, wakati zana za kufundishia ni kifaa au vifaa ambavyo mwalimu anavitumia katika kufundishia wanafunzi wake awepo darasani.

Zana za matamshi mazuri ya sauti za Kiswahili kama zilivyoandikwa kwenye jedwali namba 2.1 na jedwali namba 2.4 zinaweza kutumika kuwasaidia wanfunzi kuondoa tatizo la kifonolojia kwa wanafunzi wa jamii ya Kihaya. Pia kamusi ya Kiswahili, upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada, vitini vilivyochorwa alama za sauti, vitini vilivyochorwa picha zilizochorwa namna ya kutamka na mahali pa kuzitamkia vinaweza kutimika kuwasaidia wanafunzi na kuelewa kwa haraka zaidi.

Kwa mujibu wa mwalimu huyu wa shule ya msingi Kalagala, zana za kufundisha na kufundishia zinalenga kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa kwa njia nyepesi zaidi kuliko ya kutumia maelezo. Kauli hii aliyoitoa mwalimu mkuu wa shule mojawapo iliyofanyiwa utafiti alipokuwa akijadili mbinu za kuwasaidia wanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Kauli hii iliungwa mkono na mwalimu wa shule shule ya msingi Kyanumbu ambaye alitoa zana ambazo huwa anazitumia kuwafundishia wanafunzi wa darasa la kwanza huku akielezea namna zinavyomsaidia katika kufundisha wanafunzi wa jamii ya Kihaya lugha ya Kiswahili.

Katika zana hizo, mtafiti aliona chati zenye herufi mbalimbali za Kiswahili zikiwa zimechorwa picha na kuambatanishwa na maneno ya Kiswahili. Mfano “silabi” /g/ iliambatanishwa na picha “gari”. Baada ya kuonesha zana hizi, walimu walipata nafasi

ya kusikiliza namna zana hizo zinavyowasaidia wanafunzi katika kutofautisha sauti na kutamka sauti kwa ufasaha. kwa mujibu wa mwalimu wa shule ya msingi Kiwelu, yeye alisema matumizi ya zana humsaidia sana kwani hupunguza muda wa kuelezea jambo kwa muda mrefu.

Mtafiti alibaini kuwa 90% ya walimu wanaofundisha darasa la awali hadi darasa la pili kwa shule zote alizotembelea wanatumia zana katika ufundishaji wao. Ila changamoto kubwa aliyoiona mtafiti ni kuwa, walimu wengi wanatumia zana za kununua ambazo ni ghali ukilinganisha kama ambavyo wangetumia zana za kutoka katika mazingira yao, au kutengeneza. Matumizi ya zana za kununua ni kasumba ambayo imejengekeka minongoni mwa walimu wengi wanaoamini kuwa ili uonekane umetumia zana ni lazima uwe umeitoa dukani. Lakini pia mtafiti alibaini kuwepo kwa changamoto kubwa ya utunzwaji wa zana mara baada ya kuzitumia. Wengi wa walimu walionekana kuwa na zana mpya ambazo zinanunuliwa kila mwaka hali ambayo ingeepukwa kwa kuwepo na utunzwaji mzuri wa zana za kujifunzia na kufundishia.

### 4.6.4 Kuepuka Matumuzi ya Lugha Mbili za Kufundishia

Kwa mujibu wa utafiti huu, mtafiti amegundua kwamba, ili kuwasaidia wanafunzi wa jamii ya Kihaya kujifunza vizuri na kwa ufasaha lugha ya Kiswahili, mwalimu lazima awe mahiri katika umilisi wa lugha ya Kiswahili. Hii itasababisha uwepo kwa ufundishaji mzuri wa lugha ya Kiswahili darasani. Katika utafiti, imeonekana kwamba baadhi ya walimu hasa wanaofundisha madarasa ya awali kwa maana ya darasa la awali, darasa la kwanza hadi la tatu, aghalabu hukosa elimu mwafaka wafundishapo lugha ya Kiswahili. Hii hupelekea walimu hasa wale ambao wanajua lugha ya Kihaya

kuwasiliana na wanafunzi kwa lugha ya Kiswahili na Kihaya. Hali hii huwafanya wanafunzi kujihisi huru zaidi watumiapo lugha ya Kihaya hata wakiwa katika mazingira ya shule. Mtafiti aliona wanafunzi wakiwasiliana wao kwa wao kwa lugha ya Kihaya ndani ya darasa. Mwalimu aliyekuwepo darasani alipoulizwa ni kwa nini wanafunzi wanawasiliana kwa lugha ya Kihaya darasani, alisema;

> Yaani hawa wanafunzi wewe acha tu, tumeongea waache hiyo tabia lakini hawasikii. Jana tu niliwapa adhabu ya kufagia darasa wale waliokuwa wanaongea kilugha darasani, ona na leo wanazungumza tena mbele ya wageni.

Akizungumza kwenye mahojiano walimu mmoja wa shule ya msingi ambaye anafundisha darasa la kwanza alisema kuwa;

> Sisi walimu tunaofundisha madarasa ya chini kwa maana ya darasa la awali na la kwanza huwa tunapata shida sana katika kuwasiliana na wanafunzi wetu. Kuna wakati huwa tunalazimika kutoa matangazo kwa lugha ya Kihaya na Kiswahili ili wanafunzi wakuelewe. Mara nyingi huwa tunawatumia walimu ambao ni wahaya au wanaojua lugha ya Kihaya.

Mtafiti alishihudia wakati wa kuwaruhusu wanafunzi wa darasa la kwanza walimu wakitoa matangazo kama ifuatavyo;

Mwalimu mmoja alianza kwa kusema kwa Kiswahili, sentensi hii

> "kesho njooni na jembe"

Baada ya kusema hivyo, mwalimu mwingine alisimama na kutafsri kwa lugha ya Kihaya kwa kusema;

> "nyenkya mwije nenfuka" akimaanisha ""kesho njooni na jembe"

Data za utafiti huu zinaonesha kwamba wanafunzi wengi wa wilaya ya Misenyi wanapokuwa wanataka kujifunza lugha ya Kiswahili inakuwa ni vigumu kwa sababu hawana msamiati wa kutosha wa ile lugha nyingine na hivyo kujikuta wakishindwa kuelewa baadhi ya mambo katika kujifunza, kwa sababu ya upungufu wa msamiati wa lugha ya kujifunzia.

Katika utafiti huu, matafiti amebaini kwamba, lugha ya Kiswahili imeathiriwa sana na lugha za Kihaya katika jamii ya Misenyi. Hivyo, lugha mama humuathiri mtu anayejifunza lugha nyingine katika matamshi, maana, msamiati, na sarufi matokeo yake utaona mtu anahangaika kubadilisha maneno ya Kihaya kwenda Kiswahili.

Wanafunzi wao walipohojiwa na mtafiti baada ya kutoka darasani kutaka kujua kwa nini wanaongea lugha ya Kihaya hata wakiwa darasani walisema;

> Kwa kweli mimi huwa naongea lugha ya Kihaya kila siku hata nikiwa shule. Ni mara chache sana kuongea Kiswahili nikiwa na wenzangu. Huku kwetu, ukimsemesha mhaya mwenzako kwa lugha ya Kiswahili utaonekana wewe ni mswahili na wenzako wataanza kukutenga. Haya mazoea ndiyo hunipelekea mimi na wengine kujikuta tunaongea Kihaya hata tukiwa darasani.

Mwanafunzi mmoja wa darasa la sita yeye alipotakiwa kujibu kwa nini huongea lugha ya Kihaya hata wakiwa darasani alisema kuwa;

> Hakuna shida kuongea lugha ya Kihaya ukiwa darasani kwani hata walimu huwa tunawasiliana nao kwa lugha ya Kihaya kwa hiyo huku kwetu haya ni mambo ya kawaida tu.

Mtafiti alibaini kuwa, ni kweli walimu hutumia lugha ya Kiswahili na Kihaya katika kuwasiliana na wanafunzi. Mara nyingi mawasiliano hayo hufanyika nje ya shughuli za shuleni au kitaaluma. Wanafunzi wanapoona hivyo, huona kama ni fursa kwao kuendeleza kutumia lugha ya Kihaya katika kuwasiliana na walimu wao kwani huona kama lugha ya Kiswahili ni nzito kuitumia ukilinganisha na lugha ya Kihaya. Walimu wanapolazimika kutumia lugha ya Kihaya katika kuwasiliana na wanafunzi hulenga kuwapungunzia mzigo wa kuelewa kile wanachofundisha, bila kujua kuwa hilo ni kosa katika kuwasidia wanafunzi.  Kwa mujibu wa utafiti huu, matumizi ya lugha mbili katika ufundishaji ni tatizo sugu kwani hata walimu wanaofundisha somo la Kiingereza hulazimika kuchanganya na lugha ya Kiswahili na Kihaya katika kuelezea misamiati wa lugha ya Kiingereza.

Alipotakiwa kuelezea kwa nini hutumia mbinu ya kuchanganya lugha mbili wakati wa kufundisha lugha ya Kiswahili, mwalimu mkuu wa shule mojawapo alisema kuwa hii hutokea kwani ukitumia lugha ya Kiswahili kuanzia mwanzo hadi mwisho, wanafunzi watakaokuelewa na wachache sana, wengi watatoka wakiwa hawajaelewa. Kauli hii iliungwa mkono na mwalimu wa darasa la pili katika shule ya msingi Nyakahanga ambaye alisema kuwa ni vigumu sana kufundisha wanafunzi wetu hawa bila kuchanganya lugha. Kwa mujibu wa utafiti, uchanganyaji wa lugha mbili huleta madhara makubwa kwenye fonolojia ya lugha inayojifunzwa. Mwanafunzi anaweza kuelewa maana ya kilichofundishwa lakini akaashindwa kutofautisha matumizi ya fonolojia husika.

Mtafiti anaona kuwa walimu wa somo la Kiswahili kwa upande mwingine wanapaswa kuwajibika katika ufundishaji wa lugha ya pili, wanapaswa kujitolea kuwasaidia

wanafunzi wao katika Kiswahili. Kwa ujumla, mtafiti anapendekeza kuwa wanafunzi wafundishwe vizuri wanapokuwa darasani juu ya matamshi sahihi ya maneno ya Kiswahili ili kuondoa tatizo la athari katika lugha ya kwanza. Licha ya hayo baadhi walimu hukosa ujuzi wa kutosha katika lugha kwa kuwa baadhi yao hutumia mbinu zisizofaa zikiwemo ujumlishaji wa kiholela na pia matumizi mabaya ya sheria za lugha husika.

### 4.6.5 Mwalimu Atumie Lugha ya Kiswahili Fasaha

Katika utafiti huu, matafiti alibaini kuwa mwalimu ili aweze kuwa msaada kwa wanafunzi wake inabidi yeye mwenyewe awe hodari wa lugha anayotumia yaani Kiswahili. Mwalimu lazima ajue fonolojia nzuri ya maneno yote ya lugha ya Kiswahili. Mwanafunzi hujifunza lugha kwa kusikia mwalimu wake anavyozungumza na kutamka maneno ya lugha hiyo. Mwanafunzi anaposikia matamshi mabaya kutoka kwa mwalimu wake, naye hufanya makosa hayohayo bila kujua kuwa amekosea.

Katika utafiti huu, mtafiti alikutana na walimu wengi ambao wanatoka katika jamii ya Kihaya. Wengi wao ni wale walioomba uhamisho kutoka walipokuwa wanafundisha ili kukaa jirani na ndugu zao au familia zao. Kwa kuwa na wao ni wahanga wa lugha ya awali, hivyo hujikuta wamefanya makosa mengi ya kifonolojia bila wao kujua. Hivyo mwanafunzi naye ataathiriwa na kufanya makosa hayohayo kutokana na matamshi ya mwalimu wake. Mwanafunzi huyachukua makosa yale na kuyachukulia kama maumbo au sauti sahihi, hufanya hivi kwa kusahihisha sarufi ili kufikia utimilifu. Athari hizi hutokea katika ngazi mbalimbali kama vile katika ngazi ya sauti, pale ambapo sauti aliyoizoea katika lugha yake ya Kihaya haipatikani katika lugha ya pili ya Kiswahili.

### 4.6.6 Wazazi Waweke Kipaumbele cha Kuzungumza Lugha ya Kiswahili

Wazazi wanapaswa kufanya kila jitihada ili kuwa vielelezo katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa watoto wao, hasa wakiwa nao nyumbani. Wazazi wanapaswa kuienzi lugha hii ya Kiswahili kwa kuwasiliana na watoto wao na hata kuwasaidia katika mazoezi ya kuongea wakiwa nyumbani. Hali hii itasaidia sana wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kuwajengea msingi na uwezo zaidi wa kujiamini wanapokuwa wanazungumza lugha ya Kiswahili mbele ya watu wengine. Kutokana na hali hiyo itasaidi jamii ya kabila la wahaya kuwajengea watoto wao moyo wa kupenda kusoma vitabu mbali mbali vya hadithi vinavyohusiana na lugha ya Kiswahili, lengo ni kukuza suala zima la mawasiliano. Pia lugha hii itawaunganisha wanajamii wa kabila la Kihaya kufahamiana na watu wengi.

## 4.7 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amefafanua athari zilizopo za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili, kubainisha sababu ambazo zinaifanya lugha ya Kihaya iweze kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, na kuchambua mbinu za kutumia ili kuwasaidia wanafunzi wa Kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili. Katika sura hii mtafiti amegundua kuwa baadhi ya maneno yanayodhihirisha athari katika lugha ya Kihaya katika kujfunza Kiswahili Kama vile mifumo ya sauti kutokana na miundo ya maneno. Sura ifuatayo itajadili hitimisho, muhtasari na mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii huelezea muhtasari wa utafiti, mapendekezo na hitimisho la utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza athari ya lugha ya Kihaya katika kujifunza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi. Katika kufanya utafiti huu, mtafiti aliongozwa na malengo makuu matatu ambayo ni; Kwanza, kuainisha athari za lugha ya Kihaya zinazoathiri wanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Pili, kubainisha sababu zinazopelekea wanafunzi kuathiriwa na lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Tatu, kufafanua mbinu mbalimbali za kusaidia wanafunzi wanaojifunza kiswahili kama lugha yao ya pili.

Utafiti huu ulifanyika katika wilaya ya Misenyi ambayo inapatikana katika mkoa wa Kagera. Utafiti huu ulichunguza maoni, mitazamo, na uelewa wa walimu, wanafunzi na wazazi hasa kaatika kuchunguza athari za lugha ya Kihaya katika kujifunza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi. Katika kufikia lengo la utafiti, mtafiti alitumia watafitiwa 297 ambao walitumika kama sampuli ya utafiti huu. Kigezo kikubwa kilichotumika katika kuwapata watafitiwa ilikuwa ni Wahaya wanaojua kuongea lugha ya Kihaya na wanaishi katika wilaya Missenyi. Mtafiti aliamua kutumia lugha ya Kihaya kama sehemu ya kigezo kikuu kwani kinaendana na lengo mama la utafiti huu.

Mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji wa data za utafiti ambazo ni hojaji, mahojiano, na majadiliano ya vikundi. Pia utafiti huu ulitumia mkabala wa uwandani

na maelezo katika ukusanyaji wa data. Data za utafiti huu zinaonesha kuwa kuna tofauti kubwa ya mfumo wa fonolojia za Kihaya na Kiswahili ambayo huathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kihaya.

Aidha, matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba wanafunzi wa kabila la Kihaya walishindwa kutofautisha baadhi ya sauti kama /ð/ na /z/, /ɵ/ na /s/, /γ/ na /g/, /ɿ / na /g/, /tʃ/ na /ki/, /r/ na /l/, /s/ na /ʧ/. Lakini pia data za utafiti zinaonesha kuwa wanafunzi walikuwa wanaongeza Viambishi Visivyohitajika katikati mwa Neno kama vile Muzee badala ya mzee, nawo badala ya nao, muji badala ya mji, waitu badala ya watu, pia kulikuwa na athari ya uchopekaji wa silabi mwanzoni mwa neno kwa maneno kama "eshule" badala ya "shule" na "omuchele" badala ya "mchele". Athari nyingine ya kifonolojia iliyojitokeza ni uongezaji wa viambishi mwishoni mwa neno, mathalani, wanafunzi waliotamka vizuri neno "Nipe" walitamka "Nipepo". Pia kulikuwa na athari ya upunguzaji wa viambishi katika maneno ambapo wanafunzi wengi wakati wa kutamka, fonimu /h/ huwa haitajwi katika matamshi yao. Mfano neno "Hayupo" linatamkwa "Ayupo", neno "Hatari" hutamkwa "Atari". Data za utafiti pia zinaonesha kuwa kulikuwa na athari ya kifonolojia katika kubadilisha msamiati, Kwa mfano, neno /gari/ wao walitamka /ɛmɔtɔka/, "Machoni" akimaanisha "Mbele".

Utafiti pia uliangaza katika kutafuta sababu zinazofanya lugha ya kihaya iweze kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Data za utafiti zinaonesha kuwa sababu hizo ni matumizi makubwa ya katika shughuli za mawasiliano, uhusiano wa karibu kati ya lugha ya Kihaya na Kiswahili, kupewa hadhi ya juu katika shughuli za kijamii, ufahari wa kutumia lugha ya asili, mazingira duni ya kujifunza lugha ya Kiswahili, lugha ya

kihaya hutumika kama utambulisho, na kudumisha utamaduni wa kihaya. Kwa mujibu wa utafiti, kuna mbinu mbalimbali ambazo zinaweza kutumika katika kuwasaidia wanafunzi wa kihaya wanaojifunza lugha ya Kiswahili, mbinu hizo ni kama vile; watoto wafundishwe lugha ya Kiswahili tangia utotoni, kuwepo kwa mazingira rafiki ya kujifunza lugha ya Kiswahili, matumizi sahihi ya zana za kufundishia na kujifunzia, kuepuka matumzi ya lugha mbili za kufundishia, mwalimu atumie lugha ya Kiswahili vizuri, wazazi waweke kipaumbele cha kuzungumza lugha ya Kiswahili wawapo nyumbani.

## 5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu, mapendekezo mbalimbali yametolewa na mambo yafuatayo yamependekezwa nayo ni:

Kwanza, utafiti huu umeshughulikia athari za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili, mtafiti anapendekeza kwamba, watafiti wengine wanaweza kufanya utafiti juu ya athari za lugha nyingine za Kibatu zinazotokana na tofauti za kisarufi baina ya lugha mbili.

Pili, utafiti huu umeshughulikia kipengele kimoja tu cha kiisimu ambacho ni cha fonolojia, hivyo watafiti wengine wanaweza kushughulikia athari zingine za kiisimu kama kimsamiati, na kimaana.

Tatu, utafiti huu umezingatia kuona athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili, hivyo basi utafiti mwigine unaweza kufanywa kuona namna ambavyo lugha za kanda ya ziwa Victoria zinavyoathiriana kifonolojia.

## 5.6 Hitimisho

Utafiti uliofanyika katika wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, uliokuwa unachunguza athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili umehitimishwa katika sura hii. Mtafiti alielezea muhtasari wa utafiti kwa kuangalia malengo mahsusi ya utafiti, eneo utafiti ulipofanyikia, idadi ya watafitiwa, nadharia iliyoongoza utafiti huu, mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji wa data za utafiti na matokeo ya utafiti huu kwa ufupi.

**MAREJELEO**

Babbie, E. (1992). *The Basics of Sociol Research.* Belmont: Wadsworth Publishing Company

Barton, H. D. (1980). "*Language Use among Ilala Residents." In Polome and Hill (eds) Language in Tanzania.* Oxford: Oxford University Press.

Berg, B. C. (2007). Qualitative Research methods for the social sciences (6th Edition). Calfornia: Pearson Educational Inc.

Bosha, I. (1993). *Taathira za Kiarabu katika Kiswahili pamoja na Kamusi Thulathiya.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Brown, T. (1993). Acquisition of English Syntax by Keiyo L1 Speakers. Upublished M.A Dissertation, University of Egerton, Kenya.

Chomsky, N., na Halle, M. (1968). You can't Learn without Goofing. In J. C. Richards (Mh.), *ErrorAnalysis*. London: Longman.

Cook, R., Rodman, R., na Hyams, N. (1969). *An Introduction to Language (8thed.)*. Boston, MA: Thomson Wadsworth.

Corder, S. P. (1967). The Significance of Learners Errors. *International Review of Applied Linguistics in Language teaching, 5(2),* 161-170.

Curtain, E. (1990). The Impact of Bantu Languages in English Language Learning Processes in Tanzania Secondary Schools. *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili,* 2000, 287 – 296.

Ewan, C., and Calvert. D. (2000). *The Crisis of Scientific Research, in Garrick CAL* New York: Sage Publications.

Enon, C. J. (1998). *Educational Research, Statistics and Measurement.* Kampala: Makerere University.

Ghanem, R. (2005). Understanding the Transfer of Prepositions. *Forum, 38(3)*, 67-80.

Giles, H., and Byrne, J. L. (1982), "An Intergroup Approach to Second LanguageAcquisition." *Journal of Multilingual and Multicultural Development,* 3(19), 17-40.

Giles, H. (1979). *"Ethnicity Markers in Speech." In K.R. Scheres and H. Giles (eds.).* London: Cambridge University Press.

Goldsmith, J. A. (1990). *Autosegmental and Metrical Phonology*. London: TJ Press Ltd.

Habwe. J., and Karanja, P. (2004). *Msingi wa sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers

Hagège, C. (1999). The Child between Two Languages. In M. Karra. *Second Language Acquisition: Learners' Errors and Error Correction in Language Teaching*. New York: Cambridge University Press.

Haule, F. (2014). Muundo wa Njeo za Lugha ya Kingoni. Tasnifu za Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.

Hooper, J. (1976). *Introduction to Genative Phonology.* Nairobi: Oxford University press.

Iribemwangi, P. I. (2010). The Use of Overgeneralization and Transfer Learning Strategies by Elementary and Intermediate Students of ESL. *Language Learning, 25(3),* 73-107.

Kahn, D. (1976). Syllable – Based Generalization in English Phonology. PhD Dissertation. MIT. (Published by Garland, 1980).

Katamba, F. (1989). *An Introduction to Phonology.* New York: Longman Publishers.

Katoke, K. I. (1970) "The Making of Karagwe Kingdom." In *Tanzanian History from Oral Traditions*. Nairobi: East African Publication House.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. ( 2006). *Proposal and Thesis Writing: Introduction.* Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, R. C. (2009). *Research Methodology; Methods and Techniques.* New Delhi New Age International (P) Ltd.

Krashen, S. D., na Tracy D. T. (1987). The Natural Aproach Language Acquisition in The Classroom. Oxford: Pergamon Press.

Lucius, M. T. (1978). *Misingi ya Kiswahili,* Dar es Salaam: Mhenga publishing Consultants Company Limited.

Masebo, J. A. na Nyangwine, N. (2008), Nadharia ya Lugha.Kiswahili 1.Kidato cha 5 Na 6. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Massamba D. P. B. (2001). Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo

Massamba, D. P. B. (1986). On the Influence of Local Languages on Kiswahili: The Case of Mara Region in Tanzania. *Kiswahili*, 53/1 na 53/2, 67-83.

Mdee, D., na Mangwa, D. O. (2011). Athari za Kikisii katika Kiswahili na Zinavyochangia Matokeo Mabaya ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili kwa Wanafunzi Wakisii Wilayani Kisii Kusini. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Mgullu, R. S. (2001). *MTAALA WA ISIMU: Fonetiki,Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhom Publishers.

Mgullu, R. S. (2012). *Mtalaa wa Isimu Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mhilu, G. D. (2005). Language It's Nature and Use. Retrieved on 2nd October 2018 from: http://www.bhojvirtualuniversity.com/slm/B.Ed_SLM/bedteb1u1.pdf.

Mligo, E .S. (2012). *Jifunze utafiti mwongozo kuhusu utafiti na utamaduni wa ripoti yenye Mantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGY)

Msanjila, P. Y. (2009). *Isimu Jamii: Sekondari na Vyuo. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Mudhune, D. R. (2008). Athari za Kifonolojia kwa Wasemaji wa Dholuo Wanaojifunza Kiswahili.Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Mudhune, E. S. (1994). A Contrastive Analysis Approach to the Learning of Swahili Morphosyntax by Luo Speakers. Tasnifu ya M.A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Mukuthuria, M. (2004). Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na Wanafunzi wa Kitigania, Kenya. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Munyua, J. G. (2002). The Emerging Viswahili and Kiswahili Research. Katika K. I. Simala (Mh.) *Jarida la Utafiti wa Kiswahili* (kur. 97 – 107). Eldoret: Moi University Press.

National Bureau of Statistics, (2012). Ministry of Finance Dar es Salaam, population and housing census Population Distribution by Administrative Areas and March, 2013, Office of Chief Government Statistician President's Office, Report of Finance, Economy and Development Planning, Dar es Salaam, TZ.

Neuman, W.L. (1991) *Social Research Methods*. Washington, DC: Allyn and Bacon.

Ngugi, J. K. (2007). Uchunguzi wa Taathari za Kifonolojia miongoni mwa Wanafunzi Wagikuyu: Mfano kutoka Tarafa ya Bahati, Nakuru.Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Nkwera, F. M. V. (1979). Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Nyagah, E. (2016). The Impact of Kiswahili Language on Ethnic Languages: A Case Study from Handeni District. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Ontieri, J. O. (2010). Uchanganuzi wa Makosa katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Wilaya ya Nakuru, Kenya. Tasnifu ya Uzamifu (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu Cha Egerton, Kenya.

Polomé, E. (1980) "The Languages of Tanzania." In Polomé, Edgar & C.P.Hill (eds.) *Language in Tanzania*. Oxford: Oxford University Press,

Raum, J. (1925). "Consideration for the Tribe as Lacking in the Syllabuses." In *Tanganyika Territory, Proceedings of the Advisory Committee of Native Education at the Sixth Meeting*. 1929, Dar es Salaam.

Richards, J. C. (1984). *Error Analysis: Perspectives on Second Language Acquisition*. London: Longman.

Richards, J. C. (1974). *Error Analysis and Second Language Strategies. In J. H. Schumann and N. Stenson (Wah.), New Frontiers in Second Language Learning.* Rowley, Mass: Newbury House.

Rubanza, Y. I. (1979). The Relationship between Kiswahili and other African Languages: The Case of Kihaya. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Selinker, L. (1972). *Inter Language.* New York: Rawlence Erlbaum Associates.

Sigh, K. (2007). *Quantitative Social Research Methods*: New Delhi: Sage Publications Inc.

Tabouret-Keller, A., and Le Page, R. B. (1986). “The Mother Tongue Metaphor.” Grazer Linguiscle Studien.

Vennemann, T. (1971). Morphological marking or syntactic relations in bantu languages. Unpublished dissertation of University of Dar es salaam, Tanzania

Wenceslaus, M. (2015). Athari za lugha ya kijita katika Kujifunza Kiswahili: Tasnifu ya shahada ya uzamili m.a (kiswahili) kitivo cha sanaa na sayansi ya jamii. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Williman, N. (2011). *Research Methods; The Basic*. New York, Routledge.

Yule, G. (1996). *The study of Language Cambridge.* London: University London Press.

## VIAMBATISHO

**Kiambatisho Namba 1: Hojaji la Wanafunzi**

Habari mpendwa mtafitiwa, Mimi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti kuhusu ***"Athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili"***. Kwa heshima kubwa, ninakuomba muda wako ili uweze kujaza hojaji hili. Tafadhali jaza hojaji hii kadiri unavyojua au kulingana na uzoefu wako mwenyewe bila ya kumhusisha mtu mwingine. Kila taaria itakayotolewa hapa itatumika kwa ajili ya kitaaluma tu na si vinginevyo.

**SEHEMU A: MAELEZO YA JUMLA**

i. Tafadhali usiandike jina lako katika hojaji hii

ii. Jibu swali kulingana ulivyoulizwa wenye swali husika

iii. Pale unapoona utata katika swali, usisite kuuliza kwa mtafiti

**SEHEMU B: TAARIFA BINAFSI ZA MTAFITIWA**

Weka alama ya (√) kwa kile unachokifikiria kuwa ni sahihi kwako mahali penye mabano [ ]

**Maswali:**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Miaka yako | (a) 5- 10 | [ ] | (b) | 11 -12 | [ ] |
| | | (c) 13- 14 | [ ] | (d) | 14- 15 | [ ] |
| 2. | Jinsia | (a) me | [ ] | (b) | ke | [ ] |
| 3. | Darasa lako | (a) IV | [ ] | (b) | V | [ ] |
| | | (c) VI | [ ] | (d) | VI | [ ] |

**SEHEMU C: WEKA ALAMA YA (√) KWENYE HERUFI AMBAYO UNAFIKRIA NI SAHIHI PENYE MABANO [ ]**

4. Je, wewe unaishi katika wilaya ya Misenyi?

   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

5. Je, wewe ni miongoni mwa watu wanaotokea katika kabila la Kihaya?

   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

6. Kama swali (5) ni "Ndiyo", je Kihaya ni lugha yako ya kwanza kwako?

   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

7. Je unafahamu kuongea na kuandika Kiswahili?

   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

8. Uwapo nyumbani ni lugha ipi huwa unaitumia zaidi katika mawasiliano?

9. (A) Kiswahili [ ] (B) Kihaya [ ]

10. Je, uwapo shuleni, ni lugha ipi huwa unaitumia zaidi katika mawasiliano?

    (A) Kiswahili [ ] (B) Kihaya [ ]

11. Ni eneo lipi huwa unatumia lugha ya Kihaya sana kuliko lugha ya Kiswahili

    (A) Eneo la ibada [ ] (B) Sokoni [ ]

    (C) Msibani [ ] (D) Sherehe [ ]

12. Ni eneo lipi huwa unatumia lugha ya Kiswahili sana kuliko lugha ya Kihaya

    (A) Eneo la ibada [ ] (B) Sokoni [ ]

    (C) Msibani [ ] (D) Sherehe [ ]

**SEHEMU D: JAZA TAARIFA ZAKO SEHEMU PALIPO NA NAFASI**

13. Andika maneno walau 10 ya lugha ya Kihaya

(A) ……………………….……….. (B) …………….………………

(C) ………………………………… (D) …………………………….

(E) ………………….……………… (F) …………..…………………

(G) ……………………..……….. (H) …..…………………………

(I) …………………...…………… (J) ……...………………………

14. Maneno uliyoyaandika katika swali 4, yaandike kwa lugha ya Kiswahili

(A)……………………….……….. (B) …………….………………

(C) ………………………………… (D) …………………………….

(E) ………………….……………… (F) …………..…………………

(G) ……………………..……….. (H) …..…………………………

(I) …………………...…………… (J) ……...………………………

15. Taja maneno 10 ambayo kila wakati ukiyatamka, mwalimu huwa anakurekebisha katika kutamka.

(A)……………………….……….. (B) …………….………………

(C) ………………………………… (D) …………………………….

(E) ………………….……………… (F) …………..…………………

(G) ……………………..……….. (H) …..…………………………

(I) …………………...…………… (J) ……...………………………

16. Je kuna ugumu wowote unaokutana nao unapojifunza lugha ya Kiswahili? kama upo tafadhali eleza,

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………

17. Je, mwalimu huwa unatumia mbinu zipi kukurekebisha pale unapokosea kutamka vizuri matamshi ya kiswahili?

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………

**Asante sana kwa ushirikiano wako katika kujaza hojaji hii.**

**Kiambatisho Namba 2: Hojaji la Walimu na Wazazi na Wazazi**

Habari mpendwa mtafitiwa, Mimi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti kuhusu ***"Athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili"***. Kwa heshima kubwa, ninakuomba muda wako ili uweze kujaza hojaji hili. Tafadhali jaza hojaji hii kadiri unavyojua au kulingana na uzoefu wako mwenyewe bila ya kumhusisha mtu mwingine. Kila taaria itakayotolewa hapa itatumika kwa ajili ya kitaaluma tu na si vinginevyo.

**SEHEMU A: MAELEZO YA JUMLA**

iv. Tafadhali usiandike jina lako katika hojaji hii

v. Jibu swali kulingana ulivyoulizwa wenye swali husika

vi. Pale unapoona utata katika swali, usisite kuuliza kwa mtafiti

**SEHEMU B: TAARIFA BINAFSI ZA MTAFITIWA**

Weka alama ya (√) kwa kile unachokifikiria kuwa ni sahihi kwako mahali penye mabano [ ]

**Maswali:**

**A. TAARIFA BINAFSI ZA MTAFITIWA**

Mahali penye mabano [ ] weka alama ya (√) kwa kile unachokifikiria kuwa ni sahihi kwako.

1. Miaka yako (a) 18- 25 [ ] (b) 26- 30 [ ]
   (c) 31-40 [ ] (d) 41-50 [ ]
   (e) 51 na zaidi [ ]
2. Jinsia (a) Me [ ] (b) Ke [ ]

3. Kiwango chako cha elimu (a) Sijasoma [ ] (b) Msingi [ ]
(c) Sekondari [ ] (d) Chuo [ ]

**SEHEMU C: WEKA ALAMA YA (√) KWENYE HERUFI AMBAYO UNAFIKRIA NI SAHIHI PENYE MABANO [ ]**

18. Je, wewe ufanya kazi katika wilaya ya Misenyi?

    (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

19. Je, wewe ni miongoni mwa watu wanaotokea katika kabila la Kihaya?

    (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

20. Kama swali (5) ni "Ndiyo", je Kihaya ni lugha yako ya kwanza kwako?

    (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

21. Je unafahamu kuongea lugha ya Kihaya?

    (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

22. Uwapo katika maingira ya nyumbani ni lugha ipi huwa unaitumia zaidi katika mawasiliano?

    (A) Kiswahili [ ] (B) Kihaya [ ]

23. Je, uwapo shuleni, ni lugha ipi huwa unaisikia zaidi wanafunzi wakiwasiliana wao kwa wao?

    (A) Kiswahili [ ] (B) Kihaya [ ]

24. Ni eneo lipi huwa lugha ya Kihaya huwa inatumika sana kuliko lugha ya Kiswahili

    (A) Eneo la ibada [ ] (B) Sokoni [ ]

    (C) Msibani [ ] (D) Sherehe [ ]

25. Ni eneo lipi huwa lugha ya Kiswahili huwa inatumika sana kuliko lugha ya Kihaya

(A) Eneo la ibada [ ] (B) Sokoni [ ]

(C) Msibani [ ] (D) Sherehe [ ]

**SEHEMU D: JAZA TAARIFA ZAKO SEHEMU PALIPO NA NAFASI**

26. Andika maneno walau 10 ya lugha ya Kihaya ambayo wanafunzi hupenda kuyatamka wakiwa shuleni

(B) ……………………….……….. (B) …………….……………

(C) ………………………………… (D) …………………………….

(E) ………………….…………… (F) …………..…………………

(G) ……………………..……….. (H) …..…………………………

(I) ……………………...…………… (J) ……...………………………

27. Taja maneno 10 ambayo wakati wanafunzi huyatamka kimakosa.

(A)……………………….……….. (B) …………….……………

(C) ………………………………… (D) …………………………….

(E) ………………….…………… (F) …………..…………………

(G) ……………………..……….. (H) …..…………………………

(I) ……………………...…………… (J) ……...………………………

28. Je kuna ugumu wowote unaokutana nao unapofundisha wanafunzi wa Kihaya darasani hasa katika utamkaji wa maneno ya Kiswahili? kama upo tafadhali eleza,

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………….……………

29. Hapa kwenye, huwa mnatumia maziwa ya wanyama gani?

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………….……………

30. Je, kama mwalimu huwa unatumia mbinu zipi kuwarekebisha wanafunzi pale wanapokosea kutamka vizuri matamshi ya kiswahili?

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………….……………

**Asante sana kwa ushirikiano wako katika kujaza hojaji hii.**

**Kiambatisho Namba 3: Mahojiano - Wanafunzi**

Habari mpendwa mtafitiwa, Mimi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti kuhusu ***"Athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili"***. Kwa heshima kubwa, ninakuomba muda wako ili uweze kujaza hojaji hili. Tafadhali jaza hojaji hii kadiri unavyojua au kulingana na uzoefu wako mwenyewe bila ya kumhusisha mtu mwingine. Kila taaria itakayotolewa hapa itatumika kwa ajili ya kitaaluma tu na si vinginevyo.

**SEHEMU B: TAARIFA BINAFSI ZA MTAFITIWA**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Miaka yako | (a) 8- 10 | [ ] | (b) | 11 -12 | [ ] |
| | (c) 13- 14 | [ ] | (d) | 14- 15 | [ ] |
| 2. Jinsia | (a) me | [ ] | (b) | ke | [ ] |
| 3. Darasa lako | (a) IV | [ ] | (b) | V | [ ] |
| | (c) VI | [ ] | (d) | VI | [ ] |

**SEHEMU C: KUWEKA ALAMA YA (√) KWENYE HERUFI AMBAYO NI SAHIHI PENYE MABANO [ ]**

4. Je, wewe unaishi katika wilaya ya Misenyi?

   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

5. Je, wewe ni miongoni mwa watu wanaotokea katika kabila la Kihaya?

   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

6. Kama swali (5) ni "Ndiyo", je Kihaya ni lugha yako ya kwanza kwako?

   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

7. Je unafahamu kuongea na kuandika Kiswahili?

   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

8. Uwapo nyumbani ni lugha ipi huwa unaitumia zaidi katika mawasiliano?

9. (A) Kiswahili [ ] (B) Kihaya [ ]

10. Je, uwapo shuleni, ni lugha ipi huwa unaitumia zaidi katika mawasiliano?

    (A) Kiswahili [ ] (B) Kihaya [ ]

11. Ni eneo lipi huwa unatumia lugha ya Kihaya sana kuliko lugha ya Kiswahili

    (A) Eneo la ibada [ ] (B) Sokoni [ ]

    (C) Msibani [ ] (D) Sherehe [ ]

12. Ni eneo lipi huwa unatumia lugha ya Kiswahili sana kuliko lugha ya Kihaya

    (A) Eneo la ibada [ ] (B) Sokoni [ ]

    (C) Msibani [ ] (D) Sherehe [ ]

13. Taja maneno 10 ambayo kila wakati ukiyatamka, mwalimu huwa anakurekebisha katika kutamka.

    (A)……………………….……….. (B) …………….……………

    (C) ……………………………… (D) …………………………….

    (E) ………………….…………… (F) …………..…………………

    (G) ……………………..……….. (H) …..…………………………

    (I) ……………………...…………… (J) ……...………………………

14. Je kuna ugumu wowote unaokutana nao unapojifunza lugha ya Kiswahili? kama upo tafadhali utaje,

    ……………………………………………………………………………………

    ……………………………………………………………………………………

    …………………………………………………………………….……………

15. Je, mwalimu huwa unatumia mbinu zipi kukurekebisha pale unapokosea kutamka vizuri matamshi ya kiswahili?

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………….……………

16. Soma maneno yafuatayo katika jedwali **A – I**

**Jedwali A**

| **Neno** | **Waliotamka vizuri** | **Waliokosea kutamka** |
|---|---|---|
| Dharau | | |
| Ng'ombe | | |
| Thamani | | |
| Kijana | | |
| Karanga | | |
| Shule | | |
| Mzee | | |
| Ghorofa | | |
| Nzuri | | |
| Hatari | | |
| **Jumla** | | |

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**Kiambatisho Namba 4: Mahojiano - Walimu**

Habari mpendwa mtafitiwa, Mimi ni **Asimwe Abel**, mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti kuhusu ***"Athari za kifonolojia za lugha ya Kihaya katika kujifunza lugha ya Kiswahili"***. Kwa heshima kubwa, ninakuomba muda wako ili uweze kujaza hojaji hili. Tafadhali jaza hojaji hii kadiri unavyojua au kulingana na uzoefu wako mwenyewe bila ya kumhusisha mtu mwingine. Kila taaria itakayotolewa hapa itatumika kwa ajili ya kitaaluma tu na si vinginevyo.

**SEHEMU B: TAARIFA BINAFSI ZA MTAFITIWA**

1. Miaka yako (a) 18- 25 [ ] (b) 26- 30 [ ]
   (c) 31-40 [ ] (d) 41-50 [ ]
   (e) 51 na zaidi [ ]
2. Jinsia (a) Me [ ] (b) Ke [ ]
3. Kiwango cha elimu (a) Sijasoma [ ] (b) Msingi [ ]
   (c) Sekondari [ ] (d) Chuo [ ]

**SEHEMU C: WEKA ALAMA YA (√) KWENYE HERUFI AMBAYO UNAFIKRIA NI SAHIHI PENYE MABANO [ ]**

4. Je, wewe ufanya kazi katika wilaya ya Misenyi?
   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]
5. Je, wewe ni miongoni mwa watu wanaotokea katika kabila la Kihaya?
   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]
6. Kama swali (5) ni "Ndiyo", je Kihaya ni lugha yako ya kwanza kwako?
   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

7. Je unafahamu kuongea lugha ya Kihaya?

   (A) Hapana [ ] (B) Ndiyo [ ]

8. Uwapo katika maingira ya nyumbani ni lugha ipi huwa unaitumia zaidi katika mawasiliano?

   (A) Kiswahili [ ] (B) Kihaya [ ]

9. Je, uwapo shuleni, ni lugha ipi huwa unaisikia zaidi wanafunzi wakiwasiliana wao kwa wao?

   (A) Kiswahili [ ] (B) Kihaya [ ]

10. Ni eneo lipi huwa lugha ya Kihaya huwa inatumika sana kuliko lugha ya Kiswahili

    (A) Eneo la ibada [ ] (B) Sokoni [ ]

    (C) Msibani [ ] (D) Sherehe [ ]

11. Ni eneo lipi huwa lugha ya Kiswahili huwa inatumika sana kuliko lugha ya Kihaya

    (A) Eneo la ibada [ ] (B) Sokoni [ ]

    (C) Msibani [ ] (D) Sherehe [ ]

**SEHEMU D: JAZA TAARIFA ZAKO SEHEMU PALIPO NA NAFASI**

12. Andika maneno walau 10 ya lugha ya Kihaya ambayo wanafunzi hupenda kuyatamka wakiwa shuleni

    (C) …………………….……….. (B) …………….……………

    (C) ………………………………… (D) …………………………….

    (E) ……………….……………… (F) …………..…………………

    (G) ……………………..……….. (H) …..…………………………

    (I) …………………...…………… (J) ……...………………………

13. Taja maneno 10 ya lugha ya Kiswahili ambayo wanafunzi huyatamka kimakosa.

| | |
|---|---|
| (A)……………………….……….. | (B) …………….…………… |
| (C) ……………………………… | (D) ……………………………. |
| (E) ……………….……………… | (F) …………..………………… |
| (G) ……………………..……….. | (H) …..………………………… |
| (I) …………………...…………… | (J) ……...……………………… |

14. Je kuna ugumu wowote unaokutana nao unapofundisha wanafunzi wa Kihaya darasani hasa katika utamkaji wa maneno ya Kiswahili? kama upo tafadhali eleza,

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………….……………

15. Je, kama mwalimu huwa unatumia mbinu zipi kuwarekebisha wanafunzi pale wanapokosea kutamka vizuri matamshi ya kiswahili?

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………….…………

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**Kiambatanisho 5: Barua ya Ruhusa ya Kukusanya Data**

**THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA**

***DIRECTORATE OF POSTGRADUATE STUDIES***

P.O. Box 23409
Dar es Salaam, Tanzania
http://www.openuniversity.ac.tz

Tel: 255-22-2668992/2668445
ext.2101
Fax: 255-22-2668759
E-mail: dpgs@out.ac.tz

**Our Ref: PG201702411**

Date: 2nd November 2018

District Officer,

P.o.Box 33,

Kyaka Misenyi.

**RE: RESEARCH CLEARANCE**

The Open University of Tanzania was established by an act of Parliament No. 17 of 1992, which became operational on the 1st March 1993 by public notice No. 55 in the official Gazette. The act was however replaced by the Open University of Tanzania charter of 2005, which became operational on 1st January 2007. In line with the later, the Open University mission is to generate and apply knowledge through research.

To facilitate and to simplify research process therefore, the act empowers the Vice Chancellor of the Open University of Tanzania to issue research clearance, on behalf of the Government of Tanzania and Tanzania Commission for Science and Technology, to both its staff and students who are doing research in Tanzania. With this brief background, the purpose of this letter is to introduce to you **Ms.Asimwe Abel, Reg No:PG201702411** pursuing Master of Arts in Kiswahili **(MA-KISWAHILI).**We here by grant this clearance to conduct a research titled ***"Kuchunguza Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kihaya katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.*** 'She will collect her data in Kagera Region from 05thNovember 2018 to 5th December 2018.

In case you need any further information, kindly do not hesitate to contact the Deputy Vice Chancellor (Academic) of the Open University of Tanzania, P.O. Box 23409, Dar es Salaam. Tel: 022-2-2668820.We lastly thanks you in advance for your assumed cooperation and facilitation of this research academic activity.

Yours sincerely,

Prof. Hossea Rwegoshora
**For: VICE CHANCELLOR**
**THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA**

**Kiambatanisho 6: Barua ya Ruhusa ya Afisa Elimu ya Kukusanya Data**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI**

***Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji***

**Simu: 028 732983531**
**Faksi: 028 732983307**

S.L.P. 38,
**KYAKA.**

HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI

**Unapojibu tafadhali taja :**
**Kumb.Na. KGR/MSY/E.1/14/VOL.IV/8**

08/11/2018.

Walimu wakuu,
Shule za Msingi,
**Kata ya Minziro.**

**YAH: MWANACHUO ASIMWE ABEL KUFANYA UTAFITI KATIKA SHULE ZENU**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

Ofisi imepokea barua ya mwanachuo wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) **Asimwe Abel** mwenye namba ya usajili **No. PG 201702411** kuomba kufanya utafiti katika shule zenu.

Kwa barua hii ofisi inamtambulisha rasmi kuwenu mpeni ushirikiano.

Nawatakia utekelezaji mwema,

Alfred B. Maijo,
**KAIMU AFISA ELIMU (W),**
**MISSENYI.**

AFISA ELIMU WA WILAYA
MISSENYI

Nakala Afisa Elimu,
**Kata ya Minziro.**

Position: 12
Operator: 0x
Error: IllegalTag
Subsystem: KERNEL
PCL XL error